**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Thelathini na Saba - Tarehe 28 Julai, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza nieleze ratiba ya leo kwamba tunakusudia kuendelea na shughuli zilizoko kwenye *Order Paper* na tujitahidi kuzimaliza ifikapo saa 7 ili tutakaporudi saa 11 itakuwa ni nafasi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa hotuba ya kuhitimisha Mkutano wa 20 wa Bunge na vile vile kuna mabadiliko katika *Order Paper* ya leo haikuandikwa kwenye *Order Paper* sasa naomba tuongeze kwamba baada ya Maswali kutakuwa na Kauli za Mawaziri, Kauli ambayo itatolewa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Sasa Kikao cha 37 cha Mkutano wa 20 kinaanza, agenda za leo Katibu.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Hifadhi za Taifa Tanzania kwa mwaka 2003/2004 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania National Parks for the year 2003/2004).*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Taarifa ya mwaka na Hesabu za Dhamana za Uwekezaji Tanzania kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2004 *(The Annual Report and Accounts of the Unit Trust of Tanzania for the year ended 30th June, 2004).*

Hati ya Uhamishaji Fedha Na. 3 ya mwaka 2004/2005 *(Statement of Reallocation Warrant No. 3 of 2004/2005).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 353

**Maendeleo Vijijini na Uwezeshaji Wananchi**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika mkutano wa 16 wa Bunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa alilithibitishia Bunge kuwa Wizara yake imeshajipanga kufanya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Vijijini na kwa kuwa katika mkutano huo wa Bunge, Waziri Mkuu alizindua rasmi Sera ya Uwezeshaji wananchi:-

(a) Je, kuna tofauti gani au mahusiano gani kati ya sera hizo mbili?

(b) Je, ni kwa kiasi gani Sera hiyo ya Maendeleo Vijijini itagusa maendeleo endelevu ya Watanzania maskini hasa katika kuboresha makazi, ongezeko la kipato na kadhalika na ina mtazamo gani wa kijinsia utakaonufaisha wanawake na watoto ambao hawashirikishwi kwenye maendeleo vijijini?

(c) Je, ni kwa kiwango gani wananchi hao wamehamasishwa katika kushiriki na kuielewa vema sera hiyo ili kuifanyia utekelezaji yakinifu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge wa Viti Maalum, lenye (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sera ya Uwezeshaji ni mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wa wananchi katika sekta zote. Kuwepo kwa sera hii ni matokeo ya ubinafsishaji ambao kwa sehemu kubwa wananchi wa kawaida hawakushiriki ipasavyo kwa kuwa hawakuwa na elimu ya biashara, ujuzi na mitaji. Moja ya matokeo ya Sera ya uwezeshaji ni mkakati wa kurasilimisha rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA). Walengwa wa Sera ya Uwezeshaji ni wananchi na Makampuni yao yatakuwa ni yale yaliyosajiliwa nchini ambayo walengwa wanamiliki asilimia isiyopungua hamsini ya hisa zote za makampuni hayo. Vile vile, kutambuliwa makazi yaliyojengwa kiholela kwa kuwapatia wenye nyumba leseni za makazi ni njia mojawapo ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kwani leseni hizo zinaweza kutumika kupatia mikopo.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maendeleo Vijijini imebuniwa ili kuhakikisha kwamba wananchi na wadau wote muhimu wanashirikishwa kwa ujumla katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kupambana na umaskini hasa katika maeneo ya vijijini ambako zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanaishi.

Malengo makuu ya Sera ya Maendeleo Vijijini ni pamoja na kuwezesha ukuaji mpana wa uchumi unaohusisha sekta zote, kuongeza fursa na upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi vijijini, kupunguza majanga vijijini na kuwezesha utawala bora. Kwa ujumla Sera zote hizi mbili zinalenga kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025.

(b) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Vijijini utahusisha uratibu wa utekelezaji wa Sera na Mikakati ya kisekta katika ngazi ya kijiji na utashirikisha wadau wote wakiwemo wanawake na vijana ambao hawakuwa wakishirikishwa kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Ushirikishwaji huu utafanyika kupitia Mfumo wa Upangaji wa Mipango wa Fursa na Vikwazo vya Maendeleo ambapo katika moja ya hatua za mchakato wa mfumo huo ni kushirikisha jamii katika makundi tofauti kulingana na umri na jinsia na hivyo kuwawezesha kutambua fursa na vikwazo vilivyopo. Ni katika hatua hii ambapo makundi yataibua miradi yao ya maendeleo inayolenga kuboresha hali duni ya maisha.

(c) Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha wananchi walio wengi kuielewa vema Sera ya Maendeleo vijijini na kuitekeleza kikamilifu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imetafsiri sera hii katika lugha ya Kiswahili ili ieleweke kwa urahisi. Nakala za Sera hii zitasambazwa katika ngazi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau mbalimbali. Aidha, warsha zitaandaliwa kwa Watendaji mbalimbali kwa lengo la kuwaelimisha ili kufanikisha utekelezaji wake.

Na. 354

**Malipo ya Wazee wa Mabaraza**

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imejizatiti sana katika ukusanyaji wa mapato ya kuendeshea shughuli zake kutoka shilingi bilioni 25 kwa mwezi, mwaka 1995/1996 hadi wastani wa shilingi 150 bilioni kwa mwezi hivi sasa na kwa kuwa, Serikali imekuwa ikizielekeza fedha hizo katika sekta muhimu za uchumi wetu kama ujenzi wa barabara za lami, uboreshaji wa huduma za jamii – mipango mahususi ya elimu na afya, mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda kwenye miji ya Kahama na Shinyanga, kuajiri kwa masharti ya kudumu Watendaji wa Vijiji na Kata, kulipa malimbikizo ya madeni ya walimu na kadhalika:-

(a) Je, Serikali itatatua lini tatizo la muda mrefu la malipo kwa wazee wa Mabaraza, kama wale wa Ushetu, Ukune, Mpunze, Kilago, Bulungwa, huko Wilayani Kahama?

(b) Je, uko wapi utaratibu/ratiba ya kuwalipa posho Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji ambao ndio wanaokaa na watu wengi na ni vitovu vya misingi ya maendeleo ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mbunge wa Kahama lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, swali hili linahusiana na malipo ya posho ya wazee wa mabaraza. Kwa bahati mbaya Mheshimiwa Mbunge hakueleza ni wazee wa mabaraza gani anayozungumzia kwa vile wazee wa mabataza wako wa aina mbalimbali ikiwa ni pamoja na wazee wa Mahakama za Mwanzo, Wazee wa Mabaraza ya Ardhi na Wazee wa Mabaraza ya Kata.

Hata hivyo kwa kuzingatia maelezo ya swali ni dhahiri kuwa Mheshimiwa Mbunge alikusudia kuulizia wazee wa Mabaraza ya Kata.

Mheshimiwa Spika, Mabaraza ya Kata yameanzishwa kwa Sheria ya Mabaraza ya Kata *(The Ward Tribunals Act No. 7/1985)* ambapo kila Kata inatakiwa kuwa na Baraza moja.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya kuanzishwa mabaraza haya ni pamoja na:-

(i) Kupunguza mlundikano wa kesi katika Mahakama za Mwanzo.

(ii) Kushirikisha jamii katika kutatua migogoro inayoikabili jamii husika.

(iii) Kutunza amani na utengemano miongoni mwa watu na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kanuni na msingi mkuu unaotawala wadhifa huu wa ujumbe wa mabaraza ya Kata ni kwamba wadhifa huu ni wa kujitolea na siyo wa ujira.

Hata hivyo Serikali imeweka utaratibu wa malipo ya posho kwa wazee wa mabaraza ambapo kwa mujibu wa kifungu cha 27 cha Sheria ya Mabaraza ya Kata, Kamati za Maendeleo ya Kata zinatakiwa kutoa mapendekezo ya aina na kiasi cha posho zitakazolipwa kwa Wazee wa Mabaraza. Mapendekezo hayo hujadiliwa na kuidhinishwa na Halmashauri husika.

Hivyo napenda kuchukua nafasi kumshauri Mheshimiwa Mbunge kuliwasilisha suala hili katika Halmashauri ya Wilaya ya Kahama na nina imani Halmashauri italitolea

ufumbuzi suala hili kwa kuandaa utaratibu wa kuwalipa wajumbe wa Mabaraza ya Kata katika Halmashauriya Wilaya ya Kahama.

(b) Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wamo katika kundi la Viongozi wa jamii *(Civic Leader)* na kwamba vyeo hivyo siyo ajira ndiyo maana moja ya sifa za viongozi hao ni kuwa na kipato halali kinachomwezesha kuishi.

Hata hivyo, Serikali kwa kutambua umuhimu wao katika kuhamasisha maendeleo katika maeneo yao ilitoa utaratibu wa kuwalipa posho viongozi hao. Utaratibu huo umeelezwa katika Tangazo la Serikali Namba 3 na 4 la mwaka 1993 ambapo kila Mwenyekiti anatakiwa kulipwa posho ya asilimia tatu (3) ya makusanyo aliyohamasisha katika eneo lake.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa baadhi ya kodi zimefutwa Ofisi yangu imeshatoa maelekezo kwa Halmashauri kutenga kiasi cha fedha zinazotokana na ruzuku ya kufidia vyanzo vya mapato vilivyofutwa ili kuwalipa posho wenyeviti hao.

Na. 355

**Tatizo Sugu la Mji wa Hale**

**MHE. JOEL N. BENDERA** alijibu:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu mji wa Hale umekuwa na tatizo sugu la maji na Serikali kwa kuliona tatizo hilo walitoa fedha za kuchimba kisima kirefu ili kupata maji lakini jambo la kusikitisha ni kwamba, sasa ni zaidi ya miaka mitatu tangu fedha hizo zitolewe na hadi leo hii maji hayajapatikana na kwa kuwa nimekuwa nikiulizia juu ya tatizo hilo kwa wataalam wa Maji Wilayani, Mkoani na hata Wizarani na kuahidiwa tu kuwa tatizohilo litapatiwa ufumbuzi na kwamba nisiwe na wasiwasi na kwamba matatizo madogo madogo ya kiufundi yatakapomalizika maji yatapatikana Hale:-

(a) Wananchi wanataka kufahamu hivi je, ni sababu gani zinazofanya mradi huo usikamilishwe kwa zaidi ya miaka mitatu sasa?

(b) Kwa kuwa kulikuwepo na ahadi kuwa maji hayo sasa yatatoka katika Kijiji cha Segera, je, mradi huo umeishia wapi?

(c) Wananchi wanataka kujua maji watayapata lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba mwaka 2002/2003, Serikali ilitoa kiasi cha shilingi 27 milioni kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji mjini Hale. Sehemu ya fedha hizo ilitumika kuchimbia kisima kirefu, lakini maji hayakupatikana. Kutokana na hali hiyo, Serikali iliamua kutumia maji ya mto Pangani. Kazi zilizokwishafanyika hadi sasa ni pamoja na kujenga kituo cha kusukuma maji, kuchimba udongo na kujaza mawe kwenye mfereji wa kuchepua maji, kuchimba kisima (sampu) kwa ajili ya kuhifadhi maji, na kununua mabomba ya maji. Kazi zilizobaki ili kukamilisha mradi huo ni pamoja na kuongeza kina cha sampu ya kuhifadhi maji, kujenga kibanda cha kuwashia pampu ya maji, kuvuta umeme hadi kwenye kibanda, kukamilisha uchimbaji na kujaza mawe kwenye mfereji na kufunga pampu.

(b) Mheshimiwa Spika, kijiji cha Segera kinapata maji kutoka mto Pangani kwa kutumia pampu ambayo inasukuma maji hayo hadi kwenye tanki lililoko juu ya kilima. Maji hayo husambazwa kwenda katika vijiji vya Segera, Michungwani na Kabuku, kwa mtiririko. Kutokana na udogo wa pampu, maji yanayofika katika vijiji vya Michungwani na Kabukuni kidogo na hayakidhi mahitaji ya vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, umbali kutoka Segera hadi Hale ni kilometa 12, ambao ni mrefu kuliko ule wa meta 150 tu wa kuchepua maji ya mto Pangani katika eneo la Hale. Hivyo Serikali ilona kuna unafuu wa gharama kwa kuchepua maji ya mto Pangani katika eneo la Hale kuliko kuvuta maji ya mto huo. Kwa bahati nzuri mradi huu umekwishaanza kutekelezwa na wananchi wa Hale wataweza kunufaika.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la kipengele (b), Serikali imeanza kutekeleza mradi wa kuwapatia maji wananchi wa mji wa Hale na vitongoji vyake, kwa kujenga mradi mpya utakaotumia maji ya mto Pangani. Naamini mradi huu utakamilika hivi karibuni ili wananchi wa maeneo hayo waweze kumaliza kabisa kero ya maji.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza nipongeze juhudi za Serikali kwa kuweza kuchepua maji kutoka katika Mto Pangani baada ya kuona kwamba kila wanapochimba hawapati maji Hale. Nawapongeza sana. Lakini niiombe Serikali basi kwamba kwa sababu mradi huu ni wa muda mrefu, basi Serikali iongeze fedha pale ili wananchi wa Hale wanywe maji kwa sababu ni mradi ambao umechukua muda mrefu na unaleta matatizo na hasa kufikia matatizo ya kisiasa? Naomba hilo.

Swali la pili, ni ombi tu kwamba kwa kuwa tatizo la maji katika mji wa Korogwe linafanana kabisa na ilivyo katika mji wa Hale. Na kwa muda mrefu tumekuwa tukiomba kupata maji kutoka *HTM Tabora* na Wizara imekuwa ikitoa majibu ya matumaini lakini mpaka leo bado. Je, Serikali itasemaje kuhusiana na hilo hasa ikizingatia kwamba tumeingia kwenye mradi wa Benki ya Dunia wa kupata maji ili vijiji vyote sasa vinavyohusiana na Korogwe pamoja na vitongoji vyake vipate maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napokea shukrani zake kwa juhudi ambazo Serikali

imezifanya. Lakini juhudi hizo siyo za Serikali peke yake ni pamoja na Mheshimiwa Mbunge ambaye amekuwa akifuatilia sana. *(Makofi)*

Pili, kuhusu mradi wa kutoka *HTM* eneo la Tabora kwenda mjini Korogwe. Mradi huu ambao pia unahusisha kama kilometa 12 kutoka Kituo cha kusafisha maji cha Tabora, Wizara yangu imekuwa ifuatilia ni jinsi gani ambavyo tunaweza kutekeleza mradi huo bila kuathiri upande wa pili wa bomba ambalo linakwenda Handeni.

Kwa hiyo, kwa kipindi kirefu *study* zimeshafanyika lakini gharama hizo nina hakika Mheshimiwa Mbunge kwa vile alikuwa anafuatilia kwa ukaribu sana, anaelewa kwamba Serikali ilikuwa ikitenga mafungu kwa ajili kwanza ya kufanya mradi wenyewe ufanye kazi inavyotakiwa. Kwa sababu mpaka hivi karibuni umeme ulikuwa umekatwa sehemu hizo baada ya nyaya za umeme kuibiwa. Kwa hiyo, Serikali ilisikia kilio cha Mheshimiwa Mbunge na nina hakika kwamba matatizo ya wananchi wa Korogwe yatatulika tu mara baada ya miradi hii miwili kukamilika. Nina hakika Mheshimiwa Bendera inshallah urudi tena nina hakika tutatekeleza pamoja, pamoja na Serikali. *(Makofi)*

**MHE. ADELASTELA E. MKILINDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo Mheshimiwa Waziri aliyoyasema, mimi bado naona Watanzania walio wengi tunaingia kwenye awamu ya nne ya uongozi tukiwa na kiu kubwa ya kutaka maji salama na safi na kwa kuwa kule vijijini kuna miradi mingi ya maendeleo ambayo haitekelezeki kwa kukosa maji ikiwemo ile ya afya kupambana na kipindupindu, kumpa nafasi mwanamke ili aweze kuzalisha badala ya kuendea maji kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba Wizara yake imekuwa kero kwa muda mrefu na kwa kuwa sasa kwa vile tunamaliza awamu hii akiri mbele ya Watanzania kwamba Wizara yake imekuwa kikwazo kwa Wizara nyingine kutimiza malengo yake ya muda mrefu na mfupi tuliyojiwekea? Ahsante Mheshimiwa Spika. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kulingana na takwimu zinaonyesha kwamba Tanzania tuko mbele kwa kusambaza maji vijijini. *(Makofi)*

Sasa hivi tunakimbilia asilimia 55 ambapo majirani zetu Kenya wako kwenye asilimia 44, Uganda wako chini zaidi. Sasa kitakwimu siwezi kuelewa Mheshimiwa Mbunge ametoa wapi, amesema kwamba sisi hatufanyi vizuri na tunakuwa kero kwa Wizara nyingine. Na kuwa kero kwa Wizara nyingine ina maana kwamba sisi tunaonekana kama ni tatizo, kitu ambacho si sahihi. Na nikizingatia Mheshimiwa Mbunge kwamba anatoka upande wa pili siasa, inawezekana tu anatania kwa sababu Wizara yetu tunafanya kazi vizuri na kambi ya upinzani walitushukuru wakati tunawakilisha Bajeti yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, naomba niongezee kidogo majibu mazuri sana ya Naibu Waziri kwa swali la Mheshimiwa Mkilindi. Mimi nadhani yeye ndiyo kero. *(Kicheko/Makofi)*

Ni kero kwa sababu anashindwa kutambua kazi nzuri iliyofanyika katika kipindi cha miaka mitano cha uongozi wa CCM. Tumeeleza hapa, ametoa *statistics* nzuri sana za kuonyesha kwamba tumefanya kazi mzuri inayokubalika. Inahitaji mtu mwenye kero wa aina ya Mbunge huyu ndiyo asitambue kazi yetu mzuri tunayoifanya. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 356

**Kifuta Machozi kwa Ndugu za watu Waliouawa na Wanyamapori**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni Serikali ilitoa kifuta machozi kwa baadhi ya ndugu za watu waliouawa na wanyamapori katika Wilaya ya Liwale lakini haikutoa chochote kwa wale waliojeruhiwa na wanyamapori hao:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwasaidia pia hao wananchi waliojeruhiwa na wanyamapori hasa wale waliopata ulemavu na hivyo kushindwa kufanya shughuli zao kama ilivyokuwa kabla ya kupata ulemavu huo?

(b) Kwa kuwa, wapo majeruhi wa aina hiyo katika Wilaya ya Liwale na wanaendelea kujigharimia kwa matibabu ambayo ni ya gharama kubwa na baadhi yao hawazimudu gharama hizo je, Serikali inawasaidiaje hao katika kukabiliana na gharama hizo kubwa za matibabu?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Wilaya ya Liwale ina utajiri mkubwa wa rasilimali ya wanyamapori. Kutokana na uwindaji wa kitalii, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale imekuwa ikipata asilimia 25% ya mapato yatokanayo na uwindaji huo ambayo kwa kipindi cha miaka 7 iliyopita kuanzia mwaka 1996, Wilaya hii ilipata jumla ya shilingi za Tanzania 156,479,855.00.

Fedha hizo zilitumika kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya wananchi wa Liwale.

Mheshimiwa Spika, kuna sababu mbalimbali zinazopelekea wananchi kujeruhiwa au kuuawa na wanyamapori wakali. Baadhi ya sababu hizo ni pamoja kama ifuatavyo:-

Wananchi kuishi au kuendesha shughuli zao karibu na maeneo yenye wanyamapori. Mara nyingi makazi hayo ni duni na ya muda.

Utafiti wa simba uliofanyika mwaka 2005, umegundua kwamba baadhi ya wananchi wanajeruhiwa au kuuawa na wanyama wakali kwa kuwa wana tabia ya kutembea usiku wakiwa wamelewa.

Uvamizi wa maeneo ya wanyamapori na kuwepo kwa mifugo karibu au ndani ya hifadhi. Aidha wapo baadhi ya wananchi wanaovamia maeneo ya wanyamapori au yaliyo karibu na hifadhi ya wanyamapori kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kuwapa pole wananchi waliojeruhiwa na wanyamapori wakali. Wizara yangu haina utaratibu wa kutoa kifuta machozi kwa wananchi wanaojeruhiwa au kupata ulemavu kutokana na wanyama wakali kwa sababu zifuatazo:-

Mwingiliano wa makazi ya wanyamapori, wakiwemo simba, chui, fisi na nyoka na yale ya binadamu, unachangia kuwepo kwa ongezeko kubwa la matukio ya wananchi kujeruhiwa na wanyamapori.

Aidha, mtawanyiko wa wanyamapori ni mkubwa kitendo kinachofanya suala hili kuwa gumu na la gharama kubwa kwa Serikali.

Serikali inasimamia uhifadhi wa wanyamapori kwa kutumia Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1974. Aidha, Sheria hiyo inatoa uwezo kwa wananchi kuchukua hatua ya kuua mnyama mkali anaposababisha uharibifu kwa maisha au mali ya wananchi. Kwa hiyo, ni wajibu wa kila mwananchi kuchukua tahadhari ya kujilinda kutokana na madhara yanayoisababishwa na wanyama wakali.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kusaidia kugharamia matibabu kwa majeruhi. Wizara yangu haina utaratibu wa kugharamia matibabu kwa majeruhi kutokana na wanyama wakali. Kwa kuwa Wizara ya Afya na utaratibu wa kutoa matibabu kwa wananachi wasio na uwezo wa kujigharmia, nashauri majeruhi kutokana na wanyama wakali watumie fursa hiyo kulingana na utaratibu uliowekwa na Wizara hiyo.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, anaweza akatoa kilevi gani ambacho wana Liwale huwa wanatumia baadaye wanaathirika na wanyamapori?

Kwa kuwa ninachoelewa mimi hivi sasa ni kwamba wanyamapori hasa tembo wanashambulia sana mikorosho na wanakula mabibo, wakishakula mabibo huwa wanachanganyikiwa na wanalewa ndiyo wanaowaua wananchi wa Liwale. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Swali la pili, hii asilimia 25 inayozungumzwa tangu wakati ule imebakia asilimia 25, na umekiri katika maelezo yako kwamba Liwale kuna wanyama wakali wengi na kwamba wamezagaa Liwale nzima. Je, hii asilimia 25 kwanini isiongezwe kwa asilimia 30 au 35 ili tuweze kumudu matatizo yaliyoko yanayotokana na wanayama pori kule Liwale?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa spika, kwanza kabisa nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Kigwalilo kwamba kwa muda wa miaka yote mitano amekuwa karibu sana na wananchi wake ambao wapiga kura. Amefuatilia kabisa masuala mbalimbali kuhusu hasa wananyama pori, suala la tembo kuingia katika maeneo haya kama vile suala la simba, tumewahi kusema kwamba kwa kweli katika nchi yetu tembo wamekuwa wengi hivi sasa, kutokana na uhifadhi lakini pia kutokana na ushirikishaji wa wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nimetoa tarakimu hapa wakati wa bajeti kwamba tembo wamekuwa kutoka kama 50,000 mpaka zaidi ya 100,000.

Mheshimiwa Spika, lakini sera ya wanyama pori hivi sasa inazungumzia uundaji wa maeneo ambapo wananchi wenyewe katika vijiji watasimamia au tunaita WMS na katika WMS tunaamini kabisa kwamba wananchi wenyewe wataamua ni jinsi gani ambavyo wanyama pori ambao wakali lakini wataweza kuwatumia katika shughuli mbalimbali za kiutalii na kwa maana hiyo kuongeza kipato kwa wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika suala la asilimia 25 tumekuwa tunalitoa ni kweli kwa muda mrefu na limekuwa kwa kweli linasaidia sana maendeleo ya wananchi, hili ni wazo ambalo ni la Mheshimiwa Mbunge amelitoa.

Lakini pia Serikali inapenda kusisitiza kwamba asilimia 25 itumike vilivyo kwenye Halmashauri zetu, kwa sababu mara nyingine kwamba fedha hizi hazitumiki vilivyo mara nyingine zinatumika kwa ajili ya vikao vya madiwani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinatakiwa zitumike kwa maendeleo asilimia 60 zitumike angalau kwa uhifadhi na asilimia 40 zitumike kwa ajili ya maendeleo na naamini kabisa kwamba fedha hizi zikitumika hivyo basi wananchi wataweza kunusurika na wanayama pori hao waliokuwepo.

Na. 357

**Ajali za Barabarani**

**MHE. OMAR S. CHUBI** aliuliza:-

(a) Je, ni ajali ngapi za barabarani zilizohusisha mabasi ya abiria zimetokea tangu Januari, 2003 hadi Novemba, 2004 ikitaja jina la mmiliki wa basi, tarehe ya ajali iliyotokea, idadi ya abiria waliojeruhusiwa na kulazwa hospitali na idadi ya abiria waliofariki kwa kila tukio?

(b) Katika siku za miaka ya nyuma Serikali ilikuwa ikitoa salamu za rambirambi kwa kila ajali inapotokea; lakini cha kushangaza ni kuwa Serikali imekaa kimya kwa ajili ya lori iliyotokea Novemba mwaka 2004

na kuua watu 26 na wengine 27 kujeruhiwa huko Tabora; je kwa nini utamaduni huo uliachwa?

(c) Je, chanzo cha ajali hiyo ni nini na wahusika wamechukuliwa hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Chubi, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kati ya Januari, 2003 hadi Novemba, 2004 ajali zilizohusisha mabasi ya abiria ni kumi na saba (17). Ajali hizo zilisababisha vifo vya watu 165 na kujeruhui watu wengine 740. Ajali hizi za mabasi ya abiria zilitokea sehemu mbalimbali nchini na kwa tarehe mbalimbali. Taarifa zaidi juu ya majina ya wamiliki wa kila basi, tarehe na mahali kila ajali ilipotokea na idadi ya abiria waliofariki na waliojeruhiwa, imeambatishwa na tutamkabidhi Mheshimiwa Mbunge muda mfupi ujao.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali ina utamaduni wa kutoa rambirambi kila ajali inapotokea, na Serikali haijaacha utamaduni huo. Pamoja na kutoa salamu za rambirambi, viongozi mbalimbali wa kitaifa, Mkoa, Wilaya na kadhalika huwa na utamaduni wa kufika eneo la ajali na kuwafariji waliofiwa na kusimamia huduma za majeruhi. Kwa mfano katika tukio alilolitaja Mheshimiwa Mbunge lililotokea tarehe 2/11/2004 katika barabara kati ya Uyui na Sikonge eneo la Mto Wala, Viongozi wa Mkoa walifika eneo la tukio na walitoa salamu za pole kwa wafiwa.

(c) Mheshimiwa Spika, ajali hiyo iliyohusisha lori lenye usajili Na. TAT 758 ilisababishwa na mwendo wa kasi wa gari hilo ambalo ilijaza mizigo pamoja na abiria ambapo ambapo dereva alishindwa kumudu gari akiwa karibu na daraja, na taa za mbele kuzimika na kusababisha kugonga kingo za daraja na kisha likatumbukia mtoni. Mizigo iliyokuwemo ndani ya gari iliwaangukia abiria na hivyo ilisababisha vifo vya watu wengi (26) na wengine 27 walijeruhiwa.

Hivyo mwendo wa kasi wa gari pasipo dereva kuzingatia alama za barabarani ndiyo chanzo hasa cha ajali ya gari hiyo. Dereva aliyesababisha ajali hii alikamatwa na kufunduliwa mashtaka; na hivi sasa kesi inaendelea Mahakamani.

**MHE. OMAR S. CHUBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru pamoja na kazi nzuri zinazofanywa na kitengo cha usalama barabarani. Je, Waziri akafanya mpango wa kupeleka baadhi ya askari wajifunze kama *South Africa* hasa kwenye mabasi kuanzia Mbabane, *Darban, Port Elizabeth, Cape Town* mpaka *Johannesburg* na kumalizia wajifunze Namibia?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, wazo la Mheshimiwa Mbunge ni wazo nzuri kwamba ma-*traffic* wetu wapate nafasi ya kwenda nchi zingine wajifunze wenzao wanavyofanya ni wazo nzuri pindi Wizara yangu

ikipata uwezo kwa maana ya fedha za kuwapeleka ma-*traffic* kwenda kusoma kama tunavyopeleka polisi wa idara zingine kule nje hatutasita vilevile na hawa *traffic* kuwapeleka wakasome nchi za nje.

Na. 358

**Ujazo Sahihi wa Mazao Katika Gunia**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Ushirika na Masoko inao wajibu wa kudumisha Ushirika nchini na kuhakikisha upatikanaji wa masoko kwa mazao ya mkulima na kuhakikisha vipimo sahihi ya ujazo wa mazao katika magunia vinasimmamiwa ipasavyo na wakulima wanatumia vipimo hiyo kuliko mtindo wa sasa wa ujazo maarufu kama Lumbesa:-

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba, mtindo wa Lumbesa unaotumiwa na wafanyabiashara wengi nchini wa kujaza mazao kama mahindi, vitunguu, alizeti, viazi n.k. unawaumiza sana wakulima?

(b) Kama Serikali inafahamu kuwa mtindo huo ni mbaya, itakuwa tayari kuanzia sasa kutunga sheria (kama haipo sheria ya namna hiyo) ili mazao yote toka kwa wakulima yauzwe kwa kutumia kapani (kilo)?

(c) Je, Serikali haioni kuwa kutoingilia tatizo hilo la mtindo wa lumbesa hakutaisaidia sera nzuri ya Serikali ya kutaka kumuondolea umaskini mkulima mdogo wa nchi hii?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika mkutano wa kumi na saba wa Bunge lako Tukufu wakati nikijibu swali la Na.114 la Mheshimiwa Jackson Makwetta, kuhusu mtindo wa ujazaji wa mazao kwenye maguni ujulikanao kama lumbesa, Serikali haina ushahidi wa kutosha unaoonyesha kuwa ujazo wa lumbesa ni kipimo kinachotumika kununuliwa mazao kutoka kwa wakulima katika magulio. Utafiti uliofanywa na Wizara ya Ushirika na Masoko unaonyesha kuwa ujazaji wa magunia katika mtindo wa lumbesa hufanywa na wafanyabiashara baada ya kununua mazao kutoka kwa wakulima kwa lengo la kupunguza gharama za usafirishaji kwani wenye vyombo vya usafiri mara nyingi hutoza gharama za usafirishaji kulingana na idadi ya magunia na sio uzito wake.

Aidha, wafanyabiashara hao hupendelea kutumia ujazo wa lumbesa kwa lengo la kukwepa kulipa ushuru mkubwa wa Halmashauri za Wilaya kwa kuwa Halmashauri hizo hutoza ushuru wa mazao kulingana na idadi ya magunia na sio uzito.

Mheshimiwa Spika, katika utafiti huo pia, Wizara imebaini kuwa upo udanganyifu ambao hufanywa na wanunuzi wa mazao hasa wale ambao hununulia mazao majumbani aau mashambani kwa kutumia vipimo visivyo rasmi. Vipimo hivyo ni pamoja na mafungu, ndoo, madebe na mizani zisisokuwa sahihi. Kwa kutambua ufanganyifu huo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya imekuwa ikihimiza ununuzi na uuzaji wa mazo yote ya kilimo kufanyika katika vituo vilivyoteuliwa ambapo ukaguzi wa vipimo unaweza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, juhudi hizi za Serikali za kusimamia sheria ya ununuzi wa mazao kwa kutumia vipimo rasmi zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa zaidi katika ununuzi na uuzaji wa mazao makuu ya biashara ambapo Bodi za Mazao zimekuwa zikihakikisha kuwa mazao yote yanauzwa na kununuliwa katika vituo vilivyoteuliwa.

Kwa upande wa mazao mchanganyiko kama yale aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, Serikali inatambua kuwa matatizo bado yapo na ndiyo maana Serikali inahimiza uuzaji wa mazao hayo kupitia vituo vilivyoteuliwa ili iwe rahisi kufanya ukaguzi wa vipimo rasmi.

Hata hivyo katika kuhakikisha kuwa sheria, kanuni na taratibu za ununuzi wa mazao zinafuatwa, Serikali inakamilsha Sera ya Masoko ya Mazao ya Kilimo itakayoambatana na Mkakati wa utekelezaji wake. Sera hiyo itawezesha kufanyiwa marekebisho sheria, kanuni na taratibu za ununuzi wa mazao ili kuondoa kero mbalimbali zinazomkabili mkulima hivi sasa, ikiwa ni pamoja na kupunjwa bei kwa kutumia vipimo visivyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inatambua kuwa wananchi hulazimika kuuza mazao yao kwa bei ya chini na kwa kutumia vipimo visivyo rasmi kutokana na kutokuwepo kwa ushindani wa kutosha wa ununuzi wa mazao katika maeneo yao. Sababu mojawapo inayosababisha kukosekana kwa ushindani katika ununuzi wa mazao ni uduni wa miundombinu ya masoko vijijini hususan barabara za vijijini. Ili kukabiliana na tatizo hilo la uduni wa miundombinu ya masoko vijijini, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya zinatekeleza Programu ya Kuendeleza Mifumo ya Masoko ya Mazao ambayo pamoja na mambo mengine imepanga kuendeleza miundombinu ya masoko katika Wilaya 36 za Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Ruvuma, Iringa, Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Mafanikio yatakayopatikana katika programu hiyo yataendelezwa katika sehemu nyingine nchini kulingana na upatikanaji wa fedha.

Pamoja na uimarishaji wa miundombinu ya masoko, Serikali imeandaa sheria itakayoruhusu matumizi ya Stakabadhi za Mazao Ghalani zitakazotumika kama dhamana ya kupata mikopo kwa wakulima na hivyo kuwawezesha kuhifadhi mazao na kuyauza wakati wa bei nzuri.

**MHE. MGANA I. MSINDAI**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza kwa kuwa sisi Wabunge ndio tunakaa na wananchi kule, na tunaona haya yanafanyika. Nikitoa mfano wa uuzaji wa vitunguu Iramba Mashariki:

(a) Je, Serikali haituamini sisi Wabunge na inataka ushahindi gani?

(b) Kwa kuwa Serikali imesema haina ushahidi, Je, itakuwa tayari wakati wa msimu wa vitunguu na viazi, kwenda Iramba Mashariki, Nzega, Mbeya na Iringa kushuhudia hayo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, sio kwamba Serikali haiamini Wabunge, wala sijasema kwamba hayo yaliyosemwa hayapo, nilichosema katika jibu hapa, nilisema huo utaratibu wa lumbesa upo, lakini ambacho tulikuwa tunasema kwamba hatuna uhakika nacho ni kile kwamba ujazo huo wa lumbesa ndio unatumika rasmi katika kuuzia mazao. Lakini nimekiri kwamba wafanyabiashara binafsi hawa wanayajaza mazao yao katika utaratibu wa lumbesa ili kukwepa gharama mbalimbali ikiwepo na za usafirishaji pamoja na zile ushuru wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka niseme tu kwamba Serikali baada ya kugundua hivyo imefanya utafiti na kuona kwamba tatizo linalokabiliana na jambo hili la kupunjwa kwa wakulima ni lile ambalo linatokana na miundombinu mibovu na ndio maana inachukua hatua mbalimbali za kuweza kuirekebisha, na kwa hiyo nataka tu nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba haya yote ambayo ameyasema tunayafahamu na kwa hiyo hata kutukaribisha tuweze tukasirike wakati wa ununuzi wa vitunguu kule Iramba, sisi tumeshapita kule na kama tutakavyokumbuka nilipokuwa namjibu swali lake lingine tulisema kwamba tutashirikiana naye katika kuanda soko la mazao mchanganyiko katika eneo lake lile la Sekenke.

Na. 359

**Kilimo cha Mboga**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI (k.n.y. MHE. STEPHEN KAZI)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wanaoishi mijini/jijini karibu na maeneo ya mabonde wameanzisha kilimo cha mboga mboga kama vile mchicha, saladi, spinachi, vitunguu, nyanya, kabichi, matikiti maji na kadhalika.

(a) Je, Serikali inalifahamu hilo: na kama inalifahamu, inawatembelea wananchi hao kujionea shughuli zao?

(b) Je, Serikali inawajengea mazingira gani wananchi hao yatakayonuaisha kilimo hicho ili mazao hayo yaongezeke na bei iwe nafuu?

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inafahamu kwamba kuna wananchi wanaoendeleza shughuli za kilimo cha mboga katika maeneo ya mijini iliyouruhusiwa na Halmashauri za Wilaya katika jiji/miji. Jiji la Mwanza lina vikundi 46 vya wakulima vinavyoendesha kilimo cha mboga mchanganyiko. Vikundi hivyo vinaendesha shughuli zao kwa usimamizi wa karibu wa wataalam wa kilimo waliopo kwenye Halmashauri za Wilaya ambao huwatembelea na kuwashauri wakulima juu ya kilimo bora cha mazao hayo.

(b) Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa kushiriana na Halmashauri za Wilaya na wahisani, inasaidia wakulima katika maeneo hayo kuongeza tija, uzalishaji na faida. Kwa mfano:-

- Kati ya mwaka 1998 hadi 2000, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)* na Mpango wa Taifa wa kuzalisha Mali *(National Income Generation Programme-NIGP),* imewasaidia wakulima 3,500 kwa kuboresha miundo mbinu ya umwagiliaji maji mashambani na kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mboga na matunda. Msaada huo uliwalenga wakulima kutoka vijiji vya Luchele, Kishili, Kahama, Nyamwilolekwa, Nyamadoke na Buswelu.

- Kuanzia mwaka wa 202/2003, Wizara inatekeleza mpango wa kuendeleza ukanda wa kijani kuzunguka Ziwa Viktoria ambapo Jiji la Mwanza ni sehemu ya ukanda huo. Kuanzia mwaka wa 2004 hadi 2005, Wizara ya kilimo na chakula imetoa jumla ya pampu za maji 16 kwa ajili ya kusambaza maji katika wilaya za Nyamagana na Ilemela.

- Kati ya mwezi wa Januari hadi Desemba 2004, Serikali ilishirikiana na *Plan International* kuwapatia wakulima wa Tarafa ya Nyamagana zana za kilimo. Zana zilizotolewa kwa wakulima ni pamoja na mapampu ya kunyunyizia madawa na mipira ya kumwagilia maji. Jumla ya wakulima 450 wamefaidika na misaada hiyo.

- Aidha, Serikali inashirikiana na mashirika ya *ACORD* kutoa mikopo nafuu kwa wakulima wa kata ya Ilemela na *CARE International* kutoa pembejeo za kilimo kwa wakulima katika Kata ya Mkolani.

Na. 360

**Kilimo cha Pamba Ukanda wa Kusini**

**MHE. ALI SAID SALIM** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilipiga marufuku kilimo cha Pamba katika mikoa ya kusini kutokana na kuonekana kwa mdudu mharibifu wa zao hilo aitwaje funza Mwekundu kwenye badhi ya vijiji, lakini taarifa ya watafiti waliokwenda kwenye maeneo hayo hawakumwona mdudu huyo kwenye sehemu kadhaa:-

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka kuondoa karantini iliyowekwa ili wananchi wa Mikoa hiyo waruhusiwe kulima pamba.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:

Nilipojibu swali Na. 202 la Mheshimiwa Benson Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, katika kikao cha 21 cha Mkutano wa 20 wa Bunge lako Tukufu, nilieleza kwamba kuanzia mwezi wa Desemba 2004, watafiti kutoka kwenye vituo vya utafiti vya Wizara ya Kilimo na Chakula walianzisha vishamba vya pamba vya majaribio kwenye wilaya za Chunya, Nachingwea, Masasi na Newala ili kubaini ukweli wa kuwepo au kutokuwepo kwa funza mwekundu katika maeneo yaliyo chini ya karantini ya funza mwekundu.

Ukaguzi wa awali wa vishamba vya majaribio uliofanywa katika miezi ya Machi na Aprili, 2005 ulibaini kwamba funza mwekundu alionekana katika vijiji vya Mbala, Galula, Magamba, Chang'ombe, Kanga na Ifumbo vilivyopo katika wilaya ya Chunya, Rweje na Mpiruka vilivyopo katika wilaya ya Nachingwea na Mkwera kilichopo katika wilaya ya Masasi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo hayo ya awali na ukweli kwamba taarifa rasmi ya matokeo ya utafiti huo itatolewa baada ya kukamilika kwa utafiti huo katika mwaka wa 2006/2007, Serikali haikubali kwamba huu ni wakati mwafaka wa kuruhusu kilimo cha pamba katika mikoa ya kusini mwa nchi.

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, na swali moja dogo la nyongeza, kwa kuwa Serikali haijapata ithibati kamili ya kuwepo au kutokuwepo kwa mdudu huyo na hivyo wananchi wa mikoa ya kusini wataendelea kukosa huduma hiyo. Je, Serikali inampango gani ya kuwatafutia watu wa kusini zao mbadala ili waweze kuondokana na umaskini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kuona *concern* zako kuhusu wakulima Mheshimiwa Salim, ukweli ni kwamba mazao mbadala yapo, ikijumisha korosho, ufuta, karanga hata alizeti yapo. Kwa hiyo Mheshimiwa tunaomba tuendelee kufanya utafiti kabla hatujaeneza janga hili likafika kaskazini ambapo *king cotton* ni zao maarufu la utajirisho.

Na. 361

**Mikopo na Biashara za Nchi za Nje**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa mikopo na biashara za nchi za nje ni mambo ya Muungano:-

(a) Je, ni kiasi gani cha mikopo kimekopwa katika kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 1992 – 2002?

(b) Je, utaratibu wa kulipa madeni hayo ukoje?

(c) Je, ni biashara gani ya nje inayofanywa na kwa pamoja (Kimuungano) kama ilivyoainishwa ndani ya Katiba na Sheria ya kuanzisha *External Trade*?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed Mbunge wa kuteuliwa lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kuanzia mwaka wa fedha 1991/92 hadi 2001/2002, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa imesaini na nchi wahisani, Mashiriki ya Fedha ya Kimataifa pamoja na benki mbali mbali za kibiashara, mikataba ya mikop yenye jumla ya dola 3.2 bilioni za kimarekani ambapo mikopo iliyopokelewa ni dola za Marekani bilioni 2.6 sawa na asilimia 79.5.

(b) Serikali ya Jamhuri ya Muungano imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwenye bajeti yake kulipia madeni ya nje kwa kadri yanavyopevuka. Kwa mikopo ambayo inanufaisha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar pekee au Mashirika yake kumekuwa na mikataba ya ndani inayotaka madeni hayo yarejeshwe kupitia Serikali ya Muungano na Benki Kuu ya Tanzania.

(c) Mheshimiwa Spika, hakuna biashara ya nje inayofanywa kwa pamoja kimuungano. Masuala ya biashara ya nje ambayo yanaratibiwa kwa pamoja yameainishwa katika kifungu cha Sheria Na. 5 ya mwaka 1978 iliyoanzisha Halmasharui ya Biashara ya Nje (*BET*) ambapo shughuli zote za uendelezaji wa biahsara za nje *(trade development and promotion*) zinafanywa kimuungano bila kutofautisha. Mfano mmoja wapo ni ushiriki kwenye maonyesho ya nchi za nje au ngazi ya taifa ambapo wafanyabiashara wa Bara na wa Zanzibar hukaribishwa kushiriki.Kwa upande wa kupata takwimu na taarifa za kibiashara Halmashauri ya biashara za nje inashirikiana kwa karibu na kituo cha Biashara Zanzibar, yaani *Zanzibar Trade Centre*.

**MHE. HAMAD RASHIDI MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, asante kwa maswali mawili ya nyongeza, kwa kuwa kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria tuliyopitisha hapa Bungeni ya kumpa Waziri wa Fedha madaraka ya kukopa na kwa kuwa ni deni la Muungano. Je, Waziri atatuthibitishia katika Bunge kwamba deni linalodaiwa Serikali ya Zanzibar, nalo ni sehemu ya deni la Muungano, na kwa hiyo linatakiwa kulipwa katika *Consolidated* fulani ya muungano?

La pili kwa kuwa *external trade* ni suala la muungano, na kwa kuwa mazoa yote makuu ya nchi hii kwa upande wa Tanzania Bara, yameruhusiwa watu binafsi kusafirisha. Je, hawaoni kwazuia wananchi wa Zanzibar wanaozalisha hasa zao la

karafu, karafu zao bado kudhibitiwa katika mfumo wa ukiritimba ni kuvunja sheria na katiba ya nchi ambayo *external trade* ni suala la muungano?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi katika kipengele cha (b) nilijibu kwamba mikopo ambayo inainufaisha Serikali ya Mapinduzi Zanzibara peke yake au mashirika yake, kumekuwa na mikataba ya ndani, ambayo inataka mashirika madeni hayo yarejeshwe kupitia Serikali ya muungano na benki kuu ya Tanzania. Kwa hiyo nafikiri hili halina utata na taratibu zote zinafuatwa kulingana na mikataba yenyewe, na madeni ya Tanzania yanajumuisha pia Zanzibar, kwa hiyo hilo nafikiri halina utata na endapo kuna matatizo kuhusiana na hili Kamati ya pamoja ya fedha ya Mheshimiwa Shellukindo, *joint finance committee* itaangalia na kuchambua mambo ambayo bado yanahitaji kufanyiwa kazi. Ukiritimba kwenye karafu, ili tatizo limeshughulikiwa na limefanyiwa kazi katika hatua mbalimbali ndani na Serikali ya Zanzibar na naomba hili lifanyiwe kazi na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuongezea jibu la Naibu Waziri kama ifuatavyo:  Madeni ya nje, madeni yetu kwa nchi za nje, yanalipwa na Serikali ya muungano, yanalipwa na Serikali ya muungano. Misamaha ikitoka inakuja kwa Serikali ya muungano, lakini kuna madeni ambayo yanakopwa kwa matumizi ya Zanzibar pekee, kwa mfano hivi tunavyozungumza kidogo kuna madeni ambayo ya fedha zitakazotoka Badea kwa ajili ya barabara za Pemba au kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Zanzibar. Madeni yale anayekwenda kusaini ni mimi hapa lakini maalumu kwa ajili ya Zanzibar, siku ya kulipa Zanzibar inalipa kupitia benki kuu, na sisi muungano tunaratibu tunajua kwamba tarehe hii imefika nido ya kulipa, yanaenda benki kuu tunarudisha kule. Hiyo tunasema kwamba madeni ambayo ni ya miradi ya Zanzibar peke maalum yanalipwa na kile chombo cha Zanzibar kinachohusika kupitia benki kuu. Nafirikiri hilo halina utata kabisa na hili la pili la biashara, katika biashara katia katiba ya muungano biashara ya muungano ni takwimu, biashara ya muungano ni takwimu kama tulivyosema kwenye jibu letu, na ndio maana Serikali ya Mapinduzi Zanzibara ina Wizara ya Biashara na Serikali ya Muungano ina Wizara ya Biashara. Kwa sababu mambo ya biashara karafu na biashara nyingine yanashughulikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pekee, nafikiri hilo pia linaeleweka.

Na. 362

**Fedha Zilizotengwa kwa Ajili ya Matengenezo ya Barabara**.

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa kiwango cha fedha kinachotolewa kutengeneza barabara katika mkoa wa Shinyanga ni cha chini ukilinganisha na idadi ya barabara zinazotengenezwa na Serikali Kuu.

(a) Je, ni kwanini Serikali inatoa fedha chache kiasi hicho?

(b) Je, mpaka sasa pamekuwepo na mita ngapi za barabara zinazotengenezwa na Serikali kwa kila Km. 2 ya eneo la Mkoa wa Shinyanga?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Makolo, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mapato ya Serikali kwa ajili ya matengenezo yanategemea kwa kiasi kikubwa fedha za makusanyo ya mfuko wa barabara *(Road Fund)*. Fedha hizi bado hazikidhi mahitaji ya mtandao wa barabara nchini ambapo unajumuisha barabara kuu, barabara za Mikoa na barabara za Halmashauri za Wilaya. Kwa hali hiyo Serikali inalazimika kutafuta vyanzo vingine vya fedha ikiwa ni pamoja na misaada toka kwa wahisani na mikopo toka taasisi mbalimbali za fedha duniani.

Hata hivyo pamoja na ufinyu wa fedha za Mfuko wa barabara natumaini Mheshimiwa Mbunge atakubalina na juhudi za dhati ambazo zinafanywa na Serikali kupitia Wizara yangu katika kuboresha mtandao wa barabara katika Mkoa wa Shinyanga. Kwa mfano:-

Katika mwaka wa fedha wa 2001/2002 jumla ya shilingi milioni 587.5 zilitumika kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara za Mkoa na Shilingi milioni 319.2 zilitumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu.

Katika mwaka wa fedha 2002/2003 Serikali ilisaini mkataba wa ujenzi wa barabara kuu kwa kiwango cha lami zenye jumla ya kilometa 169 kutoka mpakani mwa Mkoa wa Mwanza na Shinyanga hadi Tinde za kutoka Isaka hadi Nzega kupitia Tinde.

Ujenzi huo ulioanza kufanyika katikati ya mwaka 2004, unatekelezwa na mkandarasi Grinaker LTA wa Afrika ya Kusini. Ujenzi huo utagharimu kiasi cha shilingi bilioni 60 ikiwa ni msaada kutoka Jumuiya ya Ulaya *(EU)*. Kilometa 146 za barabara hizo zimo ndani ya Mkoa wa Shinyanga peke yake. Aidha katika mwaka huo jumla ya shilingi milioni 781.8 zilitumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Mkoa na shilingi milioni 916.9 kwa matengenezo ya barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2003/ 2004 jumla ya shilingi milioni 640 zilitumika kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara za Mikoa na shilingi milioni 598 zilitumika kufanyia matengenezo ya Barabara kuu.

Aidha katika mwaka wa fedha 2004/2005 jumla ya shilingi milioni 1,074 zimetumika kwa ajili ya matengenezo ya barababara za Mkoa na shilinggi milioni 788 zimetumika kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara kuu.

Mheshimiwa Spika, natumaini kuwa Mheshimiwa Mbunge atakubalina nami kuwa viwango hivyo vya bajeti vilivyotolewa na kutumika kwa matengenezo ya barabara mkoani shinyanga ni vikubwa ukilinganisha na uwezo wa Serikali yetu kiuchumi.

(b) Mheshimiwa Spika Mkoa wa Shinyanga unao eneo lenye jumla ya Kilometa za mraba 50,810. Mtandao wa barabara mkoani unaohudumiwa na Serikali kupitia ofisi ya Wakala wa Barabara Mkoa *(TANROADS)* una jumla ya urefu wa kilomita 1,336 kwa uwiamo huo, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi inalo jukumu la kuhudumia wastani wa kilomita 1 ya barabara kwa kilomita 38 za mraba Mkoani Shinyanga ambayo ni sawa na mita 52.6 kwa kilomita 2 za mraba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Paul N. Makolo ameridhika nashukuru kwa sababu muda wa maswali umekwisha, kwa hiyo tunaendelea na mambo mengine. Matangazo ya vikao, vikao vya leo ni kama ifuatavyo Kamati ya Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti Haroub Masudi, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kwamba kutakuwa na kikao leo saa 5 asubuhi kwenye ukumbi Na. 428. Kamati nyingine ni Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *LAAC*, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mgana Msindai, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kikao kitafanyika saa 5 asubuhi chumba Na. 219. Vilevile kutakuwa na kikao cha Kamati ya uongozi na kikao cha Tume ya Huduma za Bunge saa 4.30 katika chumba cha mikutano cha Spika. Vilevile Mheshimiwa Paul Kimiti, Mwenyekiti wa Chama cha Idadi ya Watu na Maendeleo anawakumbusha Wajumbe wake kwamba kutakuwa na kikao leo saa 7 mchana, tukishaahirisha shughuli za hapa saa 7 mchana Wajumbe wa kikao hicho wabaki humu humu ndani ya ukumbi, hivyo ni vikao.

Sasa mambo mengine yanayofaa kujulikana ni kwamba Serikali kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali amechapisha upya vitendea kazi, yaani Katiba ya Jamhuri ya Muungano pamoja na Sheria ya Uchaguzi matoleo ya mwaka huu. *(Makofi)*

Kwa hiyo hivi ndio vitendea kazi ambavyo tunahitaji kuwa navyo Waheshimiwa Wabunge tunapokwenda kwenye shughuli za uchaguzi, ndio maana tumeamua tuvigawe humu ndani kwa sababu tukiweka kwenye *pigeon hole* wengine pengine watatoka bila kuziona. Kwa hiyo ni Katiba ya Jamhuri toleo la 2005, Sheria ya Uchaguzi toleo la 2005. *(Makofi)*

Sasa pengine ni vyombo vya habari vinaelekea kukosea kosea, napenda kutoa ufafanuzi kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano atalihutubia Bunge kesho, lakini hatavunja Bunge kesho. Bunge atalivunja kwa amri ya Rais itakayotoka kwenye gazeti la Serikali tarehe 5 mwezi wa 8, kwa hiyo Wabunge wanapoondoka hapa kesho na kesho kutwa watakuwa bado ni Wabunge mpaka watakapofika kwenye maeneo yao, Ubunge wao unakwisha tarehe 5 mwezi wa 8 siyo kesho. *(Makofi)*

Sasa matokeo ya kuvunjwa kwa Bunge nayo ni vizuri yakajulikana ni kwamba kila kitu ambacho kilikuwa kimeandaliwa kufanyiwa kazi katika Bunge hili kinakoma, kama kinakoma na Bunge lijalo liweze kuanza upya. Maana yake ni kwamba kama kuna maswali ya Waheshimiwa Wabunge yalishawasilishwa kwa Katibu wa Bunge ambayo

hayakupata kujibiwa katika mkutano huu sasa yanafutika itabidi tuanze upya. Itabidi wanaokuja waanze upya kuandikisha maswali upya. Pia shughuli nyingine ambayo haikukamailika kwa mfano jana tumesoma Miswada mara ya kwanza, ndio mwisho wake. Bunge litakalokuja itabidi lianze upya kusoma hiyo Miswada mara ya kwanza tena.

Vilevile chaguzi zilizofanywa na Bunge hili, chaguzi zitakazofanywa na Bunge hili nazo zinafikia mwisho. Ndio maana Bunge lijalo litafanya uchaguzi wa uongozi wa Bunge, Spika, Naibu Spika na wenyeviti ndio maana Bunge lijalo litafanya uchaguzi mpya wa wale tuliowachagua hapa kwenda kwenye vyombo vingine kwa mfano Mabaraza ya Vyuo Vikuu huwa tunachagua hapa wawakilishi wanaokwenda kutuwakilisha. Uwakilishi wao unakoma tarehe 5 Agosti, 2005. Waliochaguliwa kwenda kwenye Bunge la Afrika Ubunge wao wa Afrika unakoma tarehe 5 mwezi ujao 2005, kila kitu kinakoma. Kamati za Bunge zinakoma ili kusudi Bunge linalokuja linaanza upya kabisa ni vizuri ikajulikana hivyo. Ahsante sana.*(Makofi)*

## KAULI ZA MAWAZIRI

### MAREKEBISHO YA VIWANGO VYA USHURU WA FORODHA KWA BAADHI YA BIDHAA

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa kauli ya Serikali naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Benki ya Maendeleo ya Afrika yaani *African Development Bank* yenye Makao yake Makuu ya muda huko Tunis Tunisia imepata Rais mpya. Tarehe 21 Julai Mheshimiwa Donald Kaberuka Waziri wa Fedha wa Rwanda alichaguliwa na Magavana wa Benki hiyo kushika wadhifa wa Urais wa Benki hiyo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Kwa niaba ya Serikali nami binafsi natoa pongezi nyingi na za dhati kwa Mheshimiwa Donald Kaberuka ambaye amewahi kuishi Tanzania kwa muda mrefu kabla ya kurejea Rwanda kujiunga na Serikali ya huko. Naamini kwamba uteuzi huo utainufaisha sana Tanzania kutokana na uwezo wake mkubwa na ukweli kuwa Benki hiyo ni mfadhili muhimu sana wa miradi yetu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kauli kuhusu hatua za kodi kutokana na itifaki hii ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, marekebisho ya viwango cha Ushuru wa Forodha kwa baadhi ya bidhaa katika mwaka 2005/2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu litakavyokumbuka wakati nikiwasilisha hotuba ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2005/2006, nilisema kwamba nitawasilisha taarifa kuhusu hatua mbalimbali za marekebisho ya kodi husasan ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazotoka nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki baada ya kuidhinishwa na kikao cha Mawaziri husika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, baada ya nchi zetu kuridhia itifaki ya Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mamlaka ya kubadilisha viwango, kutoa misamaha au unafuu wa Ushuru wa Forodha kwa bidhaa mbalimbali zinazoagizwa kutoka ya nje ya nchi wanachama wa Jumuiya hii yamekabidhiwa kwa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya na huchapishwa katika gazeti la Baraza yaani *council* gazeti. Maamuzi ya Baraza hilo la

Mawaziri hayajadiliwi tena na chombo kingine cha Afrika Mashariki kwa lengo la kufanya mabadiliko yoyote. Kwa hiyo basi marekebisho ya ushuru niliyogusia kwenye hotuba yangu ya Bajeti yanahusu maeneo yafuatayo:-

(a) Msamaha wa Ushuru wa Forodha ambao utatolewa kwa bidhaa zifuatazo:-

1. Vifaa vya matumizi ya nyumbani kwa wakazi wa nchi za Jumuiya za Afrika ya Mashariki wakati wanaporudi nyumbani kutoka nje pindi watimizapo sharti la kukaa nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 12.

2. Mizigo mingineyo ya abiria wanaorudi nchini ambayo thamani yake haizidi dola za Kimarekani 300.

3. Pembejeo zinazotumika katika sekta ya kilimo cha mboga, maua na kilimo kwa ujumla yaani *inputs for horticulture na agricultural sector.*

4. Vifungashio vya madawa ya binadamu yaani *packaging for pharmaceutical products.*

(b) Eneo lingine ni la kutotoza Ushuru wa Forodha yaani kuweka kiwango cha *0 percent* kwa bidhaa zifuatazo:-

1. Vifaa vinavyotumia mionzi ya jua na spea zake yaani *solar equipment and accessories*.

2.Malighafi ya kutengeneza zana za kilimo yaani *inputs for the manufacture of agricultural equipment.*

3.Tatu vifaa vinavyotumika mahotelini, hili ni muhimu yaani mashine za kufua nguo, vifaa vinavyotumika jikoni yaani *kitchen wear*, majokofu *kitchen wear* katika mahoteli, majokofu yaani *fridges and freezers* katika mahoteli, viyoyozi katika mahoteli, *air condition systems*, luninga yaani *television* katika mahoteli, mazulia katika mahoteli, samani, shuka na mapazia katika mahoteli na pia vifaa mbalimbali vinavyotumiwa na wawekezaji katika sekta ya utalii na mahoteli.

4.Malori yaliyowekezewa vipoza joto yaani *refrigerated tracks*.

5.Njiti ghafi yaani *sprints* kwa ajili ya kutengenezea viberiti.

6.Madawa mbalimbali ya binadamu yanayoagizwa kutoka nje kama yalivyoainishwa. 7.Mikanda inayotumika kwenye magari yaani *safety belts* kwa ajili ya usalama wa abiria.

8.Mafuta ghafi ya mawese kwa ajili ya kutengeneza sabuni yaani *palm*s *stearing fraction under HS called* 1511.90.20.

9.Taulo za usafi kwa ajili ya kina mama yaani *sanitary* taulo na *temples under HS called* 4818.40 na *HS called* 5601.10.00. 10.Malighafi kwa ajili ya kuzalisha taulo za usafi yaani taulo hizo hizo yaani *row materials for making diapers and sanitary pads.*

11.Gesi kwa ajili ya matumizi ya nyumbani yaani *liquefied petrol gas LPG.*

12.Vifaa vya utaalam wa *computer* yaani *computer soft wear*, kuna moja aina zote za makaa ya mawe yaani *coal under HS called* 27.01 na

13.W*ear* za *alluminium* zenye kipenyo ki(c)Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni kutoza ushuru wa forodha kwa asilimia 10 kwa bidhaa zifuatazo:-

(a.) Nguo zinazotengenezwa kwa kuwekwa tabaka la *plastic* yaani *cloth coated with plastic materials HS called* 5900.

Pili, mashine za kutengeneza chai, kahawa na zile za kukausha mikate yaani *coffee and tea makers and tosters***.**(b)Mitumba yaani *worn of second hand cloth* hili nalo naomba lieleweke mitumba.

(d) Ni kupunguza kiwango cha ushuru wa forodha kwa nguo za mitumba kutoka asilimia 50 yaani 50 *percent,* au dola za Kimarekani 0.75 kwa kilo hadi asilimia 45 au dola za Kimarekani 0.30 kwa kilo.

(e) Eneo la tano linahusu shule za Kimataifa, vyuo vikuu binafsi na hospitali binafsi.

Kwa kuwa wanajitokeza wawekezaji binafsi kujenga vyuo vikuu, shule za kiwango cha Kimataifa na hospitali ili kutoa huduma za kijamii zinazofanana sana na zile za madhehebu au taasisi zisizo za Kiserikali yaani *NGOs,* imeamuriwa kwamba wawekezaji hao binafsi yaani *private investors* waingizwe katika utaratibu wa kulipiwa Ushuru wa Kodi ya *VAT* kwa njia ya *voucher* za Hazina yaani *treasury voucher system* ambayo tunaitumia sasa hivi, kwenye vifaa vya kujengea miradi hiyo. Wahusika watatakiwa kutimiza masharti ambayo ni pamoja na mapendekezo ya Mkuu wa Wilaya husika, Katibu Mkuu mwenye dhamana ya elimu ya juu wa shule na vyuo hivyo vya Kimataifa na wa afya kwa hospitali kama ilivyo kwa miradi ya *NGOs*. Misamaha ya Ushuru wa *VAT* itahusu vifaa vya ujenzi pekee, uamuzi huo una lengo la kuvutia wawekezaji wa ndani na nje kwenye sekta za elimu ya juu na hospitali za kisasa

(f) Eneo la sita ni karatasi za kuchapisha makala za kitaalum paper for printing educational materials. Imekubalika kuingiza karatasi za kuchapisha makala za kitaaluma yaani za mitahani, vitabu vya shule na majalada katika mfumo wa duty remission ili kupunguza gharama za karatasi hizo. Tayari karatasi kwa ajili ya kuchapisha madaftari zilishaingizwa katika utaratibu huo hivyo pendekezo hili lina lengo la kupanua wigo wa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwa sekta ya elimu. *(Makofi)*

(g) Eneo la saba ni zawadi za wanariadha yaani *athletics prices*, ushuru unaotozwa kwenye zawadi zinazoletwa na wanamichezo wa nchi za Jumuiya ya Afrika

ya Mashariki sasa utalipwa na Serikali kwa utaratibu wa *voucher* za Hazina, yaani Serikali itawalipia ushuru huo badala ya wao kulipa. *(Makofi)*

(h) Kuhusu magari, ushuru unaotozwa hivi sasa wa asilimia 25 kwa magari ya abiria na mizigo unaathiri kwa kiwango kikubwa sekta ya usafirishaji hasa ikizingatiwa kuwa gharama za mafuta nazo zimepanda sana.

Aidha, baada ya wawekezaji wameanza kujitokeza kuwekeza katika sekta ya magari ili kulinda maslahi ya watumiaji na utengenezaji wa magari katika eneo la Afrika ya Mashariki, imeamuliwa kwamba nchi wanachama kwa pamoja wakutane na wazalishaji wa magari yaani *motor assemblies* ili kuangalia uwezekano wa kuwasaidia na kutatua tatizo la ubora wa bidhaa zao, bei na jinsi watakavyoweza kuzalisha kwa kutosheleza mahitaji ya soko la Afrika ya Mashariki.

(i) Maamuzi mengine ni kwamba Baraza la Mawaziri wa Jumuiya lilijadili kwa kina haja ya kuwepo mipango na mikakati maalumu ya kutumia upenyo wa uwezo tulionao katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji ili kuyaendeleza kwa pamoja kwa kuwapatia msukumo wawekezaji kwenye maeneo hayo.

Kenya wametakiwa kusimamia eneo la utengenezaji wa magari yaani *motor vehicle assembly* ambapo Uganda watasimamia suala la uhamasishaji katika mkakati wa kutengeneza gundi yaani *glue,* wanga yaani *starch* na pikipiki. Aidha, Tanzania imepewa jukumu la kuhamasisha usindikaji wa matunda hasa kwa ajili ya maji ya soda na ya matunda yaani *juices and contrates* na pia uzalishaji wa nguo za pamba yaani *cotton textiles*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, hatua hizi zote zinategemewa zitatekelezwa kote Afrika ya Mashariki kuanzia tarehe 1/7/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia kiti*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2005 *(The Appropriation Bill, 2005).*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa kutumia shilingi 3,647,906,296,400/= kutoka mfuko mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo itakayotekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2005/2006 na kutumia fedha zitakazotolewa na Serikali kwa ajili hiyo sasa usomwe mara

ya pili. Itakumbukwa kwamba katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka 2005/2006 nilieleza shabaha na malengo ya Serikali ya kutumia shilingi 3,647,906,296,400 kwa mwaka 2005/2006 kama ifuatavyo:-

1. Matumizi ya kawaida shilingi 2,262,723,184,000.
2. Matumizi ya miradi ya maendeleo shilingi 1,385,183,112,400.
3. Jumla ni shilingi 3,647,906,296,400.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako Tukufu limekwisha jadili na kupitisha hoja mbalimbali za Waheshimiwa Mawaziri wakati walipowasilisha makadirio ya Wizara zao. Madhumuni ya Muswada huu ni kuliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe matumizi ya Serikali ya mwaka 2005/2006 ya jumla ya shilingi 3,647,906,296,400 kutoka mfuko mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo iliyokubaliwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2005 *(The Appropriation Bill, 2005)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la *Muswada*

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2005 *(The Appropriation Bill, 2005)***

*(Kusomwa mara ya Tatu)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa kutumia fedha Sh.3,647,906,296,400/= kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo itakayotekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2005/2006 sasa umekubaliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006 yalipitishwa na Bunge)*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2005**
***(The Finance Bill, 2005)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2005, yaani *The Finance Bill* 2005 pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Njelu Kasaka – Mbunge wa Lupa kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako kwamba tutazingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati na tutayafanyia kazi ipasavyo. Aidha, kwa mara nyingine napenda kutoa tena shukurani kwa Waheshimiwa Wabunge wengine wote ambao walichangia katika hotuba ya Bajeti. Tumezingatia kwa dhati michango yenu ambayo imesaidia sana kuboresha Muswada huu.

Vile vile nawashukuru pia wadau mbalimbali katika sekta ya fedha, biashara, sekta binafsi, wakulima na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti wametoa ushauri wao ambao kwa kiwango kikubwa tumezingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudia kuzifanyia marekebisho, Sheria 14 zinazohusu fedha, kodi na ushuru, kwa lengo la kuweka, kurekebisha au kufuta viwango vya kodi, ushuru na ada mbalimbali.
Sheria hizo ni:

(i) Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 200;
(ii) Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 332;
(iii) Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004;
(iv) Sheria ya Ushuru wa *Stamp* ya mwaka 1972;
(v) Sheria ya Bodi ya Rufaa za Kodi ya mwaka 2000;
(vi) Sheria ya Leseni za Usafirishaji ya mwaka 1973;
(vii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya 1997;
(viii) Sheria ya Kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Afrika ya Mashariki *(EADB)* ya mwaka 1984;
(ix) Sheria ya Kodi ya Ukadiriaji Majengo Mijini ya mwaka 1983;
(x) Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta ya mwaka 1985;
(xi) Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2001;
(xii) Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo Sura ya 108;
(xiii) Sheria ya Bima ya mwaka 1996; na
(xiv) Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ulio mbele yenu, umegawanyika katika sehemu kuu 15. Sehemu ya kwanza, inahusu masuala ya Utangulizi kama vile jina na tarehe ya kuanza kutumika kwa Muswada wenyewe. Sehemu ya pili, inapendekeza kuifanyia Marekebisho Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001. Katika marekebisho haya, inapendekezwa kufuta kifungu cha 12, vifungu vidogo vya tatu na tano ili kuondoa msamaha wa Kodi ya Mapato, Kodi ya Ongezeko la Thamani na Ushuru wa Forodha, kwa wanachangia Mfuko huo ili wachangiaji hao wawe wamepata punguzo hilo la kodi kwa mkondo mmoja tu wa kifungu cha 16 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa katika Kifungu cha tatu, jedwali la kwanza sura ya 332. Katika marekebisho hayo inapendekezwa:-

(a) Kurekebisha kifungu cha tatu cha Sheria hiyo kwa kuongeza kifungu kidogo cha pili ili kutoa nguvu ya kisheria ya kubadilisha viwango vya ushuru wa bidhaa kulingana na mfumuko wa bei, yaani *inflation* kwa kila mwaka husika.

(b) Kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwa asilimia tano tu, sawa na mfumuko wa bei kwa bidhaa za vinywaji baridi, bia mvinyo na vinywaji vikali.

(c) Kurekebisha mfumo wa kutoza ushuru wa bidhaa kwenye sigara ili kutumia kigezo cha kuwa na kichungi yaani *(filter)* badala ya urefu wa sigara.

(d) Kufanya marekebisho yenye lengo la kuainisha *Tariff Codes* za bidhaa za mafuta ya petroli zilizomo kwenye Sheria ili zilingane na *Tariff Codes* zinazoainishwa ndani ya utaratibu wa bidhaa toka nje ya Afrika ya Mashariki, yaani *Common External Tariff* chini ya itifaki ya kuunda Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ya Mwaka 2004 bila kuathiri viwango cha kodi.

Aidha, marekebisho mengine ni kutoa msamaha wa ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya ndege *(JET A 1)* ili kuweka usawa katika ushindani kwa faida ya wenye ndege wa hapa nchini.

Sehemu ya Nne inapendekeza kurekebisha sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kifungu cha 16 (1) kuongeza kifungu kidogo (e) ili kusamehe kodi ya mapato, michango inayochangwa na Taasisi za Serikali kwa lengo la kugharamia Miradi ya Maendeleo ya Wananchi ili isitozwe kodi ya mapato. Kwa hivi sasa michango hii haitambuliwi na sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 kama ni gharama za biashara na hivyo, hutozwa kodi ya mapato. Nia ni kutoa unafuu wa kodi kwa michango ambayo inasaidia maendeleo ya Wananchi kama ile iliyokuwa inazungumzwa hapa leo ya Mbuga za Wanyama.

(b) Kurejesha vifungu vya 83 na 90 kama vilivyo hivi sasa badala ya mapendekezo ya awali ya kuvibadili kama ilivyopendekezwa katika Muswada huu kifungu cha 10. Hatua hii itapunguza usumbufu katika ukusanyaji wa kodi.

(c) Katika Jedwali la kwanza kuongeza kiwango cha chini cha mapato ya ajira yasiyotozwa kodi kutoka shilingi 60,000/= kwa mwezi hadi shilingi 80,000/= kwa mwezi, kwa lengo la kuwaondoa kwenye wigo wa kodi, wafanyakazi wa kipato cha chini na hivyo kutoa unafuu wa kodi kwa wafanyakazi hao. Viwango vya ukokotoaji wa kodi hiyo kwa ngazi mbalimbali za mishahara vimebaki kama vilivyokuwa, yaani asilimia 18.5, 20, 25 na 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Ushuru wa *stamp* ya mwaka 1972 katika Jedwali kama ifuatavyo:-

(i) Kupunguza kiwango cha ushuru wa *stamp* kwenye utambuzi wa madeni, yaani *Acknowledgement of Date* kutoka shilingi 40 kwa kila shilingi 1,000 sawa na asilimia nne hadi shilingi 500 tu;

(ii) Kupunguza Ushuru wa *Stamp* kutoka asilimia nne hadi moja ya mali husika kwenye kubadilishana mali, hati za mauzo na zawadi, uhamishaji wa mali ya kukodi na kadhalika; na

(iii) Inapendekezwa kupunguza Ushuru wa *Stamp* kutoka asilimia mbili hadi moja kwa ajili ya haki ya ugawanyaji, utoaji na usuluhishi.

Marekebisho haya yana lengo la kurahisisha utawala wa kodi, pamoja na kupunguza gharama za usimamizi wa biashara.

Sehemu ya sita, inahusu marekebisho katika Sheria ya Bodi za Rufaa ya Kodi ya mwaka 2000. Kifungu cha 12 cha Sheria hiyo, kinarekebishwa ili kulinda haki ya mlipa kodi kwa kumuwezesha kuwasilisha pingamizi la kodi aliyokadiriwa na Mamlaka ya Mapato, baada ya muda wa Sheria kupita endapo kutakuwa na sababu za msingi za kuchelewa kuwasilisha pingamizi husika kutokana na ugonjwa, kutokuwepo nchini wakati wa makadirio ama sababu nyingine zozote ambazo Kamishna wa Kodi ya Mapato, ataridhika kuwa ni za msingi.

Sehemu ya saba, inahusu marekebisho katika Sheria ya Ada ya Leseni za usafirishaji ya mwaka 1973. Marekebisho yanayopendekezwa ni ya kiujumla na yanahusu vifungu vya 11, 12, 13, 14, 22 na 23, ambayo msingi wake ni kufuta ada ya leseni ya magari madogo madogo ya mizigo, yaani *Pick-ups* na magari makubwa ya mizigo, yaani *Lorries* na kadhalika kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nane, inapendekeza kufanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* ya mwaka 1997 katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kifungu cha 19 kwa kufuta vifungu vidogo vya 5, 6, 7 na 8, ili kuhamishia utaratibu wa kuahirishakulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* kwa bidhaa za mtaji, kwenye jedwali la tatu la sheria. Mapendekezo haya yanakusudia kufafanua zaidi utaratibu huu na vilevile kuendana na Sera ya Serikali, inayokataza kutoza kodi hii kwa bidhaa za mtaji *(Capital Goods).*

(b) Jedwali la kwanza, kungiza msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa wazalishaji wa humu nchini wa vifaa vya usafi wa akina mama *(Sanitary Pads),* pamoja na dawa za mbu za kuchoma *(Mosquito Coils)* katika kipengele cha 11(c).

(c) Jedwali la pili, kwanza, kuingiza msamaha wa *VAT* kwa vifaa vya usafi wa akina mama, pamoja na dawa za mbu za kuchoma. Pale vinapouzwa na wafanyabiara ambao si wazalishaji na kwa wale wanaoviagiza kutoka nje ya nchi. Pili, kuingiza msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mafuta ya ndege, kwa wenye ndege za kibiashara au huduma za jamii za hapa nchini. Hatua hii inalenga kuwawezesha wenye ndege hizo hapa nchini, kuhimili ongezeko kubwa la gharama za kuendesha ndege hasa baada ya tukio la kigaidi la Septemba 11 na ongezeko la sasa la bei ya mafuta ya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba, hili suala la *sanitary pads,* linashughulikiwa katika ngazi mbili ya Afrika ya Mashariki na ndani ya nchi yetu kwa taratibu na sheria zetu.

(d) Jedwali la tatu, kwanza, kuahirisha utekelezaji wa kipengele cha saba cha Jedwali hili ili kujipa muda zaidi wa kuweka utaratibu muafaka wa kushughulikia misamaha hii baina ya Mamlaka ya Mapato na wenye migodi.

Pili, kufuta kipengele cha 13 ambacho kinatoa msamaha kwa taasisi za umma, ambazo zinapata ruzuku kutoka Serikalini kwa kuwa Sera ya Serikali na Taasisi zake kwa sasa ni kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani.

Katika Jedwali la 3 (e) kutoa msamaha wa *VAT* kwenye magari yanayotumika kutoa huduma za afya *(Mobile Health Clinics)* ili kuvutia huduma hizo katika maeneo yasiyo na vituo vya afya au zahanati. Aidha, inapendekezwa kuingiza msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye magari ya zimamoto, yanayoagizwa na Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa ili kuziwezesha kukabiliana na kukithiri kwa majanga ya moto, hivyo, kuokoa maisha ya watu na mali zao.

Marekebishao mengine yanayopendekezwa ni kuingiza msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani katika vipuri vya treni na vifaa vingine vinavyotumika katika treni ili kupunguza gharama za usafirishaji na kusaidia Shirika la Reli na Shirika la *TAZARA,* kumudu gharama za matengenezo

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tisa inahusu sheria ya kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Afrika ya Mashariki ya mwaka 1984, ambapo vifungu vya 44 na 45 vinafanyiwa marekebisho, kwa lengo la kutoa kinga kwa Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki, Tawi la hapa nchini, kutokana na amri za Kimahakama zenye kuathiri uhai wake wa kibiashara, zikiwemo za kukamata mali. Hatua hii ni utekelezaji wa Azimio Namba 6 la mwaka 2004, lililoridhiwa na Baraza la Mawaziri wa Fedha wa nchi Mwananchama wa Kenya, Uganda na Tanzania, kwa mujibu wa Ibara ya 52 ya Katiba ya Benki hiyo ya *EADB (EADB Charter).* Azimio hili lilifikiwa ili kuinusuru Benki hii kutokana na hasara zitokanazo na amri za Mahakama za kukamata mali za Benki hii, ambapo katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, Benki ilipata hasara ya takriban shilingi bilioni 19, kwa kutokuwa na kinga ya aina hii na kuiweka katika hali ya kunusurika kufilisika.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakusudiwa kukifanyia marekebisho kifungu cha saba cha Sheria ya Ukadiriaji wa Kodi ya Majengo Mijini ili kuongeza katika orodha ya misamaha ya kodi kwa majengo yanayomilikiwa na Madhehebu na Taasisi za Kidini kwa shughuli ambazo ni za huruma *(Charitable and not for Profit),* kwa ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia maamuzi ya Mawaziri wa Fedha wa Kenya na Tanzania, katika kikao cha mashauriano kilichofanyika mnamo Februari, 2005, katika kuimarisha mfumo wa kodi wa nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, inapendekezwa katika sehemu ya 11 kufanyia marekebisho Sheria ya Uhuru wa Barabara

na Mafuta *(Road and Fuel Tools Act of 1985),* ili kutoa msamaha wa ushuru wa barabara kwa magari yenye namba za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, yanapovuka mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 12 inakusudia kufanyia marekebisho, Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2001, ili kuhuisha katika jedwali la sheria hii, Mfuko wa *Advances Fund,* ambao hutumika kukopeshea Waheshimiwa Wabunge, vifaa vya usafiri, pamoja na *Government Store Fund.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko hii kwa pamoja ilianzishwa chini ya Sheria ya iliyokuwa *Exchequer and Audit Ordinance* ya mwaka 1961, ambayo ilifutwa mwaka 2001, baada ya kupitishwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2001. Kwa bahati mbaya, Mifuko hii ilisahaulika kuhuishwa katika Jedwali la sasa, chini ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2001 kama Mifuko mingine, pamoja na kwamba, iliendelea kufanya kazi. Madhumuni ya Marekebisho haya yanayokusudiwa ni kuipa Mifuko hii uhalali wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 13 inahusu marekebisho ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Kusajili Vizazi na Vifo, Sura ya 108 ili kuwawezesha wasajili wa Vizazi na Vifo wa Wilaya, kusajili uzazi wa mtoto au mtu aliyezidi miaka 10, pasipo kulazimika kupata kibali cha Kabidhi Wasii Mkuu. Hatua hii itawapunguzia usumbufu Wananchi ambao hulazimika kuchukua mufa mrefu kufuatilia vyeti vyao pindi wanapohitajika kwa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 14 inahusu marekebisho ya Sheria ya Bima ya mwaka 1996, ambapo inapendekezwa kukifanyia marekebisho kifungu cha 70 ili kuyataka Makampuni ya Bima yaliyosajiliwa nchini, kutoa kwa Kampuni ya Kitaifa ya mtawanyo ya Bima *(TANRAY),* mgawo wa biashara ya Bima *(Policy Session),* pamoja na mgawo utokanao na Mkataba wa Bima *(Treaty Session).*

Kifungu hiki cha 70 kama kilivyo hivi sasa, kinatoa chaguo kwa Kampuni hizi kutoa mgawo kwa sehemu tu za biashara zao, yaani Mkataba wa Bima *(Treaty)* au Hati ya Bima *(Policy).* Hali hii imesababisha Kampuni ya Kitaifa ya Bima *(TANRAY),* kukosa mapato tumilifu kutoka kwa mashirika husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya 15 na ya mwisho, inahusu marekebisho ya Sheria ya Mafao ya Watumishi wa Umma ya mwaka 1999, ambapo vifungu Namba 28 na 66, vinafanyiwa marekebisho ili kuwezesha mafao yatokanayo na michango ya wanachama kuweza kutumika kama dhamana au kulipia mkopo ambao mwanachama amekopa Benki, Taasisi yoyote ya fedha na pia kukopa kutoka katika Mfuko wenyewe. Aidha, marekebisho mengine yanahusu kutoa uwezo kwa Bodi ya Mfuko, kukopesha wanachama wa Mfuko tofauti na ilivyo sasa ambapo stahili hii hutolewa kwa wafanyakazi wa Mfuko pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, mengi ya mabadiliko ninayopendekeza ni utekelezaji wa Mapendekezo ya Serikali, ambayo yalikubaliwa na Bunge wakati wa Mjadala wa

Hotuba ya Bajeti. Hivyo, naomba Bunge lako Tukufu, lipitishe Muswada huu ili kuhalalisha kisheria, bajeti iliyokwishapitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, napenda kuchukua nafasi hii, nikushukuru wewe kwa niaba ya Wajumbe wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi, ili niweze kutoa maoni ya Kamati yetu baada ya kuchambua na kujadili Muswada wa Fedha wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 70 kifungu cha pili ya kanuni za Bunge, toleo la mwaka 2004, naomba sasa niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Fedha wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudia kufanya mabadiliko katika sheria mbalimbali za fedha na kodi mbalimbali kwa nia ya kuboresha na kubadilisha viwango mbalimbali vya kodi na ushuru. Kamati imepitia na kuchambua Muswada huu kwa kina na kupendekeza mabadiliko ambayo kimsingi Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameyakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi huu, Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijadili mfumo wa kutoza kodi, ushuru wa bidhaa ya sigara, kwa kujumuisha kichungi, yaani *filter* badala ya urefu wa sigara. Kamati imeishauri Wizara kuchukua hatua za kushirikisha viwanda vyote vinavyozalisha bidhaa hizi ili kutoa maoni yao juu ya bidhaa hii ili muafaka ufikiwe kwa kupata vigezo vya kutoza kodi kwa kulingana aidha na ujazo wa tumbaku au na kujumuisha kichungi. Aidha, Kamati imebaini kuwa, hali hii itaondoa wingu la mashaka la kuchochea ukiritimba kwa kiwanda kimoja na kuua ushindani nchini na hatimaye kuipunguzia mapato Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa jitihada zake za kukusanya mapato, kwa kuvuka malengo yaliyowekwa hususan baada ya kupitisha Sheria ya Mapato ya mwaka 2004. Aidha, pamoja na mafanikio hayo, Kamati bado ina wasiwasi wa kuwepo ukwepaji wa kulipa kodi hususan katika Sekta ya Mafuta ya Kula kutokana na kuwepo na mianya ya kukwepa kulipa kodi, kunakofanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu, ambapo mafuta ya safi yanaingizwa nchini na

hatimaye kutolewa maelezo kuwa ni mafuta ghafi yanayotumika kutengeneza mafuta ya kula na bidhaa nyingine kama vile sabuni.

Kamati imeridhika kwamba, Serikali inafahamu kuwa, kwa kipindi kirefu takriban karibu miaka 10 iliyopita, imekuwa ikipoteza mabilioni ya fedha kutokana na ukwepaji huo wa kulipa kodi. Ni maoni kwamba, mikakati ya kuwabana wafanyabiashara hao, iongezewe nguvu na pili, Serikali iweke mikakati ya kutoa elimu kwa Wananchi na wadau mbalimbali wenye viwanda vya mafuta juu ya kilimo cha zao la mawese, ambalo linalimwa katika Mikoa ya Kigoma, Mbeya, Tanga na linaweza kustawi sehemu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeafiki nia ya Serikali ya kutoa msamaha wa *VAT,* kwa vifaa vya usafi wa akina mama, pamoja na dawa za mbu za kuchoma pale vinapouzwa na wafanyabiashara siyo wazalishaji na kwa wale wanaoviagiza kutoka nje ya nchi. Kamati inashauri ili kuvilinda viwanda vya hapa nchini na kuchochea kasi ya uzalishaji, kipaumbele cha misamaha ya kodi kitolewe kwa wazalishaji wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia inaipongeza Wizara kwa kusogeza huduma ya usajili wa vizazi na vifo kuletwa katika ngazi ya Wilaya. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kwamba, iendelee kutafakari suala hili ili huduma hii isogezwe mpaka kwenye ngazi ya Kata, kwa nia ya kuondoa kero kwa Wananchi ya kusafiri na kutumia fedha na muda mwingi kufuatilia vyeti vya Makao Makuu ya Wilaya na hata wakati mwingine kutozwa rushwa na wale wanaovishughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano ya kina, Kamati iliupitisha Muswada na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa jitihada anazochukua za kurekebisha sheria mbalimbali za fedha ili ziendane na wakati tulionao hivi sasa. Kamati pia iliipongeza Serikali kwa jitihada kubwa ambazo imekuwa inafanya za kukuza uchumi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE GRACE S. KIWELU (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kutoa maoni ya Kambi hiyo juu ya Muswada wa fedha wa mwaka 2005 kama ulivyowasilishwa na Waziri wa Fedha. Kuna baadhi ya maeneo ambayo Kambi imeona ni vema kuyatolea ushauri au kupata ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya Muswada ambayo inahusu Sheria ya Mfuko wa Elimu wa mwaka 2001, Waziri anapendekeza kufuta kifungu cha 12 vifungu vidogo vya tatu na tano, ambavyo vinaondoa msamaha wa Kodi ya Mapato, Kodi ya Ongezeko la Thamani na Ushuru wa Forodha kwa wachangiaji wa Mfuko, ili wachangiaji sasa wapate punguzo hilo kwa mkondo mmoja tu wa kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato wa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani, haina pingamizi na hatua hii ila ingependa kupata maelezo kutoka kwa Waziri, je, kumefanywa tathmini ili kujua mafanikio au hasara iliyopatikana kutokana na utaratibu wa sheria ya awali ya mwaka 2001?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunauliza hivyo kwa kuwa Bunge lako Tukufu, huwa linapitisha Miswada na hatimaye kuwa na Sheria na halafu siyo muda mrefu sheria hiyo hurudishwa tena Bungeni kufanyiwa marekebisho katika kipindi cha muda mfupi kutokana na kutofanyiwa utafiti wa kutosha wakati wa matayarisho ya Muswada wenyewe. Aidha, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi kuwa, mabadiliko haya yanayopendekezwa yanaweza kuwarudisha nyuma wale waliokuwa wakichangia Mfuko huu wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 332, ambayo inakusudia kuweka viwango vya ushuru wa bidhaa kulingana na mfumuko wa bei, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi kuwa viwango vilivyowekwa, havijaangalia kwa undani pato la mwananchi la kila siku. Baadhi ya bidhaa zinazopendekezwa ni zile ambazo Watanzania wengi wa hali ya chini, huzitumia katika kufanya biashara ili kuweza kumudu maisha yeo vyema kwa kunyanyua vipato vyao. Kwa kuweka viwango vya ushuru kuwa asilimia tano ni kuwanyima nafasi Wananchi katika kujiendeleza kibiashara. Kwa mfano, *HS Code* Namba 2710, 1922, *Eliminating Kerosine,* ambayo yanatumika zaidi kila siku ya uhai wa Mtanzania ni sawa na kumwongezea ugumu katika maisha na kumfanya azidi kudidimia katika dimbwi la umaskini. Waziri hatukumwelewa katika badiliko hili, tunaomba ufafanuzi, lakini kama maelezo yetu ni sahihi, Kambi ya Upinzani haikubaliani na badiliko hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hivi sasa tunajenga ushindani wa kibiashara na kwa kuwa tunakoelekea, mfumo wetu wa kodi unakuwa mmoja kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kambi ya Upinzani inashauri kila badiliko la Sheria linaloletwa, ambalo hatimaye litawahusisha Watanzania ni vema Waziri akawa anatoa ulinganisho ili tujue hatma ya mfumo wetu wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tumejifunza kuwa baadhi ya sheria tunazozitunga katika utekelezaji wake, huwa kuna gharama kwa mfano, sheria ya vitambulisho vya uraia, ambayo gharama yake sasa imefikia shilingi bilioni 100 hivyo, wakati umefika wa kujua na bajeti za utekelezaji wa kila sheria ambayo inapotekelezwa, itakuwa na gharama ili Bunge lielewe *Financial Implication.* Mfano mzuri ni hizi sheria za kodi ambazo Waziri huwa anatuletea hasara au faida inayopatikana kutokana na mabadiliko yanayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo ya ujumla, Kambi ya Upinzani inakubaliana na mapendekezo yaliyosalia na yaliyobakia, yote tutayakubali baada ya kupata ufafanuzi wa kifungu cha 27, 10, 19 na 22.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, nimepata wachangiaji wawili tu na wanatosha, maana shughuli hii ni lazima tuimalize kwa kipindi hiki cha asubuhi.

Sasa namwita Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Leonard Derefa.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kuhusu Muswada huu uliowasilishwa na Waziri wa Fedha.

Kwanza, naunga mkono Muswada ulioletwa. Nataka nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu wote na Wafanyakazi wote wa Wizara ile, kwa kazi nzuri wanayoifanyia Serikali yetu. *(Makofi)*

Sasa ninayo mambo miwili ambayo ningependa kuyasema. La kwanza, ni kuhusu Usajili wa Vifo na Vizazi. Nilipokuwa Jimboni nilikuta malalamiko ya waziwazi kwa Wananchi kwa sababu ingawa gharama ya kulipa mtu anapokwenda kusajili ni shilingi 3,500/=, unaweza ukaona ni ndogo lakini gharama ni kubwa kwa sababu kwa mfano, kwenye Jimbo langu ili mtu atoke kwa mfano, Kamsamba au atoke Mambwekenya kwenda Sumbawanga Makao Mkuu, kwa ajili ya kusajili vizazi na vifo nauli yakwenda na kurudi ni shilingi 20,000/=. Kwa hiyo, atakuwa amekwenda kusajili kifo kwa zaidi ya shilingi 20,000/=, hatujaweka gharama ya kulala. Sasa haya yote yanafanyika hata Serikali kusema wamejitahidi sasa kufika Wilayani ni kwa sababu tumezoea sana kuhodhi madaraka Makao Makuu ya Serikali, hatujazoea kupeleka madaraka kwa Wananchi. Sasa kuna ugumu gani wa kufundisha Watendaji wa Kata ili wao ndio wafanye kazi hiyo. Haya malalamiko na manung'uniko ni makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu vilevile tufikirie tu kwa akili ya kawaida tu, mimi nimefiwa halafu nisafiri kwenda Sumbawanga kwa ajili ya kusajili kifo cha mtoto wangu, halafu nigharamie na fedha, haieleweki. Nina faida gani kwenda kusajili kifo cha mtoto wangu alikufa wakati ninalia, halafu nitoe fedha za nauli kwenda kusajili kifo, haieleweki. Ni msiba mwingine huo Waheshimiwa Wabunge wanasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninataka niliseme hili, ni malalamiko makubwa sana na tumezua malalamiko na Serikali inaona yenyewe kwamba, ilipokuwa Dar es Salaam hakuna mtu aliyekuwa anashughulika. Sasa kwa kuwa tumeendelea na teknolojia inaongezeka, nashauri yaanzishwe mafunzo maalum ili kazi hii ya kusajili vifo na vizazi, ifanyike katika ngazi ya Kata na baadaye tunaweza kwenda katika Kijiji.

Kwa hiyo, huo ndiyo ushauri wangu na ninaomba katika jambo hili, najua watasema unajua ni mwanzo mzuri, ndiyo tumefika kwenye Wilaya. Lakini naomba tuseme rasmi kwamba, nia iwe ni kwenda kule waliko Wananchi wengi na mipango hiyo ianze kuandaliwa kwenda kule waliko Wananchi, wengi haya ni manung'uniko makubwa sana kutoka kwa Wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, mimi pia nataka niipongeze Serikali na Wizara kwa kutazama hasa ile Waziri aliyosemea kuhusu mafuta ambayo hayo hayo ni ya kupikia na mengine ni ya kutengenezea sabuni. Ujanja huo unaotumika wa watu kukwepa kulipa kodi, vyombo vyetu ndivyo vinaukaribisha. Kama Serikali inasema hakuna *crude oil* na *Customs* wanapitisha *crude oil* kuna nini? Kwa hiyo, naomba kweli kabisa, jambo hili tusilifanyie mzaha na kwa upande wangu, sitaki kusema maneno mengi. Lakini kwa upande wangu, miaka sita, saba, iliyopita nilikuwa nasema habari ya mafuta ya kupikia na ilishapata kumgharimu mtu kazi na watu wote wanaelewa na bado msimamo wangu ni ule ule kwamba, suala la mafuta ya kupikia kupewa jina la *crude oil* wakati hakuna *crude oil,* lazima jambo hili Serikali kwa kuwa imelitambua na imeliona, iliangalie kabisa si sawa na wala si haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nchi yetu ni nzuri na ina ardhi nzuri. Mimi mwenyewe nilikwenda Malaysia mara mbili, wakati nikiwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, tulitengeneza mpango kabambe wa kulima michikichi katika Mkoa wa Kigoma. Sasa kwa sababu Tanzania mtu anasafiri na mipango yake tulipoondoka ile keki imekufa hakuna. Tanzania ina eneo kubwa kuliko Malaysia, linaloweza kulimwa michikichi na Malaysia hawakubali kutoa mbegu kwa nchi yoyote wala kuuzia nchi yoyote mafuta yanayoitwa *crude oil* isipokuwa Misri. Nataka niseme *on record,* nilipokuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na kwa kuwa nilikwenda mara mbili Malaysia, nilipata bahati ya kuonana na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa kule wakati ule. Alipokuja Tanzania kwa ziara rasmi, nilialikwa Ikulu na Waziri Mkuu wa Malaysia alisema naipa Tanzania nafasi ya upendeleo nitawapeni mbegu ya michikichi ambayo huwa hatuitoi nchi yoyote. Lakini mpaka leo Serikali haikushughulika. Kwa sababu ugonjwa wetu ni kuagiza vilivyotengenezwa na watu wengine.

Mheshimiwa Spika, nchi nzuri kama Tanzania, tutaendelea kuagiza mafuta ya kupikia. Hivi ugomvi wote huu wa kodi na wafanyabiashara tunautafuta wenyewe. Tungeweza kusema miaka mitano ijayo hakuna kuingiza mafuta ya kupikia kutoka nje. Lakini hakuna anayeamua. Hakuna anayeamua kwa dhati kabisa kwamba, tuache jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaiomba Wizara ya Fedha, sisi Wajumbe wa Kamati ya Fedha, tuliridhika sana na kazi ya Mheshimiwa Basil Mramba, kwa sababu kila tulichozungumza na kukubaliana, alifanya. Kwa hiyo, sisi tunaomba Wizara ya Fedha, itoe mwongozo kuziambia Wizara zote ambazo bado zina kasumba ya ku-*import* vitu vinavyotengenezwa nje, waambiwe waache mchezo huo tuwe na mipango ya kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu vilevile lazima hili niliseme kwa moyo wangu, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, anaondoka anaiacha nchi katika hali nzuri sana ya kuweza kuendeleza uchumi, kwa hiyo, hatuna kisingizio na hakuna mtu wa kutoa kisingizio sasa. Maana kama ni madeni, amejitahidi tumefutiwa na kwa kufutiwa madeni sasa tunaokoa dola milioni tano kwa mwezi. Nilifurahi sana, Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, aliposimama alikiri kwamba, nilivyosema ni sawa na mara nyingi napenda kusema jambo ambalo nina uhakika nalo, siwezi kuzua mambo ya ovyo

hapa. Sasa hizo fedha zitumike vizuri, hatuna zawadi ya kumpa Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa, lakini tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu, ampe afya njema ashike mkongojo. *(Makofi)*

Pili, anaondoka anaacha nchi hii inakopesheka, tuna sifa kubwa dunia nzima. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge mtakaochaguliwa na Mawaziri mtakaoteuliwa, msitafute visingizio, msingi aliouweka Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa ni sawasawa na kusema sasa ndege i-*take off,* ameshaweka mazingira ya ndege kuruka. Sasa hakuna kisingizio katika Serikali ya ijayo, maana nina uhakika kama nilivyosema Serikali itakayoingia madarakani ni ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba tena kuunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyo mbele yetu. Kwanza, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii, kuishukuru sana Serikali ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa na Wizara ya Fedha, ambao kwa kweli wametuwezesha kuwa na fedha za kutosha na kwa hiyo kukidhi mahitaji na mapungufu na kutatua kero mbalimbali ambazo zilikuwa zinakabili nchi yetu. Kwa hiyo, nawapongeza sana vilevile na Wizara zote ambazo kwa kweli wameshirikiana katika kutatua matatizo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningelipenda sana nimpongeze Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha, hasa katika kusaidia kuboresha mapato. Lakini ninaamini kabisa kwamba, mapato yangeliweza yakaboreka zaidi kama Serikali ingeliweza ikajaribu kuweka vyombo vya udhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la udhibiti, ningelipenda niseme kwamba, kuna baadhi ya Mashirika ambayo wangeliweza wakawa wanalipa kodi nzuri ama kodi kubwa zaidi kama Serikali ingeliweka udhibiti wa kutosha. Niliwahi kuuliza swali hapa kwamba, kwa nini kwa mfano, haya Mashirika ya Michango ya Watumishi kama *LAPF, NSSF, Insurance Companies, PPF* na *GEPF.* Nilikuwa nasema kwamba, haya Mashirika tungeweza tukaweka utaratibu mzuri na yenyewe yakawa yanapata udhibiti. Tunaamini kabisa kwamba, *Commercial Banks* zote zinadhibitiwa na Benki Kuu. Lakini je, nani anadhibiti hayo Mashirika kwa mfano, tumeona baadhi ya Wananchi ambao walikuwa wameweka fedha zao, kwa mfano, kwenye *Insurance Companies* wakati mwingine *insurance* zinaiva lakini wanashindwa kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kwamba, Mashirika haya yanakaguliwa na watu binafsi, utakuta ile *relationship* kati ya Mkaguzi na Mkaguliwa ni kama ya mtoto na baba, utakuta inawezekana hata taarifa zao wakati mwingine haziaminiki sana kwa sababu tumejifunza huko nyuma kwamba, kulikuwa na Mashirika ya Umma, ambayo yalikuwa yanakaguliwa na *Tanzania Audit Corporation* na wanaonesha yanafanya faida

na watu wanalipwa *bonus* lakini wamekuja kugundua ghafla kwamba, hata faida ilikuwa haipatikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nina wasiwasi vilevile kwamba, kama Mashirika ambayo yako *sensitive,* nilikuwa naomba kwamba, yawe yanakaguliwa kwa kumshirikisha Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa mfano, maana yake ukisoma kwenye *scandals* ambazo zimeweza kutokea hata nchi za nje kwa mfano, *Heneron Scandal, World Com, Pamarade, Bristol Mayor, Squible Company* na mengine na hapa yalikuwa yanafanyika kwamba, unakuta mkaguzi anakagua anatoa kabisa ripoti ya kwamba, kampuni inafanya faida kumbe hata faida hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye *Companies* ambazo ziko *sensitive* na Kampuni ambazo zinalinda uchumi wetu ni vyema zikakaguliwa kwa kushirikiana na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali, pamoja na kwamba, wanaweza wakawa na Mkaguzi mwingine, lakini Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali, sharti na yeye awepo ili alinde maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika haya, ningependa niyataje kwa mfano, *National Bank of Commerce* ya sasa, ambayo inatunza rasilimali zetu, halafu Benki Kuu, *Tanzania Harbours Authority,* Mashirika haya lazima yasaidiwe kukaguliwa. Lakini jicho la Serikali liwe vilevile Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali na yeye ahusishwe ili kulinda maslahi yetu, wakiwemo pamoja na wawekezaji wakubwa wa madini na viwanda vikubwa ambavyo vinalinda uchumi wetu kwa mfano, *Tanzania Breweries, Cigarette Company* na Mashirika makubwa ya namna hiyo. Kwa sababu pamoja na kwamba, kwa mfano, *Tanzania Audit Corporation* ime-*collapse,* lakini kuna *Tanzania Audit Associate,* ambayo sasa hivi inakagua. Kwa hiyo, si kwamba, siwaamini, lakini kutokana na ukishaumwa na nyoka hata kamba inakutisha. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ningelipenda niishukuru sana Serikali kwa kuwarudisha na kuanza kuwalipa wastaafu. Lakini kitu ambacho nimeshangaa huko Jimboni kwangu, kuna baadhi ya wastaafu ambao walitakiwa kuwa wameanza kulipwa, lakini bado hawajaanza kulipwa na kwa bahati nzuri, nilijaribu kumwandikia mhusika katika Mkoa anayeshughulikia kuwalipa kwenye *Sub-Treasury,* sikupata majibu. Badala yake wakaambiwa kwamba wanashughulikiwa, mpaka sasa hivi kuna baadhi ya wastaafu ambao wame- *qualify* lakini hawajaanza kulipwa. Nilikuwa naomba suala hili lijaribu kutazamwa limekwama wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa niongelee, siku mbili, tatu, hizi zilizopita, niliuliza swali kuhusiana na *exchange rate* kwamba, mfumuko wa *exchange rate,* ninaweza nikasema labda ni *traditional economist.* Mfumuko wa *exchange rate* una madhara kwenye uchumi hasa katika maisha ya Wananchi. Kutokana na kwamba, Tanzania ni *net import,* chochote tunachokitengeneza hata hapa nchini, zile *component* au vile vifaa tunavyovitumia lazima tuviagize. Ni kweli hata kwa mfano, katika viwanda vya pamba, tunapotengeneza pamba na baadaye tunapoiuza kwamba, *exchange rate* iko juu. Lakini kwa kuwa vitendea kazi tunavyovitumia kwa mfano, kama mafuta tunayaagiza, *spare parts* tunaziagiza pamoja vitu vingine tunavyovitumia vyote

vinatoka nje na kwa hiyo, utakuta vinakuja na bei kubwa hata kama tunapata bei kubwa tunapouza ile faida pale siioni.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa pamoja na kwamba, nilijibiwa nikaambiwa *exchange rate* inapokuwa kubwa inasaidia wakulima, sioni kama inawasaidia. Kwa sababu ingelikuwa vizuri kama tungelikuwa na vitendea kazi kwa mfano, *spare parts,* vipuri vyote tulingekuwa tunatengeneza sisi hapa, kweli hiyo ingeweza ikaonekana kwamba, inasaidia uchumi. Suala hili pamoja na kwamba, tunaliona labda halileti madhara, lakini naona lina madhara makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mafuta sasa hivi kadri ya *exchange rate* inapokwama yanazidi kupanda. Miaka miwili iliyopita, Shinyanga tulikuwa tunanunua mafuta kwa shilingi 500 kwa lita, sasa hivi wananunua mafuta kwa shilingi 1,200 kwa lita. Kwa hiyo, utakuta hali ya maisha inakuwa ni ngumu sana. Halafu hata utendaji na utengenezaji wa vitu ambavyo tunatakiwa tuvi-*export* vinakuwa na gharama kiasi kwamba, wakati mwingine wafanyabiashara wanashindwa kumudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka kulisemea, tuna utaratibu ambao naamini, Serikali imeweka *control* kwa mfano, katika uagizaji wa mafuta ya petroli. Lakini bado ninaona kwamba, bado nafikiri kuna kasoro na Serikali nilikuwa naishauri ijaribu kufuatilia zaidi kwa sababu ukitazama unaposafiri kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, unakuta kuna *Filling Stations* nyingi, ambazo zinajengwa njiani mle, sijui zinauza mafuta kwa nani? Lakini ukisafiri njia ya kutoka Dar es Salaam kwenda Lindi, huoni *Filling Station!*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri kwamba, inawezekana *Filling Station* ambazo zimejengwa kwenye njia ya Dar es Salaam kuja Dodoma, zinatumika kwa kuuza mafuta kweli ama zinatumiwa katika kuleta mafuta ambayo inawezekana yanaagizwa ni *transit oil* ambayo inakwenda labda Rwanda, Burundi, pamoja na labda *North Zaire,* Kongo kule. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri suala hili ni vema wakalitazama sababu kama kweli ni biashara ya mafuta, kwa nini njia ya Dar es Salaam kwenda Lindi haina *Filling Station* nyingi kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba mambo haya vilevile wajaribu kuyaona na kuyawekea mikakati. Ninaamini kabisa kwamba, mikakati mizuri ikiwekwa tunaweza tukapata mapato makubwa zaidi na kuweza kutatua matatizo na kero mbalimbali za Wananchi wetu wa Tanzania na hatimaye kuwafanya waweze kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda niseme ninaunga mkono hoja hii tena. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi niseme kwamba, ninakubaliana na mawazo ya Kamati ya Fedha kwamba, ndivyo tulivyozungumza na tumepeana kazi ya kufanya ambayo niliahidi jana kwamba, Wizara ya Fedha itaendelea kufuatilia. Lakini ningependa nisahihishe jambo moja, bahati

mbaya simwoni msemaji lakini acha iingie kwenye *Hansard.* Jana kwenye Kamati tulizungumza juu ya *GN 1* moja iliyotolewa kuhusiana na kiwanda fulani cha Nguo, nadhani kinaitwa *Lakhan* na nilisema pale kwamba, sikumbuki kama nilitoa *GN* hiyo. Ningependa iingie kwenye rekodi kwamba, ni kweli nilitoa hiyo *GN* mwezi Juni, nimekuja kugundua hivyo. Kwa hiyo, hoja ile tutaifuatilia, ilikuwa hoja ya watu watatu, kwa nini moja ilitolewa na wengine hawakupata. Nilitafuatilia hao wengine ili kuona namna ya kurekebisha kasoro yoyote iliyojitokeza kutokana na hali hiyo. Nilitaka hiyo iingie kwenye rekodi isije ikasemekana kwamba, niliidanganya Kamati. Lakini mengine yote ni kweli kama alivyosema na tutaendelea kutekeleza kama tulivyokubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na hoja ya Kambi ya Upinzani, kwa kweli hakuna matatizo. Hili la asilimia tano ni jambo ambalo tulilieleza na lilipita kwenye bajeti kwamba, tuliongeza ushuru kwenye bia, soda kwa asilimia tano na tukasema hili alilokuwa anasema Mheshimiwa Leonard Derefa hapa kwamba, ilitokana na kitu kinaitwa *adjustment for inflation,* yaani unarekebisha kitu ili kilingane na mfumuko wa bei ulivyo. Ni jambo la kawaida na ni zuri na kusema kweli hata wenye viwanda wenyewe hawalalamiki, kuonesha kwamba ni jambo zuri hata wenye viwanda ambao ndiyo wanaokamuliwa hawalalamiki. Kwa hiyo, kama unakamua ng'ombe na hapigi teke, una uhakika ng'ombe ameridhika na mkamuaji atakuwa ameridhika. Kwa hiyo, hilo lisituletee wasiwasi.

Mheshimwa Naibu Spika, la pili, kulikuwepo na hoja nyingine ya Kambi ya Upinzani kwamba, hii *adjustment* tunayoifanya kwenye kifungu cha 16(1) yako mambo mawili. Kumekuwepo na msingi kwamba, watu au makampuni yakichangia shughuli za kijamii elimu, afya, maji, wakichangia wanapokuja kutozwa kodi ya mapato mchango ule uondoshwe kwa sababu ulienda kwa jamii hakuingia kwenye mfuko wake. Kwa hiyo, kwa wanaochangia mfuko wa elimu ule tunaoufahamu hapa Mfuko Maarufu ule, kwenye bajeti hii tulisema kwamba, wawe wanaleta maombi wakati wa kulipa kodi ya mapato kwamba, walichangia kiasi fulani kwenye Mfuko ule ili kiasi kile kipunguzwe kwenye kodi yao ya mapato, hiyo ilikuwa kwa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa baadhi ya Mbuga za Wanyama, swali la leo asubuhi kwamba, mara nyingine nao wanatakiwa walipe asilimia 25 kama alivyoeleza Waziri wa Maliasili na Utalii hapa leo asubuhi, wanatakiwa walipe asilimia 25 ya mapato yao kusaidia maendeleo ya vijiji vinavyowazunguka. Hadi sasa wanapofanya hivyo, *National Park* Maarufu ni Ngorongoro. Huko nyuma tulikuwa hatuwasamehi kodi. Sasa tunasema wanapotoa zile nao wanaweza wakaja wakazidai kwenye kodi kwenye kodi ya mapato, tukawaondolea kwa sababu wamesaidia maendeleo ya Wananchi kwa mujibu wa Sera ya Serikali na kwa mujibu wa uhusiano wao mzuri na Wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunasema njia ya kudai malipo ya namna hiyo iwe ni moja tu kupitia kodi ya mapato. Unapojaza zile fomu za kusema mapato yako yalikuwa hivi, gharama zako zilikuwa hivi, kwa hiyo, kodi yako ya mapato ilikuwa hivi, pale tu ndipo tutazungumza lugha hiyo. Mtu asije akawa anadai kila anapotoa, akitoa mwezi Juni anaenda kudai, akitoa mwezi Julai anaenda kudai, akitoa mwezi Agosti

anaenda kudai, hapana adai mara moja tu ile siku ya kutoa maelezo kuhusiana na mapato na matumizi kwa masuala ya kodi. Ndivyo tunavyosema na hili ni jambo zuri, limekuwepo, tunaliweka kwenye mkondo mzuri tu wa kulitawala ili kila mtu aweze kuelewa kinachoendelea ni nini na kila mtu aweze kuwa na uhusiano ambao unaeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo lilikuwa linasumbua Kambi ya Upinzani ni gharama za sheria. Ni kweli kimsingi kila mara Serikali inapoamua jambo, huwa inazingatia gharama. Maamuzi yote ya Baraza la Mawaziri yanazingatia gharama. Nataka kutunga sheria hii ili sheria hii itekelezwe, itaigharimu Serikali *XYZ,* hili kila mara lipo. Lakini huwa hatuleti hapa Bungeni, lakini ndani ya Baraza la Mawaziri, *paper* haipiti mpaka tujue gharama ni kiasi gani na wanaodai sana hizo gharama ni sisi Hazina kwa sababu kila gharama ni kodi, lazima nitafute hizo fedha mahali. Lakini Serikali kila mara haifanyi kama wafanyabiashara kwamba, kama hiki kitu ni gharama basi ikiache. Serikali inatunga sheria kwa gharama ndogo kiasi iwezekanavyo. Serikali haiwezi kusema kwa sababu gharama ni kubwa kwa hiyo inaacha, kwa sababu gharama ni kubwa, kwa hiyo, situngi sheria ya kudhibiti wahalifu, Serikali haiwezi kusema hivyo kwa sababu wahalifu wataongezeka. Kwa hiyo, kuna baadhi ya Sheria ambazo hata kama gharama ni kubwa, lakini huna namna kama kuna namna fanya iwe ndogo zaidi, kama huna namna na kazi ya Serikali ni kutawala na kuleta amani na utengamano katika jamii, lazima ile gharama itabidi ipatikane na ndiyo tunaleta hapa Bungeni kusema jamani, kwa sababu hizi na hizi, tunaomba mtupe fedha kiasi hiki na hiki na ndiyo maana mnatoa fedha nyingi sana, hata sasa hivi mnatoa fedha nyingi sana kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kadhalika na kadhalika. Nilitaka kufafanua hilo lakini ni kweli kama Kambi ya Upinzani ilivyosema kwamba, Serikali inazingatia sana gharama za kutekeleza jambo lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwepo na wasiwasi juu ya mafuta ya taa. Narudia kwamba, kwenye bajeti iliyopita, hatukuzungumzia kabisa habari za kuongeza kodi kwenye mafuta yoyote, badala yake tulizungumzia kupunguza kodi kwa mafuta yake *Jet A1,* ambayo ni mafuta ya ndege, yanatumika tu kwenye ndege. Sasa ni kweli kwenye Muswada hapa tumeonesha gharama nyingine ile tumeonesha tu ili ule uwiano ujulikane kwamba, bei itakuwa hivi kwa bidhaa hii, hakuna mabadiliko na hii kuna mabadiliko. Ndiyo maana mkisoma vizuri kwenye ule Muswada, mtaona kwenye *Jet A1* tumeweka *Nil* na kule nyingine tumezitoa kama zilivyo. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Grace Kiwelu kwamba, hakuna ongezeko kabisa lililojitokeza kwenye mafuta kutokana na bajeti hii ni hilo moja tu la kupunguza mafuta kwenye *Jet A1.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani sasa tumeelewana. Kulikuwepo na wasiwasi kwamba, mbona kila mara mnabadilisha badilisha sheria, inakuja baada ya mwaka mmoja au miaka miwili, mnaibadilisha na kadhalika. Mbona hiyo nilifikiri ni sifa kwa sababu huwezi kukaa na mzigo tu, jambo ambalo tayari ni mzigo uendelee kukaa nalo tu kwa sababu halijakomaa. Mwaka 2004 mwishoni nilileta pendekezo hapa la kufuta ile Sheria ya Manunuzi ya Serikali, ni sheria ya mwaka 2001, tumeifuta mwaka 2004 kwa sababu tuliona tayari zimeanza kujitokeza kasoro, mambo yamebadilika ni lazima tuletee

sheria mpya ya kuboresha zaidi suala la manunuzi ya Serikali. Kwa hiyo, ni kweli kabisa, unaweza ukatunga sheria mwezi Januari na ukaifuta mwezi Desemba mwaka huo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sababu Sheria ni *dynamic,* sheria ni jambo ambalo saa zote linabadilika kutokana na mabadiliko katika jamii au katika suala lenyewe au katika miondoko ya Kimataifa, huwezi kubaki na jambo ambalo duniani wanafanya vitu tofauti. Ndiyo maana na yeye mwenyewe amesema kwamba, sheria hizi za Afrika ya Mashariki ni lazima ziendane na ziwiainishwe na sheria za nchi moja moja na ni kweli. Likitoka jambo huko Afrika ya Mashariki sasa hivi kama nilivyoeleza, mara moja linakuwa ni la hapa nchini, lakini jambo lile linaweza likaleta mgongano na sheria za hapa nchini.

Kwa hiyo, huwa tunatekeleza kwa sababu sheria ya Afrika ya Mashariki sasa inakuwa na nguvu zaidi kuliko sheria za hapa nchini. Lakini pale ambapo ni lazima kurudi Bungeni kubadili mambo kwa sababu labda ndivyo sheria yenyewe ilivyokuwa, lazima tunarudi hapa Bungeni. Kwa hiyo, huko tuendako tunaweza kuona mabadiliko yakitokea mengi sana kwenye sheria za Ushuru wa Forodha ambazo zinahusu Afrika yetu ya Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mheshimwa Dr. Chrisant Mzindakaya, nakubaliana naye na ninamshukuru kwa mawazo yake na jana aliyatoa kwenye Kamati kwamba, kwa kweli hasa hili la vifo sisi Wizara ya Fedha, tumekuwa tukisikiliza maswali mengi sana hapa Bungeni ya Waheshimiwa Wabunge, kuhusiana na usajili wa vizazi na vifo na tukaona labda tusaidie kwa sababu jambo hili haliko ndani ya Wizara ya Fedha, lakini liko kwenye Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba na Waheshimiwa Wabunge, wanalalamika na Wananchi wanalalamika. Kwa hiyo, tukasema kwa sababu labda itachukua muda mrefu kuangalia sheria nzima na kuona nini kifanywe, lakini angalau basi tuondoe lile sharti la watu kwenda Dar es Salaam badala yake waweze kufanya vitu hivyo hapo Wilayani mwao kama baadaye mambo haya yatasogezwa mpaka Vijijini.

Kama jana kulikuwepo wazo kwamba, kwa nini lisifanywe ngazi ya Kijiji. Mwingine anaweza akasema kwa nini lisifanywe ngazi ya kitongoji. Kwa sababu hizo hizo, nimefiwa lakini unataka nitafute nauli ya kwenda Wilayani. Kuna Wilaya nyingine ni mamia ya kilomita kutoka vijiji fulani. Kwa hiyo, jambo hili itabidi liangaliwe vizuri zaidi, lakini kwa sasa hivi Wizara imeomba tuwasaidie ili angalau wasogeze huduma hii mpaka Wilayani, pindi wakiangalia njia bora zaidi ya kulifanya. Kwa hiyo, tumaini langu ni kwamba, Wizara ya Sheria itaendeleza jambo hili ili liweze kulingana na hali halisi ya vijiji vyetu.

Mheshimiwa Leonard Derefa, alionesha wasi wasi ambao na sisi tunao Serikalini, juu ya Mamlaka ya Pensheni, *NSSF, PPF, Local Government Pension Fund* na mifuko mingi ya pensheni, udhibiti wake unakuaje? Sisi tunasema kwamba, udhibiti sio ule tu wa ukaguzi wa fedha ni udhibiti pia wa mfumo. Kwa hiyo, sasa hivi Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu na kwa kweli kwa uamuzi wa Serikali, tunafanya uchunguzi kuona

namna gani mifuko hii inavyoweza kusimamiwa. Mifuko yote hii iwe na kitu kama Wakala *(Regulator)* wa kuisimamia. Sababu kubwa ni kwamba, Serikali inadhamini mifuko yote hii. Sasa huwezi kudhamini kitu ambacho hujui hasa kinaelekea wapi.

Pili, Mifuko hii katika nchi nyingi duniani, inatumika sana kufanya mambo yenye manufaa katika jamii. Kwa hiyo, ni lazima tujue fedha zao wanawekeza wapi. Ukiangalia Mifuko hii, muda wote huu wamekuwa wakiwekeza zaidi kwenye majengo, lakini kuna mahitaji mengine ya mikopo. Sasa ni maeneo gani Serikali inaweza ikaelekeza ikasema kwa mfano, Mifuko iwe inagharamia jambo fulani katika jamii, jambo fulani katika uchumi na kadhalika, kwa mfano, jambo hili la miundombinu? Unaweza ukasema labda Mifuko hii sasa tuitumie kupeleka umeme vijijini au kusambaza simu na kuna mambo wanaweza wakafanya kwa maelekezo ya Serikali kulingana na sera na kadhalika. Kwa hiyo, utafiti huo unaendelea na ukikamilika, nina hakika labda Bunge tutakuja kuarifiwa hatma yake, ninahisi labda itatoka sheria angalau kutakuwepo na Wakala za kusimamia hii Mifuko.

Mengine ni ushauri tu, ni kweli kuna njia nyingine ambazo zina vituo vingi vya petroli na nyingine hazina. Kwa lugha ya kawaida watu wanasema, kwenye vituo vingi ndio huko kwenye wizi wa mafuta, labda na ukwepaji wa kodi. Lakini sio lazima kwa sababu ukilinganisha kwa mfano, njia ya kwenda Lindi, Mtwara na njia ya kwenda Mwanza kutoka Dar es Salaam, zote kutoka Dar es Salaam ni dhahiri kwamba, kuelekea Mwanza kuna vituo vingi zaidi kwa sababu barabara hiyo ina magari mengi zaidi, yaani soko ni kubwa kuelekea Mwanza kuliko kuelekea Kusini, kwa hiyo, utategemea vituo vingi kwa sababu hawa hawawezi kuweka bila kujua soko litakuwa wapi. Kwa hiyo, naweza nikasema hivyo tu.

Sasa haya mengine ya *exchange rate* na bei na kadhalika, ni somo kubwa naulizwa ulizwa maswali hapa, lakini tunalitambua na tunakiri kwamba, kuna uhusiano lakini ni jambo kubwa na pana zaidi ambalo mara kwa mara tunasimamiwa na Benki Kuu, Wizara ya Fedha na Wizara ya Mipango, kuangalia namna ya kuweka uchumi katika hali ambayo haitaweza kuleta madhara zaidi kwenye maisha ya watu na kwenye uchumi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru hawa wasemaji wanne, kwa mawazo yao mazuri. Kama nilivyosema, sisi tulikuwa tunataka tu uhalali wa kisheria, twende tukatekeleze yale ambayo yalipita hapa wakati wa bajeti na tuanze kutafakari haya yote yaliyotoka wakati wa bajeti kama mawazo na leo kwenye Muswada huu, kwa maana ya kujiandaa kwa bajeti ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naomba tena kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2005**
***(The Finance Bill, 2005)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yaliyofanywa)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9
Ibara ya 10

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yaliyofanywa)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yaliyofanywa)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yaliyofanywa)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yaliyofanywa)*

Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34

Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*
*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2005**
***(The Finance Bill, 2005)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2005 kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba, taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**M A A Z I M I O**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nitakapokuita nitakuomba usome Maazimio yote mawili ili yachangiwe kwa pamoja lakini wakati wa kuhoji yatahojiwa mbalimbali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, likubali kupitisha Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha, Kufuta au Kusamehe Madai au Hasara Ambazo Hazilipiki Zitokanazo na Upotevu wa Fedha na Vifaa vya Serikali kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2005, kwa

mujibu wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma ya mwaka 2001*(The Public Finance Act, 2001).* Aidha, Azimio hili lilipata ridhaa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* katika kikao chake cha tarehe 20 Julai, 2005 kilichofanyika hapa mjini Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za dhati, kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge za Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, pamoja na wajumbe wote wa Kamati hiyo, kwa maoni yao mazuri, yenye lengo la kuboresha udhibiti na uimarishaji wa usimamizi wa mali na vifaa vya umma, kwa lengo la kupunguza upotevu wa mali na vifaa hivyo. Ushauri wao umezingatiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio ninalowasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, linakusudia kufuta na kusamehe madeni, hasara na potevu ambazo hazilipiki kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa ambayo naiwasilisha mbele ya Bunge hili, hasara husika zimegawanyika katika sehemu kuu tatu. Mgawanyiko huu, umelenga kuainisha kwa uwazi hasara hizo ili Waheshimiwa Wabunge, waweze kuzielewa vizuri na hatimaye kufikia uamuzi ulio sahihi. Hasara hizo ni kama ifuatavyo: Zile zinazohusu potevu wa fedha, vifaa na malipo batili yenye thamani ya shilingi 1,554,298,253/30; zile zinazohusu mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa ya shilingi 52,775,465,687/41; na zile ambazo zinahusu usawazishaji wa kumbukumbu katika vitabu shilingi 2,465,438,060/05. Jumla ni shilingi 56,795,202,000/76.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya hasara hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Sehemu kubwa ya hasara zinazohusu potevu za fedha, vifaa na malipo batili ya shilingi 1,554,298,253/30 kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2000 hadi Juni, 2003 na chache za kipindi kinachoishia Juni, 2004. Hasara hizo zimetokana na sababu mbalimbali, kama vile wizi wa makusanyo ya mapato, wizi wa mishahara ya watumishi, hasa Walimu na aina nyingine za wizi. Hali hii sasa imepungua baada ya Serikali kuamua kupitishia mishahara ya watumishi Benki katika akaunti za watumishi na kufuatia teknolojia mpya inayotumika katika ukusanyaji wa kodi.

Aidha, upotevu unasababishwa pia na wizi wa mali, vifaa na uzembe, ambapo vifaa huachwa bila ya kuangaliwa na hivyo huharibika au kupitwa na wakati. Kwa vifaa vilivyoko katika bohari na malipo batili yaliyofanyika bila Serikali kunufaika na huduma yote, yaani *(Negative Expenditure);* na

(ii) Hasara nyingine zinazoombewa kufutwa ni shilingi 52,775,465,687/41 zinazotokana na mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa. Mapato yaliyoshindikana kukusanywa yametokana na sababu mbalimbali zikiwemo badiliko la Sheria za Kodi, Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, kufilisika kwa walipa kodi au madeni ya mikopo yaliyoambatana na Mikataba yenye dhamana ndogo au kutokuwa na dhamana kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa hasara za mikopo iliyoambatana na Mikataba yenye dhamana ndogo ni mikopo iliyotolewa na Mfuko wa Mikopo ya Pembejeo. Wadaiwa wengi katika Mfuko huu walikuwa watu binafsi na Vyama vya Ushirika, ambavyo vilikuwa na dhamana ndogo kuliko kima cha mkopo waliopewa na wengine walikuwa hawana kabisa. Hii ina maana kwamba, Mfuko huu ulikuwa unatoa mikopo isiyokuwa na dhamana thabiti *(Weak Collateral Security),* kwa kuwa wengi wao walikuwa hawana mali na wale ambao walifariki kabla ya kumaliza deni, hawakuwa na mali zozote walizoacha, ambao zingeweza kuuzwa ili kufidia madeni hayo.

Mfano mwingine ni wa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Katika kipindi cha mwaka 1996/97 na mwaka 1998/99, Mamlaka ilikuwa inabadilisha mifumo yake mingi iliyorithi kutoka Serikalini na kuanza kuitegemea kama Mamlaka. Watumishi wengi waliokuwa wanafanya kazi kabla ya Mamlaka kuanzishwa, walipunguzwa kazi na kusababisha ufuatiliaji wa madeni kuwa mgumu hasa kutokana na kutokuwepo kwa kumbukumbu za kutosha za walipa kodi. Aidha, ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, umechangia Serikali kushindwa kukusanya mapato. Wawekezaji wanaonunua Mashirika yaliyobinafsishwa, hawataki kurithi madeni ya Mashirika waliyoyanunua hivyo, Serikali hulazimika kufuta madeni yake kutoka kwa Mashirika hayo.

Tatu, ni hasara zinazotokana na usawazishaji wa kumbukumbu katika vitabu zinazofikia shilingi 2,465,438,060/05. Hasara hizi zinatokana na tatizo la kutofuata taratibu kikamilifu na kukosekana kwa nyaraka za madai kati ya Idara na Idara za Serikali. Aidha, wakati mwingine mtumishi huweza kufariki dunia bila ya kurejesha masurufu aliyokuwa anadaiwa wakati wa uhai wake na Serikali kubaini kwamba, mafao ya mtumishi huyo hayatoshelezi katika kulipia masurufu aliyokuwa anadaiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali inaweka juhudi katika kusimamia kikamilifu, Sheria ya Fedha ya Umma ya mwaka 2001, kwa lengo la kupunguza na hatimaye kuepuka hasara za namna hii. Mapema Juni, 2005, Waziri wa Fedha alitoa kanuni za adhabu za tozo kwa Maafisa Wahasibu katika kuhakikisha kwamba, fedha na vifaa vya Serikali vinatunzwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaomba kufuta hasara na kusamehe madai ambayo hayalipiki ya kiasi cha shilingi 56,795,202,000/76 kama ilivyoanishwa katika jedwali ambalo limeambatanishwa pamoja na Azimio hili, ambalo limetolewa kwa Waheshimiwa Wabunge ili kutoa picha halisi. Kufutwa kwa sera hizi, kumekuwa kukipunguza kwa kiasi kikubwa, hoja za ukaguzi mwaka hadi mwaka na papo hapo kumekuwa kukileta na kutaendelea kuleta picha hiyo sahihi ya mahesabu ya Serikali na Taifa kwa ujumla. Sio tu mbele ya Wananchi, bali hata mbele ya wadau wa maendeleo walioko ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Bunge la Kufuta na Kusamehe Madai na Hasara Itokanayo na Upotevu wa Fedha na Vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2005 kama ifuatavyo:-

KWA KUWA, kwa mujibu wa kifungu cha tano cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma ya mwaka 2001, Waziri wa Fedha anayo Mamlaka ya kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma, ikiwa ni pamoja na kugawa na kuidhinisha matumizi ya fedha hizo baada ya kupata idhini ya Bunge;

NA KWA KUWA, kwa mujibu wa kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma ya Mwaka 2001, Bunge linaweza kwa Azimio, kutoa idhini kwa Waziri wa Fedha, kufuta hasara na upotevu wa fedha, vifaa vya Serikali, madai ya kodi, pamoja na riba itokanayo na malimbikizo ya kodi;

NA KWA KUWA, Vitabu vya Hesabu za Serikali vimeonesha kuwepo na upotevu wa fedha za Serikali, pamoja na maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa;

NA KWA KUWA, kutokana na upotevu na upungufu huo wa fedha, vifaa na maduhuli ya Serikali, upo umuhimu wa kusawazisha kumbukumbu katika vitabu hivyo vya Serikali;

KWA HIYO BASI, kwa mujibu wa kifungu cha 43(1) cha Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Fedha za Umma ya mwaka 2001, sasa Bunge hili, katika Mkutano wake wa Ishirini, linaazimia kumuidhinisha Waziri wa Fedha, asamehe na kufuta upotevu wa fedha, vifaa na malipo batili, maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa na kwa ajili hiyo kusawazisha kumbukumbu katika vitabu vya Serikali kama ifuatavyo: Upotevu wa fedha, vifaa na malipo batili shilingi 1,554,298,253/30; Mapato au maduhuli yaliyoshindikana kukusanywa ya shilingi 52,775,465,687/41; na usawazishaji wa kumbukumbu katika vitabu vyenye thamani ya shilingi 2,465,438,060/05. Jumla Kuu ni shilingi 56,795,202,000/76.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu potevu hizi, yapo kwenye kabrasha ambalo naamini, Waheshimiwa Wabunge, wamepata nakala yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

**Azimio Kuhusu Kuongeza Mtaji na Mfumo wa Mikopo**
***(Advances Fund)***

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, likubali kupitisha Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha kuongeza mtaji wa Mfuko, ujulikanao kama *Advances Fund* kutoka shilingi 10,000,000,000 hadi 18,000,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko huu wa *Advances Fund,* ulianzishwa kama *Revolving Fund,* chini ya iliyokuwa Sheria ya *Exchequer and Ordinance* ya mwaka 1961, kwa madhumuni ya kuwakopesha Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Serikali, vyombo vya usafiri, pamoja na vyombo vya nyumbani ili kuleta ufanisi katika utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, watakumbuka kwamba, kwa mara ya mwisho, mtaji wa Mfuko huu uliongezwa kwa Azimio la Bunge hadi kufikia shilingi 10,000,000,000 mnamo mwaka 2001. Serikali inatambua kwamba, kupanda kwa bei ya vyombo vya usafiri, pamoja na vyombo vya nyumbani na pia ongezeko la idadi ya Waheshimiwa Wabunge, kama inavyotarajiwa katika Bunge la Awamu ya Nne hivyo, mtaji wa sasa wa shilingi 10,000,000,000 hautoshi kukidhi mahitaji ya Mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba sasa kuwasilisha Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

KWA KUWA, Serikali inazingatia umuhimu wa kuleta mazingira bora ya kazi kwa Waheshimiwa Wabunge, pamoja na watumishi wake, ili kuongeza ufanisi na tija;

NA KWA KUWA, Serikali inatambua umuhimu wa kuwapatia Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Watumishi wa Serikali, vyombo vya usafiri na pia vyombo vya nyumbani;

NA KWA KUWA, umekuwepo Mfuko uitwao *Advances Fund,* ambao mtaji wake wa kiasi cha shilingi 10,000,000,000 uliongezwa mara ya mwisho mwaka 2001 kwa kupitia Azimio la Bunge;

NA KWA KUWA, Serikali inatambua kwamba, bei za vitu mbalimbali vikiwemo vyombo vya nyumbani na vyombo vya usafiri, vimepanda na pia kwa kuzingatia ongezeko la idadi ya Waheshimiwa Wabunge katika Bunge la Awamu ya Nne na hivyo kuongezeka kwa matumizi ya Mfuko na hivyo kufanya mtaji huu usitoshe kukidhi madhumuni ya kuanzisha Mfuko huo;

KWA HIYO BASI, kwa madhumuni haya maalum, Bunge hili katika Mkutano wake wa 20, linaazimia kwamba:-

(i) Mataji wa *Advances Fund* uongezwe kutoka shilingi 10,000,000,000 hadi kufikia shilingi 18,000,000,000 ambao unaweza kurekebishwa na Waziri wa Fedha mwaka hadi mwaka kulingana na bei ya bidhaa hizo katika soko;

(ii) Baadhi ya mtaji wa *Advances Fund* kuongezwa na kufikia kiwango hicho, inaazimiwa kuwa matumizi yake yawe kama ifuatavyo:-

(a) Kukopesha Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Serikali fedha za kununua vyombo vya usafiri; na

(b) Kukopesha watumishi wa Serikali fedha za kununulia vifaa vya nyumbani kama vile friji, majiko, samani, redio, baiskeli, miwani, feni na cherehani;

(iii) Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi 16,000,000,000 zitumike kwa ajili ya mikopo ya vyombo vya usafiri;

(iv) Fedha zitokanazo na mauzo ya vyombo vya usafiri na vifaa chakavu ziingizwe kwenye Mfuko huu ili kutunisha mtaji wake; na

(v) Marejesho ya vyombo vya usafiri yanayofanywa na Waheshimiwa Wabunge, yahifadhiwe kwenye Akaunti Maalum *(Interest Bearing Account),* kwenye Benki ya Biashara ili kuwezesha kupata faida. Faida itakayopatikana, itasaidia kupunguza pengo la kiasi ambacho hakitarejeshwa na Waheshimiwa Wabunge, kutokana na msamaha uliotolewa na Serikali wa asilimia 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mwenyekiti au mwakilishi wa hiyo Kamati iliyopitia Maazimio haya, ningependa kutoa taarifa mbili muhimu. Moja, hatuna muda wa kutosha, saa saba ndiyo tunatakiwa tukamilishe. Lakini tunayo mbele yetu Maazimio mengine ya Wizara ya Mambo ya Ndani manne. Hapa kwenye *Order Paper,* mtaona yameandikwa matatu, lakini kuna moja ambalo halikuingizwa hapa kwa bahati mbaya, lakini mawasiliano yote kati ya ofisi zinazopaswa kuingiza walishayafanya. Kwa hiyo, nitamruhusu Waziri wa Mambo ya Ndani na hilo pia alisome. Sasa kama yote yakisomwa, muda utakuwa mrefu sana kiasi kwamba, nawasihi sana Waheshimiwa Wabunge, kutokupata nafasi ya kuchangia, changia *as briefly as possible* ili tuweze kukamilisha tuseme kabla ya saa saba, ikifika saa saba tuwe tumekamilisha yote.

Baada ya maelezo hayo, ninao wachangiaji watatu ambao ni Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa na Mheshimiwa Raphael Chegeni, ikibidi hata dakika tano tano nadhani zinatosha kujenga hoja.

**MHE. PROF. DAVID MWAKYUSA (K. n. y. MWENYEKITI KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe shukurani kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali juu ya Azimio la Kufuta Upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na.43 (V)(b) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Maoni ya Kamati ya Hesabu za Serikali kuhusu Azimio la Kufuta Upotevu wa Fedha na Vifaa vya Serikali kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001 kupitishwa na Bunge, Mamlaka ya kufuta hasara hizi alipewa Waziri wa Fedha. Lakini baada ya Sheria hiyo, Bunge ndilo lenye jukumu ya kufanya kazi hiyo. Sheria inaelekeza kuwa taarifa ya hasara na potevu itaandaliwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali ambaye atawakilisha mbele ya Kamati ya Hesabu za Serikali. Kamati itachunguza na hatimaye kuitolea mapendekezo ya kufuta au hatua nyingine zinazofaa kuchukuliwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na matakwa ya Sheria yaliyoainishwa hapo juu, Kamati yangu ilikutana tarehe 20 Julai, 2005 ili kufanya kazi hiyo. Taarifa inayowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu ni matokeo ya juhudi za Kamati ikisaidiwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wote walioshirikiana na Kamati katika kukamilisha zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu wa Spika, kama Naibu Waziri wa Fedha alivyosema hivi punde, hasara na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali, Serikali ilileta mbele ya Kamati maombi ya kufuta hasara na potevu yenye jumla ya Sh.58,456,633,951.94. Baada ya Kamati kufanya uchambuzi, Kamati iliridhika na hasara ya upotevu wa Sh.56,795,202,000.76 kwa mchanganuo, kama alivyosema Naibu Waziri. Potevu zilizorejeshwa ili ziendelee kushughulikiwa zina thamani ya Sh. 1,661,431,951.18.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa kutoa maelezo ya mchanganuo katika potevu za fedha ambazo ni Sh.1,554,000,000/=. Ameeleza sababu ambazo ndiyo na sisi tuliziona kwa pamoja, lakini nilitaka nitoe maelezo ya ziada katika maeneo mawili matatu. Moja, ni fungu 43 - Wizara ya Kilimo ambapo potevu zilifikia kiasi cha Sh. 212,464,552.25 na hasara hiyo ilitokana na usimamizi duni wa Mfuko wa Pembejeo. Sababu kubwa ni kwamba Mfuko huu ulikuwa unatoa mikopo bila nguzo ya dhamana thabiti, yaani *weak collateral assurance*. Wadaiwa wengi katika Mfuko huu walikuwa watu binafsi au Vyama vya Ushirika ambavyo dhamana yao ilikuwa ndogo kuliko mikopo waliyopewa na baadhi walikuwa hawana dhamana kabisa.

Hata hivyo, tunaipongeza Wizara kwa juhudi inazofanya katika kufuatilia madeni na kuna ushahidi kwamba hizi juhudi zinazaa matunda, baadhi yao wamefikishwa Mahakamani. Vile vile, kwa upande wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, katika Wizara hii kulikuwa na upotevu wa Sh.50,180,148.80. Kiasi kikubwa kilitokana na upotevu wa vitabu mashuleni. Kamati imependekeza kwamba mikakati madhubuti iandaliwe ili kudhibiti wizi wa vitabu hivyo. Wizara nyingine ni Wizara ya Mambo ya Ndani hususani Jeshi la Polisi ambapo kulitokea hasara ya Sh. 15,158,164.85. Kamati imebaini kuwa Maofisa wengi wa Polisi wanaotuhumiwa kuiba hawakamatwi na sababu zinazotolewa ni kuwa wametoroka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilishangaa kwamba wananchi wengine wanapotuhumiwa wanakamatwa lakini Polisi hawakamatwi kwa sababu wametoroka. Hii inaleta hisia za kulindana. Kamati inapendekeza kwa mara nyingine, hili pendekezo tulilitoa mwaka jana 2004 kuwa kunapotokea wizi mkubwa ndani ya Jeshi ya Polisi

chombo kingine kama vile Taasisi ya kuzuia Rushwa kichunguze tuhuma hiyo na siyo Polisi kuchunguza Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ilikuwa maduhuli ambayo yalishindikana kukusanywa ambayo ni Sh. 52,775,465,687.41. Sababu zimetolewa na Kamati inaafiki. Tuseme tu kwamba, kufuatia utekekelezaji wa sera ya ubinafsishaji imekuwa vigumu kwa Serikali kuendelea kuyadai Mashirika ya Umma ambayo yamebinafsishwa, kwani mmliki wa Mashirika hayo ni Serikali yenyewe. Hii ina maana Serikali ijilipe yenyewe.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni hasara zinazohusu urekebishaji wa kumbukumbu Sh.2,465,438,060.05. Kamati ilibaini kwamba hasara hizi zinatokana na ama kukiuka taratibu za kiuhasibu na ununuzi au kukosekana kwa nyaraka husika ingawa kazi imefanyika au huduma zimetolewa. Aidha, ilibainika kuwa baadhi ya nyaraka zinapotea zikisafirishwa kwenda au kutoka Mikoani. Kamati inapendekeza kwamba kiwekwe chombo maalum cha kusafirisha nyaraka hizi za Serikali, yaani *carrier service* ambayo inaaminika. Vile vile tunaamini kwamba Maafisa Wahasibu wakizingatia maelekezo ya Sheria za Fedha na Sheria ya Ununuzi zote tulizopitisha hapa mwaka 2001 matatizo haya yatapungua kwa kiasi kikubwa kama sio kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona tukiangalia hizi potevu Kamati inaridhika kwamba kumekuwa na uboreshaji wa mahesabu kwa jumla na utaona fungu kubwa ni maduhuli ambayo yameshindikana kukusanywa, ambayo katika Shilingi bilioni 56 ni asilimia 92.9 ni maduhuli ambayo yameshindikana kukusanywa. Kwa hiyo, tungependa kuipongeza Wizara chini ya Jemedari wao Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa utekelezaji mzuri, kwa sababu tumekuwa tukifuatilia mwaka hadi mwaka na uboreshaji unaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaliomba Bunge lako Tukufiu likubaliane na maoni na mapendekezo ya Kamati yangu ili likubali Azimio hili litakalomwezesha Waziri wa Fedha kufuta au kusamehe madeni na hasara itokanayo na upotevu wa fedha na vifaa vya Serikali na pesa zinazoombwa kufutwa ni Sh.56,795,202,000.76.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba nitoe shukrani kwa Spika, kwako mwenyewe na kwa Katibu wa Bunge na Makatibu wa Kamati yetu Bwana Anselem Mrema na Maulid Kheri kwa kuihudumia Kamati yetu na hivyo kuiwezesha kufanya kazi yake kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Bibi Blandina Nyoni - Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa utendaji wake mzuri na vile vile kwa jinsi alivyowasilisha mbele ya Kamati maelezo ya kina kuhusu madhumuni ya Azimio.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho na siyo mwisho kwa umuhimu, naomba kumpongeza tena Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa kuongoza timu ya ushindi

ambayo inajumuisha Manaibu Mawaziri wake, Makatibu Wakuu na Watendaji wote katika Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na kuliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe pendekezo la Azimio la Waziri wa Fedha na kwa niaba ya Kamati, naunga mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kwa hiyo na lile Azimio lingine nani anasoma? Sio lenu. Nani ambaye amepitia hilo azimio lingine? Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kama anayo.

**MHE. ADELASTELA MKILINDI (K.n.y. MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha, Mipango na Ubinafsishaji, naomba kutoa maoni ya upinzani kuhusu Azimio la Kumwezesha Waziri Kufuta au Kusamehe Madeni au Hasara itokanayo na Upotevu wa Fedha au Vifaa vya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kuwa, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani tunaunga mkono hoja au Azimio hili ili tuweze kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba Wapinzani tunapokuwa ndani ya Bunge hatupingi kila kitu, kwa sababu tu eti Upinzani na wala hatuungi mkono hoja ili kufurahisha Chama Tawala, ila tupo kwa ajili ya kulinda na kutetea maslahi ya nchi hii na wananchi kwa ujumla, na nikinyume kabisa na alivyosema Mheshimiwa Waziri waMaji na Maendeleo ya Mifugo asubuhi ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pamoja na kuridhia Azimio hili linaelezea wasiwasi wake na inatoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani haiamini kabisa uzembe kama ule wa kuibiwa nyaraka kwenye Kituo cha Basi - Ubungo iwe ni sababu tosha kukosekana kumbukumbu hizo na hivyo kusababisha hasara na upotevu wa fedha. Kambi ya Upinzani inataka Serikali iweke utaratibu wa aina moja wa kusafirisha au kuhamisha nyaraka za Serikali ili uzembe kama huo usirudiwe, lakini pia wahusika wachukuliwe hatua kali sana za kisheria.

Pili, ni kwamba sehemu moja tunaotakiwa kufuta ni fungu 28 la Jeshi la Polisi ambapo wizi umetokea katika Ofisi za Jeshi lenyewe, hivyo sisi hatuamini kuwa walioiba hawawezi kupatikana, ila kuna kulindana. Hivyo basi, ni lazima wahusika wawajibishwe pamoja na kwamba hasara au upotevu huo utafutwa.

Tatu, kwamba upo udanganyifu wa wanaotakiwa kufanya kazi hiyo kutokana na kipato wanachokipata kutokidhi mahitaji yao ya kila siku. Hivyo basi, inawabidi kujiingiza katika vitendo vinavyopelekea Taifa kupoteza mapato yake. Kambi ya Upinzani inashauri viwango vya mishahara ya watumishi vipandishwe. Kwamba kuna uzembe wa wanaokusanya mapato ya Serikali wa wanaokusanya mapato ya Serikali kutoyaingiza katika vitabu na kuyawasilisha Benki kwa wakati unaotakiwa, hivyo kutoa

mwanya kwa washika fedha kujikopesha na hatimaye kutoroka. Kambi ya Upinzani inashauri utaratibu wa ukaguzi wa kushitukiza uimarishwe ili kuweza kugundua wizi mapema

Tano, ni kwamba, kwa kudhibiti hali hii, Hazina iweke kitengo maalum cha kufuatilia upotevu wowote wa vifaa na fedha hata kama zimeshafutwa vitabuni na mtumishi atakayegundulika kusababisha upotevu, hasara ya fedha au mali hiyo, madhambi yake yamfuate popote atakapohamishiwa na sio kubebeshwa mzigo mtumishi aliyekabidhiwa madaraka badala yake. Kwa maana hiyo, kila mtu atabeba msalaba wake mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunaamini kabisa kuwa Wahusika wa hasara hiyo baadhi yao wanajulikana walipo na kuna uwezekano mkubwa wa kuwa kilichofanyika ni kuhamishwa Idara na kupelekwa Idara nyingine, hivyo basi pamoja na kuridhia Azimio la uamuzi wa kufuta hasara hiyo, hatua zichukuliwe kwa wahusika kwa kuchangia hasara hiyo kupitia *personal properties* zao. Hatua hii itaimarisha nidhamu kupunguza wizi na upotevu wa mali ya umma

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pamoja na kwamba inaunga mkono hoja hii ambapo upotevu wa fedha za Serikali umesababisha wananchi kukosa huduma muhimu, inamtaka Waziri akafanye *homework* yake vizuri ya kudhibiti matumizi na makusanyo ya Serikali kama ilivyoainishwa katika Sheria za Fedha na Manunuzi, yaani *Finance and Procurement Act.*

Baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na kwa niaba ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, naomba kuwasilisha na kuunga mkono hoja.

Pia, kwa niaba ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed -Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha, Mipango na Ubinafsishaji kufuatia Azimio lililowasilishwa na Waziri wa Fedha, naomba kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya hoja ya Waziri wa Fedha ya kutaka Bunge lako Tukufu likubaliane na Azimio la kuongeza Mtaji wa Mfuko wa Mikopo yaani *Advances Fund.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nalo tunaliunga mkono mapema kabisa. Kutokana na kipato kidogo wanachopata Wabunge na Watumishi wa Serikali kulinganisha na Wabunge na Watumishi wa nchi jirani na kutokana na ughali wa uchumi wetu, Kambi ya Upinzani inakubaliana na Azimio hili la kuwa na *Advance Fund.* Hivyo, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa mtaji wa *Advance Fund* uongezwe kutoka Shilingi bilioni 10 hadi bilioni 18 na kurekebishwa na Waziri kadiri atakavyoona inafaa mwaka hadi mwaka. Fedha hizo zitumike kama alivyopendekeza Waziri katika Azimio hilo kwamba fedha hizo ziingizwe kwenye biashara itakayoweza kutunisha Mfuko ili uweze kujitegemea bila kuomba fedha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Matumizi ya Mfuko huo yawe wazi na kuweza kufuatiliwa na kukaguliwa kila inapohitajika kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuleta uwiano wa shughuli za Bunge katika Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba Waziri afanye utafiti wa viwango vinavyolipwa katika Mabunge haya, utaratibu unaotumika wa bajeti

ya Bunge ili tuweze kuwa na mfumo wa aina moja katika nchi za Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na kwa niaba ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niseme machache kuhusu hoja hizi mbili ambazo ziko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hizi zote mbili. Pili, naungana na Mheshimiwa Waziri kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Bernard Kabeluka Waziri wa Fedha wa Rwanda ambaye sasa amekuwa Rais Mpya wa *African Development Bank*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Bernard Kabeluka mimi tulifahamiana nilipokuwa Abidjan, alikuja kule wakati akiwa katika Shirika la Kahawa la *Inter-African Coffee Organization*. Ni mchapa kazi. Kwa hiyo, nasema kuwa sisi tumepata jirani ambaye anaweza akatusaidia pia huku kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa taarifa kuwa pia Benki ya Maendeleo ya Afrika-*ADB*, Makao Makuu ya muda huko Tunisia, sasa hivi iko mbioni katika kutafuta mahali pa kujenga Makao Makuu yake ya kudumu. Sasa mimi wakati fulani katika Semina hapa nilikuwa nimeomba Serikali ikajaribu kushauriana na Benki ya Afrika labda kuikaribisha hii Benki ijenge Makao Makuu huko Arusha. Kwa kuwa sasa tumepata jirani yetu Mheshimiwa Kabeluka ambaye amekuwa Rais, itakuwa vizuri sana kama Mheshimiwa Waziri atajaribu kuwasiliana kuona kama tunaweza kupata bahati ya kuikaribisha Benki ya Afrika. Majengo yapo. Hata hivyo, Benki yenyewe iko tayari kujenga kwa sababu tumepata taarifa kuwa haitarudi tena *Abidjan, Ivory Coast* kwa sababu ya matatizo yaliyojitokeza. Kwa hiyo, sasa ningeomba hilo suala lishughulikiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hoja zilizopo mbele yetu hapa, mimi naona upotevu unapotokea wa fedha za Serikali maana yake inadhoofisha uwezo wa Serikali katika kuhudumia Taifa hili. Kwa hiyo, uwezo unapodhoofishwa, Sekta nyingi zinaumia. Mimi ningeomba, naunga mkono hoja hii, lakini ningeomba pia uzembe unapotokea Serikali iwe makini zaidi kudhibiti uzembe, wizi na usimamizi hafifu wa matumizi ya fedha za Serikali na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Leo hii tunazungumzia kwa mfano watu muhimu sana katika Taifa hili ni Watendaji wa Vijiji. Wengi hawakuweza kulipwa kwa sababu fedha zilinyauka, zilipotea na kuna Madiwani wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Sasa kama suala la upotevu wa fedha utapungua na utadhibitiwa, nina uhakika Watendaji wa Vijiji na Madiwani nao watalipwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala pia la wastaafu wa zamani. Mimi hapa kwa rukhsa yako, naomba kunukuu barua ambayo nimepata kutoka Wilaya ya Ilamba, iliyoandikwa kwa Mheshimiwa Rais, nakala kwa Mheshimiwa Spika. Inasema, Nanukuu: "Shukrani na pongezi kwako kwa kuwakumbuka wastaafu. Mheshimiwa Rais sisi Wazee

wastaafu wa Kinampanda, Wilaya ya Iramba, tumeona ni vyema tuchukue fursa hii kukuandikia wewe binafsi, kukupa pongezi na shukrani zetu za dhati kwa hatua ya pensheni ambayo umeturudishia."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli sasa nina uhakika uwezo wa Serikali wa kuwalipa hawa wastaafu ambao wamerudishwa katika daftari la malipo, uwezo wake utaongezeka kama uzembe na wizi na matumizi mabaya ya fedha za Serikali utadhibitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ningemalizia tu kwa kusema kuwa, ningeomba kwa kweli wale ambao wanahusika na upotevu wa fedha, isiwe tu wanategemea kuwa Bunge hili litaletewa na kufuta, lakini wafuatiliwe kabisa hata ikiwa baada ya kufuta, Serikali iwafuatilie na ikiwezekana iwawajibishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningemalizia hapa kwa kusema tu kuwa naunga mkono tena hoja hii na naomba tu Serikali iwe makini, upotevu huu usitokee ambao kwa uwezo wake unaweza ukadhibitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nikupongeze kwa kunipa nafasi hii ambayo huenda nikawa wa mwisho kuchangia na kufunga Mkutano huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakwenda moja kwa moja kwenye ombi la Mheshimiwa Waziri kuhusu kufuta. Wanasema penye tatizo, tatua. Tumekubali tutatue, tunakubali kufuta kwa sababu tusipofuta tutapata kazi ya kutafuta. Sasa unapotafuta kitu ambacho hakipo utatumia gharama kubwa kwenda kufuatilia, kufanya nini. Lakini vyema ukamwambia huyo mtu kaa pembeni, tuanze upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaanzaje upya? Ni kwamba tunawataarifu kwamba ufutaji huu ndiyo wa mwisho, kwamba hatufuti tena. Kwa hiyo, kama kuna mtu alitegemea kwamba sasa ndiyo mwanzo, wanasema, "Ukiona mwenzako ananyolewa unajiandaa kunyolewa," kwamba sasa kama wamefuta hao, tuingize lingine tena watafuta. Sasa tunaomba tu tuwataarifu Watendaji wetu kwamba wawe makini, wasituletee kazi tena ya kufuta, kazi yetu ni kutengeneza mitaji kwa ajili ya watu na ambao ni wananchi wetu. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwe tukubali ufute.

Halafu lingine ni kuhusu mitaji. Kuhusu Mfuko wa Mikopo, ninaukubali kabisa na ningedhani kwamba kuna haja ya kuongeza. Mimi kwangu wananchi wana shida mno ya mitaji na ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba tuna watu wenye vichwa vizuri kabisa katika lile Jimbo, kuanzia biashara, miradi lakini tatizo limekuwa ni mitaji. Sasa ninakubaliana moja kwa moja na hoja hii kwamba kwa asilimia 99.9 ninaiunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile umesema tuwe *brief*, ninaomba nikaribie mwisho kwa kusema kwamba ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu, pia

ninawashukuru Mawaziri kwa utendaji wao mzuri. Moja ni juzi Mheshimiwa Waziri ameonyesha kwamba kwa kweli hata tungempa nchi hii alipokuwa anagombea angefanya mambo ya maana pia, Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli baada ya juzi kuwa nimelalamika hapa ndani kwamba wananchi maeneo yetu yanagawiwa bila wao. Aliniandikia memo akasema, njoo tuongee, mimi sikujua kama kuna mambo yanatendeka huko. Sasa unasemaje?" Nikamwelezea akasema hili tutatatua. Kwa hiyo, nikahisi kwamba Serikali inayosikiliza ndiyo tunaitaka. *(Makofi)*

Sasa kama mnasikiliza, tunaomba mwendelee kusikiliza na japo mnaamini kwamba mtachukua nchi, hatujajua na kama sitakuwa Mbunge, basi naomba mwamko huo mlioufanya uendelee ili iwe kazi ndogo kuwabana. Kama hamtachukua na mimi kama nitarudi, basi tutaendeleza kazi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwanza ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri, tumeshirikiana vya kutosha, kwa raha na shida tumekuwa pamoja. Ninaomba niwapongeze. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mimi naamini mtarudi. Kwa nini nataka mrudi? Ni kwa sababu unapokuwa Mbunge, tayari una uzoefu. Unapokuwa na uzoefu kila kunapokucha unajifunza. Ukitatizwa njiani unakuwa na mengi ya kuifanyia nchi yako. Sasa ninaamini kwamba mtarudi na Mungu anakuwa karibu na anayetaka kurudi, anamwongezea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupongeze, nikutakie maisha mema, kwa kweli umetuongoza vizuri mno. Ninadhani kama utakuwepo, basi ninakutakia maisha mema, uongoze Bunge letu hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ahsanteni Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Napenda tu kusema kwamba suala la kufuta madeni limekuja muda muafaka kwa sababu ukizingatia tumetoka mbali. Lakini huu ni muda muafaka, maana yake ni kwamba Wizara husika imeweza kuchukua kwa makusudi maamuzi sahihi kwamba tunapaswa tufute madeni ambayo hayawezi tena kukusanyika wala hatuwezi tena kui-*cover* hii *lose*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hoja yangu ni kwamba, tumekuwa na *lose*. Ukiangalia, ni pesa nyingi sana! Sasa kwa Bajeti ya Mikoa peke yake, kwa mwaka huu wa Fedha ni Shilingi bilioni 51.5 na tunafuta *lose* pamoja na madeni na pesa ambazo haziwezi kukusanyika zaidi ya Shilingi bilioni 56.7. Sasa ningependa tu kusema kwamba tuangalie, haya makosa yametendeka hatuwezi kurudi nyuma, ila tunaomba sasa Waziri anayehusika, kunapotokea matatizo kama haya, waliosababisha lazima wachukuliwe hatua sahihi ili kuzuia kusitokee sababu ya kuendelea kuipatia nchi hasara ambazo hazina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuiomba sana Wizara husika kwamba hiki kiwango cha tozo kwa Maofisa Wahasibu ni kidogo sana. Ni vyema kiangaliwe na ile hasara aliyoisababisha, kama ammetenda kosa kubwa, basi ikiwezekana achukuliwe hatua kali zaidi. Tukifanya hivi, huu uzembe uzembe utakuwa umepungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuhusu suala la ufutaji, tungependa mfumo mzima uwe wazi na Bunge ikiwezekana basi lipewe taarifa mapema kabla Waziri hajafuta ili kama kuna namna yoyote ya kuweza kutafuta namna ya kudhibiti, basi kuwe na *checks and balances*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nazungumza kwa maslahi ya Taifa kwa sababu Bunge ndiyo chombo ambacho wananchi wamekipa dhamana na kama kimepewa dhamana hiyo, basi ni vyema Mheshimiwa Waziri anayehusika aweze kuhakikisha kwamba Bunge linapewa taarifa mapema zaidi. Lakini taarifa za kufuta inabidi ziambatane na hatua zinazochukuliwa juu ya watu ambao wamesababisha upotevu huu, ikiwezekana kwa majina na makosa waliyoyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kwamba Wizara hii iendelee kuhimili zaidi katika kukusanya mapatao na kudhibiti mapato na ni *credit* ambayo tumeipata kwa Watazania na mpaka sasa hivi nchi yetu imeweza kupanda chati kwa sababu ya nidhamu kubwa sana ya kukusanya na kutumia pesa. Ningependa nidhamu hii iweze kuboreshwa na kuendelezwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kutoa sahihisho moja. Nimesema potevu hizi ni kwa kipindi kinachoishia Juni 2005, lakini ni kipindi kilichoishia Juni, 2004. Kwa hiyo, naomba kusahihisha hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tunakubali mapendekezo na ushauri wote uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa kwa mujibu wa Kamati, Mheshimiwa Adelastela Mkilindi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Leonard Shango, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa na Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni. Haya yote mliyotushauri tutayafanyia kazi kama Serikali na kama tulivyofanya huko mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema wakati natoa Azimio hili, katika utangulizi wangu nilisema kwamba hatua zinachukuliwa kwa wale wote ambao wamekosea na kama alivyosema Profesa Mwakyusa, ametaja kwa mfano upande wa Polisi na wengine ambao hawakuchukuliwa hatua. Lakini tumeyapokea yote na tutayafanyia kazi kuhakikisha kwamba kila siku zinapokwenda upotevu unazidi kupungua zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *ADB*, napenda kumwambia Mheshimiwa Shango kwamba *ADB* waliwahi kuja hapo siku za nyuma wakati wanatafuta *temporally* makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hivyo, Bikabiruka kama tulivyosema ni jirani yetu na mimi nilikuweko huko katika uchaguzi huo *all the time,* siku zote ambazo nilikuwa sipo hapa, tutahakikisha kwamba tutarejea maombi yetu kwamba Tanzania iwe Makao Makuu ya *ADB* hapo wakati utakapofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Azimio la Kumwezesha Waziri wa Fedha Kufuta au Kusamehe Madai au Hasara Itokanayo na Upotevu wa Fedha au Vifaa vya Serikali liliridhiwa na Bunge)*

*(Azimio la Kuruhusu Kuongeza Mtaji wa Mfuko wa Mikopo (Advance Fund) liliridhiwa na Bunge)*

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa *(The United Nations Convention against Transnational Organized Crime)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, nitafupisha maelezo yangu ya kuwasilisha na nitajikita zaidi kwenye kusoma Maazimio. Naomba niwasilishe kwanza Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa *(The United Nations Convention against Transnational Organized Crime).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba huu unatokana na Mkutano wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa uliofanyika Palermo, Italy tarehe 12 - 15 Desemba, 2000 na katika Mkutano ule lilipitishwa Azimio la kuharamisha vikundi vilivyoundwa kwa lengo la kutenda uhalifu, fedha haramu, rushwa na kuvuruga taratibu za kisheria za utoaji wa haki na kuweka taratibu za kupambana na yote hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tukufu liridhie Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa *(The United Nations Convention Against Transnational Organized Crime)* na naomba Azimio hilo nilisome.

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja kati ya nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa;

NA KWA KUWA lengo kuu la Mkataba huu ni kupambana na uhalifu wa Kimataifa;

NA KWA KUWA nchi zote ambazo zimekubali kutia saini Mkataba huu zitakuwa tayari kushirikiana na nchi yetu katika ubadilishanaji wa taarifa za uhalifu;

NA KWA KUWA nchi yetu itafaidika kwa kupata mafunzo na mbinu za kisasa katika kupambana na uhalifu wa Kimataifa;

NA KWA KUWA tutaimarika kwa ushirikiano wa Kimataifa katika upelelezi na uendeshaji wa mashtaka ya kesi za uhalifu wa Kimataifa;

NA KWA KUWA amani na usalama wa nchi yetu utaimarika na hivyo kuvutia watalii na wawekezaji;

NA KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado haijaridhia Mkataba huu;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Mkataba huu na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake wa 20 sasa linaazimia kuridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa Dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa *(The United Nations Convention Against Transnational Organized Crime).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Azimio la Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa liliridhiwa na Bunge)*

### Azimio la Kuridhia Itifaki ya Umoja wa Mataifa dhidi ya Uvushaji Haramu wa Wahamiaji kwa Njia ya Nchi Kavu, Maji na Anga *(The United Nations Protocol against the Smuggling of Migrants by Land, Sea and Air)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Azimio la pili ni kuridhia Itifaki dhidi ya Uvushaji Haramu wa Wahamiaji kwa Njia za Nchi Kavu, Maji na Anga *(Protocol against the Smuggling of Migrants by Land, Sea and Air.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii inatokana na Mkataba ule ambao nimekwishasoma Azimio lake dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa. Katika Mkutano wa Palermo ulipitishwa Mkataba ule na Mkataba ule ulikuwa na Itifaki nyingi. Miongoni mwa Itifaki zile ni hii ambayo ninaiwasilisha hivi sasa na ambayo ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuiridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza muda naomba nisome Azimio ambalo ninalipendekeza kwa Bunge.

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja kati ya nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa;

NA KWA KUWA lengo kuu la Itifaki hii ni kudhibiti uvushaji haramu wa wahamiaji kwa njia za nchi kavu, maji na anga;

NA KWA KUWA nchi zote ambao zimekubali kutia saini Itifaki hii zitakuwa tayari kushirikiana na nchi yetu katika kupambana na wahamiaji haramu;

NA KWA KUWA tutapata fursa ya kushirikiana na Jumuiya mbalimbali za Kimataifa katika ubadilishanaji wa taarifa kuhusu uvushaji haramu wa wahamiaji;

NA KWA KUWA tutapata msaada wa mafunzo ya kuwabaini wahamiaji haramu;

NA KWA KUWA amani na usalama wa nchi yetu itaimarika na hivyo kuweka mazingira mazuri zaidi ya uwekezaji raslimali;

NA KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado haijaridhia Itifaki hii;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Itifaki hii na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake wa 20 sasa linaazimia kuridhia Itifaki dhidi ya Uvushaji Haramu wa Wahamiaji kwa Njia ya Nchi Kavu, Maji na Anga *(The United Nations Protocol Against the Smuggling of Migrants by Land, Sea and Air)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Azimio la Itifaki ya Umoja wa Mataifa dhidi ya Uvushaji Haramu wa Wahamiaji kwa Njia ya Nchi Kavu, Maji na Anga liliridhiwa na Bunge)*

**Azimio la Kuridhia Itifaki ya Umoja wa Mataifa Dhidi ya Kuzuia, Kukataza na Kuadhibu Usafirishaji Haramu wa Binadamu hasa Wanawake na Watoto *(The United Nations Protocol to Prevent, Suppress and Punish Trafficking in Persons, Especially Women and Children)***

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako liridhie Itifaki ya Umoja wa Mataifa ya Kuzuia, Kukataza na Kuadhibu Usafirishaji Haramu wa Binadamu hasa Wanawake na Watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii nayo inatokana vile vile na Mkutano wa Palermo pamoja na Mkataba wa kuzuia Uhalifu wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la usafirishaji wa binadamu limekuwa likiongezeka katika dunia yetu na katika Mkutano ule lilipitishwa Azimio la kupambana nalo na kwa hiyo, naomba Bunge lako lipitishe Azimio la Kuridhia Itifaki hiyo. Azimio hilo linasomeka kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja kati ya nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa;

NA KWA KUWA lengo kuu la Itifaki hii ni kuzuia, kukataza na kuadhibu usafirishaji haramu wa binadamu hasa wanawake na watoto;

NA KWA KUWA nchi zote ambazo zimekubali kutia saini Itifaki hii zitakuwa tayari kushirikiana na nchi yetu katika ubadilishanaji wa taarifa za uhalifu na usafirishaji haramu wa binadamu;

NA KWA KUWA tutanufaika na mafunzo juu ya udhibiti wa usafirishaji haramu wa binadamu;

NA KWA KUWA kutakuwa na utaratibu wa pamoja wa kuwasitiri na kuwalinda waathirika wa usafirishaji haramu wa binadamu;

NA KWA KUWA amani na usalama wa nchi yetu itaimarika na hivyo kuweza kuweka mazingira mazuri zaidi ya uwekezaji raslimali;

NA KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado haijaridhia Itifaki hii;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa manufaa ya Itifaki hii na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake wa 20 sasa linaazimia kuridhia Itifaki ya Kuzuia, Kukataza na Kuadhibu Usafirishaji Haramu wa Binadamu hasa Wanawake na Watoto *(The United Nations Protocol to Prevent, Suppress and Punish Trafficking and Persons especially Women and Children)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Azimio la Itifaki ya Umoja wa Mataifa Dhidi ya Kuzuia, Kukataza na Kuadhibu Usafirishaji Haramu wa Binadamu hasa Wanawake na Watoto liliridhiwa na Bunge)*

**Azimio la Kuridhia Itifaki ya Umoja wa Mataifa dhidi ya Utengenezaji na Usafirishaji Haramu wa Silaha, Vipuri pamoja**

**na Sehemu zake na Risasi** ***(The United Nations Protocol against the Illicitly Manufacturing of and Trafficking in Firearms, their Parts and Components and Ammunition)***

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja Bunge lako liridhie Itifaki ya Umoja wa Mataifa dhidi ya Utengenezaji na Usafirishaji Haramu wa Silaha, Vipuri pamoja na Sehemu zake na Risasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Itifaki hii nayo inatokana na Mkataba ule ule wa Palermo ambao unahusu kukabiliana na uhalifu wa Kimataifa na kwa bahati nzuri Bunge lako Tukufu limeisharidhia Maazimio mawili. Moja ni la *SADC* na la pili ni la Nairobi, yaani kwa nchi za Afrika ya Mashariki na Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika zote kuhusiana na suala hili la utengenezaji na usambazaji wa silaha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nilisome Azimio ambalo napendekeza lipitishwe na Bunge lako Tukufu.

KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja kati ya nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa;

NA KWA KUWA lengo kuu la Itifaki hii ni kupambana na utengenezaji na usafirishaji haramu wa silaha, vipuri, pamoja na sehemu zake na risasi;

NA KWA KUWA nchi zote ambazo zimekubali kutia saini Itifaki hii zitakuwa tayari kushirikiana na nchi yetu katika ubadilishanaji wa taarifa kuhusu utengenezaji, usafirishaji na umiliki wa silaha kinyume cha sheria;

NA KWA KUWA tutanufaika na mafunzo juu ya udhibiti wa utengenezaji na umiliki wa silaha haramu;

NA KWA KUWA nchi zote zilizotia saini Mkataba huu zitakuwa tayari kushirikiana na nchi yetu katika kukabiliana na tatizo la utengenezaji na usafirishaji wa silaha na risasi kinyume cha sheria;

NA KWA KUWA amani na usalama wa nchi yetu utaimarika na hivyo kuweka mazingira mazuri zaidi ya uwekezaji raslimali;

NA KWA KUWA Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado haijaridhia Itifaki hii;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya Itifaki hii na kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake wa 20 sasa linaazimia kuridhia Itifaki dhidi ya Utengenezaji na Usafirishaji Haramu wa Silaha, Vipuri, pamoja na Sehemu zake na Risasi. *(The United Nations Protocol against the Illicitly Manufacturing of and Trafficking in Firearms, their Parts and Components and Ammunition).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Azimio la Itifaki ya Umoja wa Mataifa dhidi ya Utengenezaji na Usafirishaji Haramu wa Silaha, Vipuri pamoja na Sehemu zake na Risasi liliridhiwa na Bunge)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA (k. n. y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama; Mheshimiwa John Malecela, ningependa kwanza kabisa kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati kuhusiana na Azimio hili la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa. Maoni haya yametolewa kwa mujibu wa kanuni ya 43(5)(b) cha Kanuni za Bunge kama lilivyotolewa mwaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama ilikutana tarehe 21 Julai, hapa Dodoma kupokea na kujadili Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa *(The United Nations Convention Against Transnational Organized Crime)* ambao uliwasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi mbele ya Kamati hiyo. Pamoja na Mkataba huu, Kamati pia ilipokea na kujadili Itifaki tatu za Mkataba huu ambazo ni:-

(i) Itifaki ya Umoja wa Mataifa dhidi ya Uvushaji Haramu wa Wahamiaji kwa Njia ya Nchi Kavu, Maji na Anga *(The United Nations Protocol against the Smuggling of Migrants by Land, Sea and Air);*

(ii) Itifaki ya Umoja wa Mataifa ya Kuzuia, Kukataza na Kuadhibu Usafirishaji Haramu wa Binadamu hasa Wanawake na Watoto *(The United Nations Protocol to Prevent, Suppress and Punish Trafficking in Persons, Especially Women and Children);*

(iii) Itifaki ya Umoja wa Mataifa dhidi ya Utengenezaji na Usafirishaji Haramu wa Silaha, Vipuri pamoja na Sehemu zake na Risasi (*The United Nations Protocol Against the Illicitly Manufacturing of and Trafficking in Firearms, their Parts and Components and Ammunition).*

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la Mkataba huu na Itifaki zake ni Mkutano wa Milenia wa Viongozi wa Dunia waliokutana kuzungumzia mambo muhimu kwa ustawi wa binadamu katika karne ya 21. Hii ilitokana na ukweli kuwa wapo kwa mamilioni watu duniani kote wanaonyimwa haki za msingi za binadamu ikiwa ni pamoja

na haki za kuishi. Mkataba huu unalenga kuifanya dunia kuwa mahali salama pa binadamu kuishi kwa amani, bila hofu wala vitisho vinavyotokana na uhalifu dhidi ya binadamu na mali zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba huu na Itifaki zake unalenga kuweka utawala wa sheria utakaoleta ustawi kwa binadamu kwa kuzifanya nchi zitakazouridhia kushirikiana kwa pamoja katika kuzima na kutokomeza vitendo vyote vya uhalifu vinavyopangwa dhidi ya binadamu na mali zake. Vitendo vya uhalifu vinavyofanywa dhidi ya binadamu kama vile usafirishaji haramu wa wanawake na watoto, uvushaji haramu wa silaha na uvushaji haramu wa wahamiaji ni mambo yanayohitaji jitihada za pamoja za Kimataifa katika kuyakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge letu likiridhia Mkataba huu na Itifaki zake litawezesha nchi yetu kupata msaada wa Kimataifa katika kukabiliana na uhalifu kama huu mara utakapotokea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa jambo kama hili ni jambo lile lililotokea wakati tukiwa hapa, Wabunge wenzetu walioshiriki kufanikisha vitendo vinavyofanana na jambo kama hili. Siku hizi kuna biashara ya watoto na biashara ya ngono ambayo inafanana na utumwa. Kwa hiyo, Mkataba huu una lengo la kuzuia utumwa wa aina hiyo ambao umeibuka katika dunia ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni sehemu ya Umoja wa Mataifa na historia ya nchi yetu ni kwamba ilikuwa chini ya usimamizi wa Umoja wa Mataifa tangu mwaka 1919 hadi tulipokuwa huru mwaka 1961. Pia, Rais wetu ni mmoja wa Viongozi waliohudhuria Mkutano wa Dunia wa Milenia uliopitisha Mkataba huu.

Kutokana na manufaa ya kiusalama, kijamii na kiuchumi ambayo Tanzania itanufaika kutokana na kuridhia Mkataba huu na itifaki zake, Kamati ya Ulinzi na Usalama inashauri kwamba, Bunge hili liridhie Mkataba huu na Itifaki zake kwa pamoja ili Mkataba huu uweze kutekelezwa mapema iwezekanavyo kwa manufaa ya nchi yetu na ustawi wa watu wa dunia hii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote, napenda kusema kuwa naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu mkubaliane na mimi kwa uamuzi huu. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI (k. n. y. MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Naibu Spika, sitarudia majina ya Mikataba na Itifaki zinazoridhiwa, isipokuwa nitakwenda moja kwa moja katika maoni ili kuokoa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani kwa mara nyingine na ya mwisho katika kipindi hiki cha uhai wa Bunge, tunasikitishwa na kuletewa kwa Itifaki za

Kuridhia humu Bungeni kwa njia za kushtukiza. Hata hivyo, tunapenda kutoa maoni na ushauri kwa kila Azimio kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Uvushaji Haramu wa Wahamiaji kwa Njia ya Nchi Kavu, Maji na Anga, tunaishauri Serikali na Umoja wa Mataifa kuzingatia kuwa zipo sababu zinazosababisha biashara hii kuendelea kuwepo hasa ikizingatiwa kuwa wanaosafirishwa hutoka katika nchi maskini sana na zinazoendelea kwenda katika nchi tajiri sana na zilizoendelea kwa sababu hizi zifuatazo:-

(i) Umaskini uliokithiri katika nchi maskini;

(ii) Ukosefu wa ajira katika nchi maskini;

(iii) Ujira kidogo kwa matumizi katika nchi maskini;

(iv) Uroho wa baadhi ya watu katika nchi zilizoendelea wa kupata watumishi wa gharama nafuu *(cheap labour)* kutoka nchi maskini;

(v) Uroho wa baadhi ya wafanyabiashara katika nchi zilizoendelea wa kupata fedha kutokana na biashara ya binadamu ambayo inatokana na uendeshaji wa utumwa wa kisasa ambapo anayesafirishwa anapenda kwenda huko kwa hiari yake; na

(vi) Udhaifu wa vyombo vya usalama, kwani haiwezekani mtu kufanya biashara kama hiyo na asijulikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Usafirishaji Haramu wa Binadamu na Hasa Wanawake na Watoto, Kambi ya Upinzani inaona sababu ni zile zile zilizotajwa hapo juu, isipokuwa tunaongeza sababu nyingine ambazo ni:-

(i) Nchi zilizoendelea kupitisha na kuhalalisha sheria za uendeshaji madanguro na uchangudoa; na

(ii) Nchi zilizoendelea kuchochea migogoro na vita katika nchi maskini kwa nia ya kupata masoko ya silaha zao pamoja na kupata nafasi ya kupora maliasili na utajiri wa nchi maskini kama inavyofanyika huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na watoto wanatumika katika vita na kuendeleza vitendo vya kigaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza sababu hizi pamoja na nyingine zichunguzwe na kupatiwa ufumbuzi na ndipo hatua za udhibiti zifuatwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Utengenezaji na Usafirishaji Haramu wa Silaha, Vipuri pamoja na Sehemu zake, Kambi ya Upinzani inayo maoni yafuatayo:-

Waingereza wana msemo huu, *like father like son.* Kama ilivyo kwamba mtu mmoja hawezi kuishi pekee katika dunia hii, vile vile Taifa moja haliwezi kuishi peke

yake hapa duniani. Taifa moja au Mataifa matano hapa duniani yanakesha yakitumia fedha nyingi katika kutafiti na kutengeneza silaha za maangamizi za kiatomiki na kinyuklia kwa sababu zifuatazo:-

(i) Kisingizio cha kulinda nchi husika dhidi ya mipaka yake;

(ii) Kujipatia fedha kutokana na mauzo ya silaha; na

(iii) Kutisha Mataifa mengine ili kuyatawala kiuchumi, kisiasa na kidiplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ndivyo ilivyo kwa mtu mmoja au kikundi cha watu wachache wanaotengeneza silaha haramu na risasi ili:-

(i) Kufanyia ujambazi ili wajipatie mali;

(ii) Kuuza silaha hizo ili wajipatie fedha; na

(iii) Kulinda mitandao yao ya kijambazi dhidi ya vyombo vya ulinzi na usalama kama vile Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kutokana na hali hiyo kwamba dunia inapaswa kuungana na kutokomeza utengenezaji na usafirishaji wa silaha haramu, kwa upande wa Tanzania, Kambi ya Upinzani inashangazwa na jinsi Serikali inavyoshughulikia tatizo la silaha na ujambazi kwani kila siku majambazi wanateka magari, wanabomoa nyumba za raia, wanapora fedha kwenye mabenki na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi za Afrika Mashariki na Maziwa Makuu ni Tanzania inayosifiwa kuwa kisiwa cha amani, lakini mfano uko nchini Uganda ambako kuna vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa takriban zaidi ya miaka 15 sasa. Mabasi kutoka Dar es Salaam kupitia Nairobi, Kampala hadi Bukoba yanasafiri masaa 24, wakati huo huo magari kutoka Mwanza, Singida kuja Dodoma kwenda Dar es Salaam hayaruhusiwi kusafiri zaidi ya saa mbili usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi kama kweli Serikali kwa kutumia Mabalozi wa Nyumba Kumi, Wenyeviti wa Vitongoji, Serikali za Mitaa na Vijiji, Polisi na Usalama wa Taifa wanaweza kushindwa kuwabainisha, kuwatambua na kuwashughulikia wasafirishaji wa silaha haramu kama ambavyo Uganda imeweza kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano wa mtu ambaye ni Kiongozi wa Serikali akiwa Mtendaji wa Kata huko Wilayani Karagwe ambaye ameghushi na kuiba fedha za mirathi ya marehemu kaka yake aliyekuwa mtumishi wa Jeshi la Polisi kiasi cha Sh.2,670,000/= na kuziweka kwenye akaunti yake binafsi na kuzitumia. Tatizo hili kesi yake iko Mahakamni na sitaki kulitaja

.

Mheshimiwa Naibu Spika, ametumia Sh.900,000/= ya sehemu ya fedha hizo kununua bastola kutoka katika Serikali ambayo amekuwa akiitumia kutishia usalama wa raia. Mfano, mwaka 2000 alitumia silaha hiyo kumtishia mfanyabiashara katika eneo la Kabingo, Kijiji cha Kakanja Wilayani Karagwe na kumnyang'anya pombe yake aina ya bia na kuinywa na kumuumiza.

Mwaka 2001 ametumia silaha hiyo katika kuteka na kunyang'anya pikipiki na mali za kijana aitwaye Venance Maishomabi wa Kijiji cha Kitwe na kuzipeleka Mahakamani ambapo Mahakama ya Mwanzo Mabira iliamua kumrejeshea kijana huyo pikipiki yake na mali zake.

Mnamo mwezi wa Juni, 2005 mtu huyo huyo akiwa sasa amesimamishwa kazi baada ya kufunguliwa mashtaka ya kughushi na kukosa uaminifu ameendelea kutumia silaha hiyo kwa kumvamia kijana mmoja aitwaye Restides Ishengoma Valentine wa Kijiji cha Kitwe na kuvunja mlango wa nyumba yake, eti akimtafuta kumkamata.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na vituko vyote hivyo, Serikali haijamchukulia hatua zozote na yeye anapita akitamba kuwa yeye ni Afisa Usalama wa Taifa. Kwa hiyo, Serikali haiwezi kufanya chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mbunge ninajua Kanuni za Bunge na ninajua haki walizonazo raia walioko nje ya Bunge. Mtu niliyemtaja Mheshimiwa Waziri akitaka nitampatia jina lake, ninamjua na nipo tayari kushirikiana na Vyombo vya Dola kuthibitisha madai niliyoyatoa. Ni mategemeo yangu kuwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na Idara ya Usalama wa Taifa watapenda kunihoji ili waweze kupata ushahidi wa hayo niliyoyasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono Maazimio yote yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa saa ile iliyopo mbele yangu, bado dakika nne ambazo itabidi Mheshimiwa Waziri ajibu halafu mimi nihoji. Mimi kuhoji nahitaji kama dakika mbili. Kwa dakika nne, maana yake na yeye atajibu kwa dakika mbili, *which I think* hatutendei haki Bunge. Kwa sababu hiyo, itabidi sasa nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 Jioni.

*(Saa 06.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kikao kilichoanza asubuhi kinaendelea, Mheshimiwa Naibu Spika, aliniambia kwamba mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, hakupata nafasi ya kuhitimisha hoja yake. Kwa hiyo, nitampa nafasi hiyo, tuimalize hiyo hoja ndiyo tuendelee na mengine.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja yangu niliyowasilisha asubuhi ambapo niliwasilisha maazimio manne. Kutokana na muda sikupata wachangiaji lakini nilipata Waheshimiwa Wabunge wawili, aliyemwakilisha Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Jackson Makwetta na pia Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, kama Msemaji wa Upinzani.

Napenda nimshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Jackson Makwetta, kwa maelezo yake ambayo kwa kiasi kikubwa yalisaidia kufafanua hoja yangu kwa sababu ya kukimbilia muda mimi mwenyewe hotuba ilikuwa fupi kwani sikupata wasaa wa kufafanua. Lakini alipokuja Mheshimiwa Jackson Makwetta, alijaliza yale ambayo ningesema hata kabla ya hapo, aidha, namshukuru kwa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi, nakubaliana naye na uchambuzi wake wa sababu ambazo zinasababisha kuibuka kwa haya makosa tunayoyaona sasa hivi za Kimataifa kama suala zima la usafirishaji haramu wa uhamiaji na usafirishaji haramu wa watu, hasa wanawake na watoto kwenda kutumikisha kwa kazi chafu kama za kwenye madangulo na kazi za sulubu.

Nataka nitofautiane naye kwa uchambuzi wake aliotoa wa ndani hasa aliposema kwamba ujambazi unaongezeka, alipokuwa akijenga hoja hata alipotoa mfano wa Uganda kwamba pamoja na kwamba pamoja na kwamba kuna vita lakini mabasi yanasafiri mpaka usiku, kwetu hayasafiri usiku. Nilipowasilisha hotuba yangu ya Bajeti nilieleza na kuonyesha takwimu za jinsi makosa, uhalifu unavyopungua katika nchi yetu, angalau limepungua katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Nilisema uhalifu wa jumla umepungua kwa asilimia 20.4 na makosa yenye sura ya ujambazi yalipungua kwa asilimia 4.2.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, si kweli anaposema kwamba ujambazi unaongezeka, unapungua ingawa imekuwa kazi ndogo. Nina uhakika hiyo ilikuwa mpaka 2004. Nina hakika takwimu za 2005 zitakuwa nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu ya kupigwa marufuku kwa mabasi kusafiri usiku kama atakumbuka Mheshimiwa Benedicto Mtungirehi, amri ya kuyapiga marufuku mabasi kutembea usiku ilitolewa wakati wa awamu ya pili na ilikuwa ni kwa sababu ya ajali za barabarani ambapo uzoefu ulionyesha kwamba mabasi mengi yalikuwa yakipata ajali za kugongana na malori yalipokuwa yanasafiri usiku.

Kwa hiyo, zilikuwa ni jitihada za kupunguza ajali ambazo zilikuwa zikipotekeza maisha ya watu. Kwa vile bado ajali tunazo nyingi nadhani isingekuwa busara sasa hivi kuzungumza kuiondoa ile amri. Kwa hiyo, amri iliwekwa kwamba mabasi yatembee

mchana malori yatembee usiku. Si kwa sababu ya ujambazi, kwa hiyo, natofautiana naye hapo alipoliunganisha hili na ujambazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimepokea kesi yake aliyoilezea hapa na kwa bahati nzuri ameniwasilishia barua rasmi na nataka kumhakikishia kwamba tutaifuatilia na tutaichukua hatua kwa pale ambapo tutaona ipo haja ya kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache naomba nikushukuru tena na naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*( Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Umoja wa Mataifa Dhidi ya Uvushaji Haramu wa Wahamiaji kwa Njia ya Nchi Kavu, Maji na Anga *(The United Nations Protocol Against the Smuggling of Migrants by Land, Sea and Air)*

*(Azimio lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Bunge*
*bila mabadiliko yoyote)*

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Umoja wa Mataifa Dhidi ya Kuzuia, Kukataza na Kuadhibu Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Hasa Wanawake na Watoto *(The United Nations Protocol to Prevent, Suppress and Punish Trafficking in Persons, Especially Women and Children).*

*(Azimio lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Bunge*
*bila mabadiliko yoyote)*

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Umoja wa Mataifa Dhidi ya Utengenezaji na Usafirishaji Haramu wa Silaha, Vipuri pamoja na sehemu zake na Risasi *(The united Nations Protocol Against the Illicitly Manufacturing of and Trafficking in Firearms, their parts and components and Ammunition)*

*(Azimio lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Bunge*
*bila mabadiliko yoyote)*

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli tulizokuwa zimepangwa kwa ajili ya Mkutano wa Ishirini wa Bunge hili sasa zote zimeshashughulikiwa.

**SPIKA:** Kwa taarifa hiyo sasa namwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe hoja ya kuahirisha Bunge. *(Makofi)*

**KUFUNGA BUNGE**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, waswahili husema bandu bandu humaliza gogo. Bunge lako hili lilipoanza uhai wake mwezi Novemba, 2000, mwezi Julai, 2005 ulionekana uko mbali sana na wala hakuna aliyefikiria mwisho wa uhai wa Bunge hili kwa wakati huo. Kweli bandu bandu ya mkutano mmoja baada ya mwingine imemaliza gogo na uhai wa Bunge hili utatoweka hivi punde Mheshimiwa Rais atakapolivunja rasmi.

Mara nyingi ninapokuwa ninaahirisha Mikutano ya Bunge huwa ninawatahadharisha Waheshimiwa Wabunge, idadi ya mikutano iliyobaki. Huu ni Mkutano wa Ishirini, hivyo leo siahirishi Mkutano huu wa Bunge kwa sababu hakijabaki kitu. Kuja kwenye Mkutano mwingine ni majaaliwa ya Mola baada ya kushinda uchaguzi. Nina matumaini makubwa kwamba, ukiwaacha wale ambao hawatagombea, wengine wote mtatetea nafasi zenu kikamilifu na mtafanikiwa kurudi humu Bungeni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, leo tumehitimisha kazi zote zilizokuwa zimepangwa kutekelezwa katika Mkutano wa Ishirini wa Bunge lako Tukufu. Kuhitimishwa kwa kazi hizo ndiyo vile vile mwisho wa uhai wa Bunge hili lililoanza Novemba, 2000 kama nilivyokwishaeleza. Kesho Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, atalihutubia Bunge na hivyo kutamka rasmi tarehe ya mwisho ya uhai wa Bunge hili. Kama nilivyosema awali leo hakuna cha kuahirisha kwa ajili ya Mkutano mwingine bali Mheshimiwa Spika umeniruhusu na umeona ni vema walau niseme maneno machache ya shukrani na kutakiana kila la kheri katika harakati mbalimbali zilizoko mbele yetu. Nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii adhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa iliyotekelezwa katika Mkutano huu wa Ishirini ni kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2005/2006 pamoja na mpango wa muda mfupi na wa muda wa kati na mfumo wa matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2005/2006 hadi 2007/2008. Aidha, Bunge pia limeidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara na Idara zinazojitegemea kwa mwaka 2005/2006.

Bajeti ya Serikali ya mwaka huu kama ilivyosifiwa na umma na kuungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge, ni Bajeti nzuri na inayomlenga mwananchi wa kawaida na huku ikijenga misingi imara ya kukuza uchumi. Mafanikio yote tunayoyaona yametokana na Bajeti nzuri na usimamizi mzuri wa Bajeti zilizopitwa za Serikali.

Napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na timu yake ya wapangaji mipango na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba na timu yake ya upangaji wa Bajeti na usimamizi wake kwa kazi nzuri. Uchumi wetu umekuwa vizuri na mapato ya Serikali kuongezeka hadi tunazozungumzia Bajeti ya zaidi ya shilingi 4.176 trilioni kwa mwaka huu wa fedha. Nani angaweza kufikiria kuwa kuna siku Tanzania tunaweza kusomesha watoto wetu wote elimu ya msingi bure, tukajenga mamia ya kilometa za lami kwa fedha zetu na mengineyo mengi ya kujivunia? *(Makofi)*

Tanzania leo ni nchi ya kujivunia sana na wengi wanatambua hivyo, pamoja na wale waliokuwa wanatudharau huko nyuma. Nchi ambayo ilikuwa haina uwezekaji, leo inaongoza kwa kuvutia wawekezaji wa nje na wa ndani katika Kanda ya Mashariki na Kati ya Afrika. Aidha, nchi yetu imeendelea kuwa na amani na utulivu mkubwa chini ya mfumo wa demokrasia ya Vyama Vingi. Kwa haya yote na mengine mengi Watanzania tuna wajibu wa kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, pili kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa uongozi wake makini, Serikali yake, mihimili mingine ya dola yaani Bunge na Mahakama na mwisho lakini siyo kwa umuhimu wananchi wote wa Tanzania na washiriki wetu wa maendeleo ambao ndiyo wameshikana mikono na Watanzania katika shughuli mbalimbali za maendeleo na huduma na jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya tunayoyaona bado safari ni ndefu. Uchumi wetu bado ni mdogo japo unakua kwa kiwango cha kuridhisha cha asilimia 6.7 mwaka 2004. Kwa vigezo vya uchumi jumla *(macro economic indicators)* tuna nafasi ya kuendeleza ukuaji wa uchumi wetu kwa kasi zaidi. Watanzania tutumie fursa zilizoko katika kujiimarisha kiuchumi na kukuza uchumi wa Taifa letu. Nina hakika Serikali ijayo itaendeleza na kukuza fursa hiyo kwa kasi na nguvu mpya zaidi. Kuna mambo ya msingi ambayo lazima Watanzania tuyafanye ili tufanikiwe katika ulimwengu huu wa biashara huria na utandawazi. Jambo la msingi ni la kufanya kazi. Hili ni tatizo kubwa kwa Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengi wanadhani kazi ni lazima iwe ajira ya mshahara tu. Kazi ni pamoja kilimo, ufugaji, uvuvi na kadhalika. Shughuli hizi na nyingine zinazofanana nazo tunatakiwa tuzifanye kwa ufanisi na kibiashara. Watalaamu wetu lazima wawasaidie wananchi. Kwa mfano, hapana haja ya kuendelea kulima mazao ambayo bei yake katika soko la dunia ni duni na haitabiriki au mazao ambayo mkulima hutumia gharama kubwa sana kuyakuza na hivyo kubakiwa na faida kidogo au hata kupata hasara kila mwaka. Suala la kuongeza ubora na uwingi wa mazao na kuongeza thamani kwa kuyasindika nayo lazima ipewe msukumu wa kutosha. Ili haya yafanikiwe ni lazima tujiondoe pole pole kutoka kilimo cha kujikimu na kwenda kwenye kilimo cha biashara hasa kwa kuongeza ukubwa wa mashamba yetu na kuwa cha mashamba makubwa na ya kati.

Mheshimiwa Spika, aidha, hata pale ambapo mashamba ni madogo kwa ajili ya uhaba wa ardhi, sura ya kilimo lazima ibadilike na kuwa cha kisasa. Uzalishaji katika kilimo ukiongezeka tutakuwa na mazao bora na mengi zaidi ya kuyasindika na kuyauza nje. Kilimo kikiwa cha uhakika zaidi pia tutaachana na tatizo la uhaba wa chakula wa mara kwa mara, jambo ambalo ni aibu kwa mtu yeyote na Taifa lolote. Watanzania ni lazima tujilishe wenyewe na tusidhani kuomba chakula hata kutoka Serikalini ni fahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila mtu mwenye nguvu akifanya kazi kwa bidii na maarifa na kwa kuzingatia ushauri wa wataalam, siyo kwamba tu tutakuwa na chakula cha kutosha, bali na mazao mengi ya kuuza nje, umaskini utatoweka na malalamiko ya kukosa ajira nayo pia yatatoweka. Naomba sisi wanasiasa tuwahimize hasa vijana wetu

kujiingiza katika ajira ya kilimo badala ya kukimbilia kwenye adha za Mijini na kuishi vijiweni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wale wachache waliobahatika kupata ajira katika Kampuni binafsi zilizowekeza nchini, kuna tatizo kubwa sana la migomo na hata kufikia kufunga baadhi ya viwanda. Hali hii ni hatari sana kwa ukuaji wa uchumi wetu na ajira zetu. Hali hii ama itawafukuza wawekezaji au kwa wale watakaovumilia, watatoa ajira kwa wafanyakazi kutoka nchi jirani ambao hawana utaratibu huu wa migomo isiyo na misingi. Ni lazima soko letu la ajira ielewe kuwa tupo katika uchumi unaoongozwa na sekta binafsi na soko la ajira nalo litahurishwa muda si mrefu katika Jumuiya zetu za Kikanda. Ni lazima tujue kuwa taratibu za ajira na utendaji kazi sasa ni tofauti na zile tulizozoea katika Mashirika yetu ya umma ambapo kwa sehemu kubwa ndizo zilizochangia sana kufa kwa Mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, katika sekta binafsi upunguzaji wa wafanyakazi hauepukiki kama hali ya kibiashara ni mbaya, katika sekta binafsi kupeana viwango vya kazi hakuepukiki, katika sekta binafsi kukatwa siku kwa vile hukuwepo kazini ndiyo wajibu na katika sekta binafsi kunyimwa ruhusa fulani fulani ni utaratibu na kadhalika. Haya yote Watanzania tujue ndiyo dini ya sekta binafsi, kiwe ni kiwanda cha Mhindi, Mwarabu, Mzungu, Mwafrika, Mtanzania, lugha au dini ni hiyo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine muhimu ni kwa Watanzania kuzalisha na kuuza nje. Bila kuongeza sana mauzo yetu ya nje ni vigumu sana kujenga utajiri ndani ya nchi. Serikali ijayo nina hakika itaendeleza uboreshaji wa fursa hizi, hivyo wananchi wazitumie kikamilifu. Eneo lingine pia muhimu sana ili Serikali iendelee kuboresha huduma zake kwa wananchi ni la kuongeza mapato yake. Watanzania ni lazima tujenge utamaduni wa kulipa kodi zinazostahili, nchi nyingi ambazo Serikali zao zimejenga uwezo mkubwa wa mapato zimefanya hivyo kwa sababu wananchi wao wanatekeleza wajibu wao wa kulipa kodi. Aidha, nchi hutoa adhabu kali sana kwa wakwepaji wa kodi. Katika nchi yetu tulikuwa tunaelimishana umuhimu wa kulipa kodi na kwamba ni wajibu wa mwananchi kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na elimu hiyo ya muda mrefu, bado wapo baadhi ya wafanyabiashara ambao wanauliza wateja kama wanataka stakabadhi au la. Kama stakabadhi itatolewa, bei ya bidhaa huwa juu kuliko kama stakabadhi haihitajiki. Jambo hili linatakiwa lipigwe vita kwa nguvu zote. Wafanyao hivi wanatuibia, wanarudisha nyuma juhudi za Serikali za kuboresha huduma kwa umma na wanakwamisha upanukaji wa biashara nchini kwa kuwafilisi wale wanaotoa stakabadhi kwa kuwapiku kibiashara. Ni vema wao wakafilisiwa kabla hawajaua biashara katika nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilvyogusia awali, bila kupata uwekezaji kutoka nje na ndani uchumi wetu utadumaa na tubaki nyuma. Ni lazima tukuze uwekezaji na tuone ndiyo uhai wa uchumi wetu. Tusithubutu hata kidogo kuhujumu uwekezaji. Nchi zote zilizoendelea na zinazoendelea zinapigania kuvutia wawekezaji. Wawekezaji hawa wakishajijenga katika nchi fulani ni vigumu sana kuwapata.

Aidha, nchi yetu ikiachwa na wawekezaji, itapata sifa mbaya na kwa kutumia utandawazi huu wa kisasa, sifa hiyo huenea haraka sana duniani kote na ni vigumu sana kuifuta au kuirekebisha. Hivyo, ni vyema sera zetu na matendo yetu yakawa yanavutia uwekezaji. Uwekezaji siyo ule wa nje tu bali hata wa ndani. Leo kuna fursa nyingi za uwekzeshaji ambazo Watanzania wanatakiwa wazichangamkie. Ningependa kuwaasa Watanzania tuchamgamkie fursa zinazotokana na mikakati na mipango mbalimbali ya Serikali kama vile MKUKUTA na MKURABITA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo ni mengi sana yanayowahusu wananchi na yanayoihusu Serikali, lakini kwa leo nimeona nitaje hayo machache. Mengi nimekuwa nikiyazungumzia katika hotuba zangu mbalimbali hapa Bungeni na kwinginepo.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu mwaka huu tuna Uchaguzi Mkuu nchini. Mchakato wa shughuli za uchaguzi zimefikia hatua muhimu na ulimwengu mzima unatuangalia jinsi gani tutakavyoendesha shughuli hii muhimu ya uchaguzi. Hivi sasa baadhi ya vyama vimekwishawateua wagombea wao wa kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kile cha Rais wa Zanzibar na mwaka huu inaelekea tutavunja rekodi kwa watu wengi kugombea nafasi kubwa katika Taifa letu. Hadi sasa kuna wagombea tisa kwa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wagombea sita kwa nafasi ya Rais wa Zanzibar. Aidha, baadhi ya vyama vimekwishawateua hata wagombea Ubunge na Udiwani. Napenda kuvipongeza vyama vyote ambavyo vimekamilisha hatua hizo kwa njia ya demokrasia na ninawapongeza wote walioteuliwa na vyama vyao hasa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye ameteuliwa na Chama cha Mapinduzi kugombea Kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Jakaya Kikwete, tunakutakia ushindi wa kishindo. Hatuna shaka utaweka nguvu mpya, kasi mpya na ari mpya katika kuendeleza mapambano ya Watanzania dhidi ya umaskini na *Inshallah* tutashinda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, vyama vingine bado vinaendelea na harakati za kukamilisha uteuzi ndani ya vyama. Kadri muda wa kuanza kampeni unapokaribia ndivyo vyama vya siasa vitakavyojitahidi kutimiza masharti yote ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ili viweze kuwaweka wagombea katika nafasi mbalimbali zinazogombewa. Jukumu kubwa linalotukabili ni kuhakikisha kuwa harakati za kisiasa za vyama hazisababishi uvunjifu wa amani na kwamba tunahitimisha mchakato wote wa uchaguzi kwa amani na utulivu. Napenda kutumia fursa hii kupongeza hatua zinazochukuliwa na viongozi kwa vyama vya siasa nchini za kujenga mazingira ya maelewano yatakayotuwezesha kufanya uchaguzi wetu kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wito wangu kwa Watanzania ni kuwa waepuke siasa za chuki, siasa za kidini, ukabila au siasa za vurugu na fujo. Sote sisi ni ndugu na umoja wa Kitaifa tulioujenga kwa kipindi cha miaka 44 ni kielelezo cha jinsi tulivyoweza kupiga vita mambo yote yanayohatarisha umoja na mshikamano wa Taifa letu. Sipendi kurudia rudia kuwa Serikali itapambana vikali na watakaofanya fujo katika Uchaguzi Mkuu ujao, lakini kweli ndivyo itakavyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika tutafute ridhaa ya umma kwa haki bila fujo, vitisho, ujanja wala rushwa. Tuwape raha wananchi waamue wakipendacho na wao wanajua wakipendacho. Vyama vya Siasa na Watanzania tuone faraja kuendelea kuwa kisiwa cha amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama taarifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi inayoonyesha jumla ya Watanzania 15,958,801wamejiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Napenda kutumia fursa hii kuwaomba wale wote waliojiandikisha kuendelea kutunza kadi zao za kupigia kura ili waweze kuzitumia wakati wa kupiga kura. Aidha, wote waliojiandikisha wajitokeze kutekeleza wajibu wao wa kuwachagua viongozi watakaoweza kuendeleza kazi kubwa na nzuri iliyotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tatu. Napenda niwahakikishie Watanzania wote kuwa Serikali itashirikiana kwa karibu sana na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuipa uwezo kifedha na kitaalamu ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Hata hivyo, napenda nisisitize kuwa ushirikiano huo hautaingilia majukumu wala uhuru wa Tume na Serikali itazingatia kwa makini matakwa yote ya kisheria kuhusu uendeshaji wa uchaguzi. Nataka niseme kuwa suala la uendeshaji na usimamizi wa uchaguzi ni la Serikali kwa kupitia Tume ya Uchaguzi na wala siyo la chama chochote cha siasa. Vyama vya Siasa ni wadau na washiriki tu katika shughuli hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge ni moja ya mihimili mitatu ya dola. Kwa matakwa ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 63(2), Bunge ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano, ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii. Hivyo Bunge ni taasisi muhimu sana na ni kielelezo cha maendeleo yote yanayotokea nchini, kielelezo cha demokrasia na kielelezo cha utawala bora katika Taifa lolote.

Bunge ndiyo sauti ya wananchi kwani kwa kupitia Bunge ndipo wawakilishi wa wananchi wanapofikisha hoja na maswali mbalimbali yanayohusu maendeleo yao Serikalini. Serikali yoyote inayojali na kuzingatia demokrasia lazima kila wakati isikilize na iyapatie majibu hoja na maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Katika majibu hayo Serikali huwaza kutoa maelezo au kufafanua masuala mbalimbali na kufanya hivyo wananchi wanaelewa jinsi Serikali yao inavyotekeleza majukumu ya kuwasaidia kujiletea maendeleo au kutoa huduma mbalimbali. Kwa kutumia chombo hiki wananchi hujua jinsi fedha za kodi zao zinavyotumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, katika maendeleo tunayojivunia Tanzania, Bunge hili ni sehemu muhimu sana ya mafanikio hayo. Waheshimiwa Wabunge hawa ndio waliosimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru sana kwa ushirikiano huo na kwa ushauri mlioipa Serikali ambayo haikuyapuuza, bali iliyafanyia kazi yote mliyoyashauri. Hongereni sana na asanteni sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge hili ni la pili baada ya mfumo wa vyama vingi vya siasa kuanzishwa hapa nchini. Nchi yetu imepata uzoefu sasa wa jinsi Bunge lenye Wawakilishi wa wananchi kutoka vyama mbalimbali linavyofanya kazi. Napenda kukiri kuwa tumefanikiwa kulifanya Bunge letu kuwa kielelezo thabiti cha demokrasia na uvumilivu wa kisiasa. Ndani ya Bunge, kila upande umeweza kujenga hoja mbalimbali kuhusu masuala ya maendeleo ya nchi yetu na ukasikilizwa. Wengi wamepewa lakini na wachache nao wamesikilizwa. Tumepingana kwa hoja na wala hapajawahi kutokea vurugu au ugomvi miongoni mwetu hapa Bungeni. *(Makofi)*

.Mheshimiwa Spika, hata pale upande mmoja ulipokataa kuunga hoja inayoungwa na upande wa pili, nje ya jengo hili ulikuta Wabunge wa pande hizo zilizopingana wamekaa pamoja wakishirikiana kwa kila hali kuonyesha kuwa kupingana kwa hoja za kisiasa siyo uadui, bali ni kujenga na kudumisha demokrasia. Vielelezo vya namna hii ni tabia halisi ya Watanzania. Katika nchi nyingine tumeshuhudia kwenye televisheni au kusoma kwenye magazeti jinsi Wabunge wanavyokosa uvumilivu kiasi cha kupigana ndani ya Ukumbi wa Bunge na nje ya Bunge ni vigumu kukuta Wabunge wa pande zinazopingana kukaa pamoja. Napenda nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuonyesha ukomavu mkubwa wa kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wito wangu kwa wale wote miongoni mwenu mtakaobahatika kurudi ndani ya ukumbi huu, ni kuwa muwe walimu kwa wale watakaokuwa wageni ili Bunge letu liendelee kuwa chimbuko la majadiliano na maamuzi ya mustakabali wa nchi yetu, yanayojengwa kwa nguvu ya hoja na kwa uvumilivu wa kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuimarika kwa Bunge kama chombo cha uwakilishi wa wananchi kumeamsha ari kubwa miongoni mwa wananchi. Wananchi wamekuwa ni wafuatiliaji wakubwa wa shughuli zote za Bunge zinazoendelea katika kila Mkutano. Wanasikiliza vipindi mbalimbali vinavyorushwa na redio na televisheni na vile vile kusoma magazeti yenye maelezo ya shughuli za Bunge. Kutokana na mafanikio hayo upo mwamko mkubwa sasa wa wananchi kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uwakilishi hususan Ubunge na Udiwani. Hali hii ni njema sana kwa nchi yetu kwani tunajenga misingi imara ya demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wanatambua sasa thamani ya kura yao na kwamba ni muhimu kufanya maamuzi sahihi wakati wa uchaguzi. Waheshimiwa Wabunge mmekuwa chachu katika mabadiliko hayo na hilo ni moja ya mafanikio makubwa ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ninayoyazungumza yasingepatikana kama tungekuwa hatuna mfumo mzuri wa uongozi na uendeshaji wa shughuli za Bunge. Katika kipindi cha miaka kumi, chini ya mfumo wa vyama vingi, tumefanikiwa kuweka kanuni na taratibu za uendeshaji Bunge ambazo kwa kiwango kikubwa zimeweza kukidhi matakwa na matarajio yetu. Inawezekana bado upo upungufu katika baadhi ya maeneo, lakini kila mara tunajifunza kwa kukabiliana na masuala yanayojitokeza kwa kubuni majibu yake na kujenga mfumo endelevu wa kukifanya chombo hiki cha uwakilishi wa wananchi kutekeleza majukumu yake vema.

Mheshimiwa Spika, uongozi bora una mchango mkubwa sana katika mafanikio ya taasisi yoyote. Napenda nikiri kuwa Bunge letu limepata sifa kubwa ndani na nje ya nchi hii kutokana na uongozi thabiti na mahiri wa Spika, Mheshimiwa Pius Msekwa. Mheshimiwa Pius Msekwa ni kiongozi na mwalimu. Ameweza kutumia uwezo na uzoefu wake katika kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Yeye ndiye amekuwa chachu katika kuweka taratibu za uendeshaji wa vikao vya Bunge. Busara na hekima zake mara kwa mara zimeliwezesha Bunge kufikia maamuzi hata pale ilipoonekana kuwa mambo ni magumu sana. Ucheshi wake vile vile umeweza kulichangamsha Bunge na hivyo kila mmoja wetu akajituliza na kuendelea na shughuli za majadiliano ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Pius Msekwa amekuwa vile vile kama rejea muhimu ya shughuli za Bunge. Uzoefu wake wa muda mrefu wa uendeshaji wa shughuli za Bunge na umahiri wake wa kufanya rejea kwa Mabunge katika nchi za Jumuiya ya Madola umemwezesha kutumia uzoefu huo katika kuliongoza Bunge letu. Sote tunaona fahari sana ya kuwa na Spika kama yeye katika Bunge letu. Napenda nitumie fursa hii kwanza kumpongeza, pili, kumshukuru na tatu kumtakia afya njema na mafaniko makubwa katika maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, Mbunge wa Tunduru, amekuwa msaidizi wako wa karibu sana katika kipindi chote cha miaka mitano. Amekuwa mwepesi kujifunza na ameonyesha uwezo mkubwa wa kuongoza shughuli za Bunge. Aidha, Wenyeviti wote wawili, Mheshimiwa Anne Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini na Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi wameweza nao kumudu shughuli za uongozi wa Bunge kwa ufanisi mkubwa. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru kwa kubeba

majukumu waliyokabidhiwa na Mheshimiwa Spika vyema na kwa ustadi mkubwa. Bunge hili sasa lina hata uwezo wa kutoa wataalam wa uongozi wa shughuli za Bunge kwa Mabunge mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi zako za uendeshaji wa shughuli za Bunge na kazi za Serikali za kuleta Miswada Bungeni zingekuwa ngumu sana kama siyo kwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu na Wajumbe wa Kamati zao kutekeleza wajibu wao kikamilifu. Kamati hizi zimechambua kwa umakini na kina Miswada yote na Bajeti za kila Wizara jambo ambalo limerahisisha sana mijadala hapa Bungeni. Aidha, Serikali nayo imechukulia kwa umakini huo ushauri wa Kamati hizo na kuuzingatia kwa kadiri ilivyowezekana, jambo ambalo limejenga kuaminiana sana baina ya Bunge na Serikali. Ninawashukuru sana Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shughuli za Bunge zimasimamiwa na Tume ya Huduma za Bunge. Tume yetu imefanya kazi vizuri sana na imetimiza wajibu wake. Kwa uchapaji wake kazi, maslahi ya Bunge na Wabunge yamelindwa kikamilifu. Aidha, chombo hiki hiki huangalia pia Bajeti ya Ofisi ya Spika kabla ya kupelekwa katika hatua zingine za mbele. Waheshimiwa Wabunge tunaridhika sana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa ili kuboresha mazingira ya Bunge letu. Ujenzi wa majengo ya kisasa ya Ofisi za Dar es Salaam na Zanzibar na ujenzi unaoendelea hapa Dodoma wa ukumbi mpya wa kisasa ni ushahidi tosha wa haya ninayoyaeleza. Napenda kuipongeza na kuishukuru sana Tume ya Huduma za Bunge chini ya Uenyekiti wako Spika, kwa kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watumishi wa ofisi yako wakiongozwa na Katibu wetu wa Bunge wamefanya kazi kubwa sana kutuhudumia. Chini ya uongozi wa Katibu wa awali ambaye sasa ni Jaji Kipenka Musa na sasa chini ya Ndugu Damian Foka, shughuli za ofisi yako zinaendeshwa kwa umakini sana. Sisi Wabunge wa pande zote yaani Wabunge wa viti vya nyuma na Wabunge wa viti vya mbele, tunaridhika sana na huduma zao. Ninawapongeza sana watumishi wote. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, shughuli za Bunge zisingetulia kama Serikali haikutimiza wajibu wake ipasavyo. Napenda kwanza niwashukuru sana Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri ambao mimi kama kiongozi wao wamenipa ushirikiano na utii wa hali ya juu sana.Mafanikio yote tunayoyaona katika kila sekta yameongozwa na hawa askari wa miavuli. Kwa kweli hawa ni askari wa miavuli waliotua katika uwanja wa kazi wakikimbia. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa ushirikiano mlionipa na kwa uchapaji kazi wenu. Waheshimiwa hawa wameweza kufanya kazi hizo kwa ufanisi kwa sababu wamesaidiwa na timu za wataalam katika Wizara zao na utumishi wa Serikali kwa ujumla. Namshukuru sana Katibu Mkuu Kiongozi, Ndugu Marten Lumbanga na Makatibu Wakuu wote kwa kuongoza timu hii ya wataalam. Napenda kuwashukuru sana kwa ushirikiano na uchapaji kazi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo watu na ofisi zao ambao hawavumi lakini wapo. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya kazi kubwa sana katika kufanikisha shughuli za Serikali Bungeni na shughuli za Bunge pia. Napenda nimshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali na timu yake ya wataalam kwa kazi hiyo nzuri. Kipekee

napenda kumtaja Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mheshimiwa Andrew Chenge ni mchapa kazi wa pekee sana. Ukiachilia mbali uwezo wake mkubwa wa kujua sheria, ni mtu ambaye hachoki kufanya kazi. Mimi nimefanya naye kazi, hata usiku wa manane ukimwita yuko tayari kwa kazi. Lakini ni mshauri mkweli wa Serikali kwa mambo ya Sheria na hata mambo mengine yanayoendana nayo. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Andrew Chenge na Mungu akujalie huko uendako. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inasifika sana kama kisiwa cha amani. Kwa Watanzania walio wengi ungewauliza wanathamini sana nini katika nchi yao, watakujibu amani na utulivu tulio nao. Tuna amani nchini na tunaishi kwa amani na maelewano na jirani zetu wote. Haya yote yapo kwa sababu kuna walinzi wa amani na utulivu huo. Napenda kuvishukuru vyombo vyote vya dola vinavyosimamia ulinzi wa amani yetu. Hawa ni pamoja na Jeshi la Ulinzi, Majeshi ya Usalama wa raia na Idara ya Usalama wa Taifa. Wote kwa kushirikiana na wananchi wametekeleza wajibu wao kikamilifu. Nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kukamilisha utawala bora ambao nchi yetu inaongoza sasa kwa sifa hiyo Kimataifa Barani Afrika, Idara ya Mahakama nayo imefanya kazi nzuri sana. Hali ya kesi kucheleweshwa au mazingira ya rushwa yaliyokuwa yanalalamikiwa sana na umma yamebadilika na kuwa bora sana. Napenda kumpongeza sana Jaji Mkuu, Mheshimiwa Barnabas Samatta na wote wanaomsaidia kwa kazi nzuri ambayo mahakama inafanya kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vyombo vya habari vimefanya kazi kubwa na nzuri katika kipindi chote cha uhai wa Bunge hili. Wananchi wamepata habari na kuelewa maamuzi mbalimbali yaliyopitishwa na Bunge hili kwa vile vyombo vya habari vimetekeleza wajibu wao kikamilifu. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati wamiliki wa vyombo vya habari, wahariri na waandishi wa habari kwa kutekeleza wajibu huo kikamilifu. Yapo mabadiliko makubwa ya utoaji wa habari za shughuli za Bunge hivi sasa ukilinganisha na hali ilivyokuwa huko nyuma. Wito wangu kwa waandishi wa habari ni kuwa waendelee kuwa wabunifu na wanaopenda kusoma na kutafiti kwani kwa kufanya hivyo wataweza kila mara kuandika habari zenye uwiano sawa na zinazowaunganisha Watanzania katika harakati zao za kupambana na umaskini.

Katika kipindi cha kuelekea Uchaguzi Mkuu, vyombo vya habari vina majukumu mazito zaidi. Vyombo hivi ndivyo vyenye uwezo wa kutoa mchango mkubwa wa kuwaelimisha Watanzania na kuwapa habari kuhusu mustakabali wa Taifa letu na sifa za viongozi wanaofaa kuliongoza Taifa.

Napenda kuviasa vyombo vya habari vijiepushe na habari za uongo, za uzushi, zenye kuegemea upande mmoja kwa sababu za binafsi au zilizoelekezwa na rushwa. Habari zenu katika kipindi hiki ziwahamasishe wananchi kuimarisha umoja wa Kitaifa na kuwaelimisha kuwa uchaguzi ni mchakato tu wa kutupatia viongozi na wala usitumike kutugawa. Tuelewe kuwa vyombo hivi vinaweza kutumika kujenga chuki, uhasama na hata uvunjifu wa amani. Aidha, vyombo hivi vielewe kuwa vipo na vinafanya kazi zao

kwa sababu kuna amani. Amani ikivurugika vyombo hivi navyo vitatoweka. Tujihadhari sana na kutia moto kichaka kinachotuhifadhi yaani amani yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana wote walioshirikiana nasi kwa namna moja au nyingine. Hawa ni nchi marafiki, Mashirika ya Kimataifa, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Makampuni binafsi, Wawekezaji mbalimbali na hata watu binafsi waliotupa ushauri na kadhalika. Kwa wote nasema ahsanteni sana kwa sababu chochote kile chema walichokifanya kimeongeza uwezo wa Serikali kuwahudumia Watanzania au uwezo wa Watanzania kujihudumia wenyewe. Kwa wote nasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sote katika nafasi zetu mbalimbali tumekuwa tunafanya tuliyoyafanya kwa ajili ya wananchi wa Tanzania. Tumefanikiwa kwa sababu tumepata ushirikiano wao. Kama mazao yamezalishwa vizuri Watanzania ndiyo wamelima, kama bidhaa zimetengenezwa na kuuzwa nje wao ndiyo wamefanya kazi ya uzalishaji na kadhalika.

Aidha, hata amani tuliyonayo ni Watanzania wameshirikiana na vyombo husika pale ambapo palitaka kujitokeza tatizo. Hivyo, napenda kuwashukuru Watanzania wote kwa ushirikiano wao na uelewa wao. Kwa ushirikiano huo nina uhakika nchi yetu itazidi kufanikiwa katika medani zote za maisha. Nawashukuru sana sana Watanzania katika ujumla wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizi sasa naomba nitoe shukrani zangu binafsi kwa wafuatao, kwanza, naomba nimshukuru tena kwa dhati Rais wetu mpendwa sana Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa imani kubwa aliyonayo kwangu kwa kipindi chote cha Serikali ya Awamu ya Tatu. Imani yake ya kuniteua mara mbili kuwa Waziri Mkuu nitaienzi siku zote. Mimi chini ya uongozi wake nimejifunza mambo mengi sana. Nimejifunza uongozi, lakini pia nimejifunza uvumilivu. Rais Benjamin Mkapa, ni mvumilivu sana na mimi sasa ni mvumilivu pia. Rais Benjamin Mkapa ni msikivu sana, nami sasa ni msikivu pia na hatimaye Rais Benjamin Mkapa sasa anastaafu na mimi ninastaafu pia. *(Makofi)*

Pili, nawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa heshima kubwa mliyonipa ya kuthibitisha uteuzi wangu Novemba ,2000 na hata ule wa mwaka 1995 kwa wale walioshiriki kipindi kile nawashukuru pia kwa ushirikiano nilioupata kutoka kwa kila mmoja wenu katika kipindi chote ambapo nimekuwa Waziri Mkuu na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni ana majukumu siyo tu ya kusimamia na kuratibu shughuli za Serikali Bungeni, lakini vile vile analo jukumu la kujenga mshikamano na ushirikiano baina ya makundi yote ya Wabunge ndani na nje ya Bunge. Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wangu yametokana na ushirikiano nilioupata kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Kwa kutumia Katiba, Wabunge wanaweza kumpigia Waziri Mkuu kura ya kutokuwa na imani naye na hivyo hata kuangusha Serikali. Miaka kumi ya ushirikiano mkubwa haikutupeleka karibu na hapo. Miaka hiyo imejenga zaidi undugu na kuaminiana baina ya Serikali na Bunge. Naamini uhusiano utaendelea kwa Waziri Mkuu ajaye na Serikali ijayo. Ninawashukuru na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba nikushukuru sana wewe binafsi. Hakika umekuwa mwalimu wangu mkubwa katika shughuli hizi za uongozi wa Bunge. Kutoka kwako nimejifunza mengi na umeniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi mkubwa. Nasema ahsante sana. Napenda pia kuwashukuru sana wasaidizi wako wa karibu, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Katibu wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu ina majukumu mengi sana. Kama nimetekeleza majukumu yangu na naamini nimeyatekeleza vinginevyo nisingekuwa Waziri Mkuu kwa miaka yote kumi, ni kwa ajili ya msaada niliopewa na wale walio karibu nami. Ni kwa ajili ya msaada niliopewa na wale walio karibu na mimi. Napenda niwataje Mawaziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib na Mheshimiwa William Lukuvi, ambao wamenishauri na kunisaidia sana. Napenda pia niwashukuru wataalam wa Ofisi ya Waziri Mkuu wakiongozwa na Katibu Mkuu Bibi Rose Lugembe ambao wamenishauri na kunisaidia bila kuchoka. Watumishi wa Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu wakiongozwa na Katibu wa Waziri Mkuu, Ndugu Sulle Michael Sella nao wamefanya kazi yangu kuwa nyepesi. Kwa hawa wote ninawashukuru sana, nasema asanteni sana kwa uaminifu wenu kwangu na nne, napenda nikishukuru sana Chama changu, Chama cha Mapinduzi (CCM) ambacho kimeniwezesha kukitumikia na kutumikia wananchi wa Tanzania. Nakitakia kila la kheri kuendelea kuongoza nchi hii. Ninakipongeza sana kwa kuongoza demokrasia ya kweli ndani ya vyama na hata katika nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tano, naomba niwashukuru mno wananchi wa Jimbo la Hanang kwa imani kubwa waliyonionyesha kwa kipindi cha miaka 20 niliyowatumikia.Wao ndio walionipa nguvu ya kutekeleza majukumu yote ya Kitaifa niliyokabidhiwa. Napenda niwahakikishie kuwa nitaendelea kushirikiana nao ili tuweze kumpata Mbunge atakayeendeleza kazi kubwa na nzuri tuliyoifanya pamoja katika kipindi hicho. Naomba waendelee kuamini kuwa siri ya maendeleo siku zote ni uongozi wa pamoja kushirikiana na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sita, naomba nimshukuru sana mke wangu Esther na familia yangu yote kwa uvumilivu wao na kwa kunipa nguvu ambayo imeniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Wao wamekuwa watu wa msaada mkubwa sana hasa pale nilipozidiwa na majukumu ya Kitaifa na wao, hasa Esther akabeba majukumu ya familia. Ahsante sana Esther kwa uvumilivu na ushupavu wako. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni binadamu na ninaowaongoza ni binadamu pia. Katika mazingira ya kufanya kazi kwa pamoja tena kwa miaka mingi hivyo, ni kawaida sana binadamu kukosana au kuhitiliafiana kwa hoja au kupishana kwa kauli au hata matendo yetu. Kwa yale yaliyotokea humu Bungeni, inawezekana mijadala iliingiza vijembe ambavyo huenda havikuwapendeza wale waliokuwa wanalengwa.Lakini napenda kuwahakikishia kuwa hakuna kati yetu aliyekuwa na nia mbaya, yote hayo yalikuwa ni sehemu ya siasa za ndani ya ukumbi huu. Kila aliyekuwa anatoa mchango wake aliutoa kwa dhamira safi ya kutetea maslahi ya Taifa na ya wale waliompa kura. Yawezekana pia mtu akachukizwa tu na mazingira na hasira akambembesha Waziri Mkuu maana ndiye Kiongozi Mkuu wa Serikali hapa Bungeni.

Karatasi ya mshahara *(Salary Slip)* inaweza ikasoma kiwango usichokifurahia ukakasirika, Jimboni kwako inawezekana hampendani na Mkuu wako wa Wilaya au Mkurugenzi Mtendaji, ukanikasirikia Waziri Mkuu au ulitarajia kupata madaraka fulani hukuyapata, ukanikasirikia na kadhalika. Kwa hiyo, inawezekana kabisa nimekusababisha maumivu bila kujua wala kukusudia. Kwa yote ya namna hiyo na yanayofanana nayo naomba kutoa wito kwenu nyote kuwa leo tunapohitimisha shughuli zenu tusameheane na nakutakieni kila la kheri kwenye mapambano ya kisiasa yaliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya hayapo tu hapa Bungeni bali hata nje ya Bunge, katika kutekeleza majukumu mazito ya Ofisi ya Waziri Mkuu haiwezekani uwe umempendeza kila mtu, wapo walioathirika na uamuzi wa Serikali wa jumla au ambao nimeutoa, mimi lakini yote ni kwa nia njema. Wapo waliotaka msaada kwa ajili ya shida fulani, nikashindwa kuwatekelezea na wapo waliotaka labda upendeleo fulani, nikawakatalia hao wote na wengineo lazima wamepata maumivu ya aina fulani, nao naomba wanisamehe huo ndio ungwana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimetaja makundi mbalimbali katika kuwashukuru, inawezekana kabisa nimeyasahau mengine na wala nisingeweza kuyamaliza yote. Kwa wale wote ambao nimewasahau au sikuwataja basi wajue ni kwamba sikuwa na nafasi ya kutosha na naomba nawao wachukue kwamba nimewashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa wengi wa Waheshimiwa Wabunge wanatetea nafasi zao katika Majimbo yao ili warejee tena Bungeni, aidha, wapo wachache ambao wameamua kwa hiari yao wenyewe kwamba hawatagombea tena nafasi ya Ubunge, hao ninawatakia maisha mema, afya njema, amani huko waendako katika maisha yao mbele ya safari. Kwa wale wanaogombea, ninawatakia kila jema katika safari hii ya kusaka kura za wananchi. Kwa uhakika kwa ninyi nyote kila mmoja katika jimbo lake hakuna anayekuudhidi kwa kufahamika. Hivyo hapana sababu za wasiwasi mkubwa, ninawatakia kila jema na ikiwezekana nyote mtetee nafasi zenu na mrudi katika Bunge lijalo. Nyote ninawatakia safari njema ya kurudi Majimboni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii uliyonipa ya kuwaaga wenzangu na pia kuwaaga Watanzania kwa ujumla. Baada ya salaam hizi za kuagana, naomba sasa kutoa hoja kuwa Bunge lako sasa liahirishwe hadi kesho saa tatu kamili asaubuhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kuamua hoja hiyo kuna mambo mawili ya matangazo tu, la kwanza ni *Chief Whip* wa Serikali ameniomba niwatangazie Wabunge kwamba ile tafrija ya Waziri Mkuu nadhani iliwekewa saa kwenye kadi, sasa wanasema ni vizuri tukaenda moja kwa moja tukitoka hapa kuliko kwenda nyumbani na kurudi na kwenye tafrija hiyo tulimwomba naye akakubali Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, awe ndio *Master of Ceremony. (Makofi)*

Pili, Waheshimiwa Wabunge kwa mazingira ya kesho Kamati iliyokuwa inafanya maandalizi imetoa kadi kwa wageni watakao kuja kwenye *gallery* kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais, wamejaza *gallery* zote, kwa hiyo, wameniomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge msije na wageni binafsi kwa sababu watakosa viti kwenye *galleries*, wameshapangiwa kadi na kwa kuzingatia usalama utakavyokuwa hali ya juu kesho tuna wakuu wote wa nchi, basi bila kadi mtu hataruhusiwa kuingia, basi nimeombwa nieleze tusije na wageni wetu binafsi na la tatu ni hilo nililolitaja kwamba kesho wale viongozi wa kawaida ambao huja kuungana na sisi wakati Rais anapohutubia Bunge watakuwepo, nao ni Makamu wa Rais, Jaji Mkuu yaani mihimili yote ya dola inakuwa pamoja hapa, tunautaratibu wa kuwaombea ruksa ya kuingia kwenye ukumbi wale ambao sio Wabunge. Kwa hiyo, ningeomba kazi hiyo tuifanye sasa, nimwombe *Chief Whip* wa Serikali atoe hoja ya kuomba ruksa kwa wale wakuu watakaokaa kwenye jukwaa la Spika, waweze kuingia katika Ukumbi wa Bunge.

## HOJA YA KUWARUHUSU VIONGOZI WASIOKUWA WABUNGE KUKAA KATIKA UKUMBI WA BUNGE WAKATI RAIS AKIHUTUBIA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE.WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, kwa mujibu wa Kanuni ya 114 ya Kanuni zetu za Bunge, naomba kutoa hoja Bunge lako Tukufu litoe idhini ya viongozi wafuatao kuingia ndani ya ukumbi ili waweze kujumuika na Waheshimiwa Wabunge katika kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nao ni Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais na Jaji Mkuu Mheshimiwa Barnabas Samata. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Mahofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge lilitoa idhini kwa Viongozi hao kukaa ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

**SPIKA:** Baada ya hapo sasa tunarudi kwenye hoja na kuahirisha Bunge mpaka kesho, tuamue hoja hiyo. Amesema mtoa hoja kwamba Bunge liahirishwe mpaka kesho asubuhi saa tatu na ni saa tatu kwa sababu gani tunasoma Dua halafu ndio tunatoka nje kumpokea Rais, kwa sababu yeye Rais amepangiwa kuanza hotuba yake saa nne kamili asubuhi.

Kwa hiyo, atafika kama saa nne kasoro robo hivi na kawaida yetu huwa tunakuwa pale kwenye ngazi kumpokea, anakagua gwaride la polisi ili kusudi saa nne maandamano ya Spika, pamoja na Rais mwenyewe tunaingia ili tuanze kusikiliza hotuba yake ifikapo saa nne kamili asubuhi. Kwa hiyo, tunaomba tukusanyike, tuwasili hapa saa tatu kama kawaida kwa ajili ya Dua na mengine yatakayokuwepo ya kuelezana hapo kesho.

*(Saa 12.12 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Ijumaa*
*Tarehe 29 Julai, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*